**OORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

**MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA**

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Ali Abdalla Ali | Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini. |
| 2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa | Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni. |
| 3. Mhe. Mgeni Hassan Juma | Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake. |
| 4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais. |
| 5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani. |
| 6. Mhe. Omar Yussuf Mzee | MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais. |
| 7. Mhe. Haji Omar Kheri | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/JimbolaTumbatu |
| 8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais. |
| 9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais. |
| 10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary | MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni. |
| 11. Mhe. Rashid Seif Suleiman | MBM/ Waziri wa Afya/Jimbo la Ziwani. |
| 12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban | MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais. |

| | |
|---|---|
| 13.Mhe. Juma Duni Haji | MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Kuteuliwa na Rais. |
| 14.Mhe. Zainab Omar Mohammed | MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais. |
| 15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan | MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni. |
| 16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge. |
| 17.Mhe Dr. Sira Ubwa Mamboya | MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Kuteuliwa na Rais. |
| 18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui | MBM/Waziri wa Biashara,Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni. |
| 19.Mhe. Said Ali Mbarouk | MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando. |
| 20.Mhe. Haroun Ali Suleiman | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi. |
| 21.Mhe. Haji Faki Shaali | MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni. |
| 22.Mhe. Machano Othman Said | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni. |
| 23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole. |
| 24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) | Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka. |

| | |
|---|---|
| 25. Mhe. Zahra Ali Hamad | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake. |
| 26.Mhe.Mahmoud Thabit Kombo | Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki |
| 27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake. |
| 28.Mhe. Haji Mwadini Makame | Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi. |
| 29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi | Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni. |
| 30.Mhe. Mohammed Said Mohammed | Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae. |
| 31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak | Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake |
| 32.Mhe. Said Hassan Said | Mwanasheria Mkuu. |
| 33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla | Jimbo la Chonga |
| 34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali | Jimbo la Mkoani |
| 35.Mhe. Abdi Mosi Kombo | Jimbo la Matemwe |
| 36.Mhe. Ali Mzee Ali | Kuteuliwa na Rais |
| 37.Mhe. Ali Salum Haji | Jimbo la Kwahani |
| 38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Nafasi za Wanawake |
| 39.Mhe. Asaa Othman Hamad | Jimbo la Wete |
| 40.Mhe. Asha Abdu Haji | Nafasi za Wanawake |
| 41.Mhe. Asha Bakari Makame | Nafasi za Wanawake |
| 42.Mhe. Ashura Sharif Ali | Nafasi za Wanawake |

| | |
|---|---|
| 43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 44.Mhe. Farida Amour Mohammed | Nafasi za Wanawake |
| 45.Mhe. Fatma Mbarouk Said | Jimbo la Amani |
| 46.Mhe. Hamad Masoud Hamad | Jimbo la Ole |
| 47.Mhe. Hamza Hassan Juma | Jimbo la Kwamtipura |
| 48.Mhe. Hassan Hamad Omar | Jimbo la Kojani |
| 49.Mhe. Hija Hassan Hija | Jimbo la Kiwani |
| 50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu | Jimbo la Bububu |
| 51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu | Jimbo la Mji Mkongwe |
| 52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub | Jimbo la Muyuni |
| 53.Mhe. Kazija Khamis Kona | Nafasi za Wanawake |
| 54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | Jimbo la Kitope |
| 55.Mhe. Marina Joel Thomas | Kuteuliwa na Rais |
| 56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) | Jimbo la Mkwajuni |
| 57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma | Jimbo la Bumbwini |
| 58.Mhe. Mohammed Haji Khalid | Jimbo la Mtambile |
| 59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali | Jimbo la Uzini |
| 60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi | Jimbo la Chambani |
| 61.Mhe. Mussa Ali Hassan | Jimbo la Koani |
| 62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | Nafasi za Wanawake |
| 63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi | Nafasi za Wanawake |
| 64.Mhe. Nassor Salim Ali | Jimbo la Rahaleo |

| | |
|---|---|
| 65.Mhe. Omar Ali Shehe | Jimbo la Chake-Chake |
| 66.Mhe. Panya Ali Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 67.Mhe. Rufai Said Rufai | Jimbo la Tumbe |
| 68.Mhe. Raya Suleiman Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 69.Mhe. Saleh Nassor Juma | Jimbo la Wawi |
| 70.Mhe. Salim Abdalla Hamad | Jimbo la Mtambwe |
| 71.Mhe. Salma Mohammed Ali | Nafasi za Wanawake |
| 72.Mhe. Salma Mussa Bilali | Nafasi za Wanawake |
| 73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman | Nafasi za Wanawake |
| 74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha | Jimbo la Mwanakwerekwe |
| 75.Mhe. Subeit Khamis Faki | Jimbo la Micheweni |
| 76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis | Jimbo la Konde |
| 77.Mhe. Suleiman Othman Nyanga | Jimbo la Jang'ombe |
| 78.Mhe. Ussi Jecha Simai | Jimbo la Chaani |
| 79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir | Nafasi za Wanawake |

**Ndugu Yahya Khamis Hamad** **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

**Kikao cha Tano – Tarehe 21 Mei, 2015**

*(Kikao Kilianza saa 3:00 za asubuhi)*

**Dua**

*Mhe. Naibu Spika ( Ali Abdalla Ali) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

**Nam. 24**

**Ujenzi wa Jengo Jipya la Baraza la Wawakilishi, Pemba**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub: (Kny: Mhe. Saleh Nassor Juma)** – Aliuliza:-

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabla ya yote nichukue fursa hii kumpa pole Mhe. Mwakilishi wa Wawi, kutokana na hali yake ya kuumwa ndio maana hajahudhuria kwenye vikao. Kwa hivyo, wananchi wa Jimbo la Wawi ikiwemo Kibokoni, Umangani, Vitongoji na Ufikiwa niwape pole kwa kutokuwepo Mwakilishi wao, lakini tunamsaidia baadhi ya hizi kazi zake. Naomba muhusika wa swali hili liliopo mbele yetu kutokana na umuhimu wake lipate jawabu muda huu.

Kwa kuwa zamani vikao vya Baraza la Wawakilishi vilikuwa vikifanyika sehemu zote mbili za Zanzibar kwa mpangilio maalum. Kwa kuwa katika kipindi hichi cha 2010/2015 Baraza lilitakiwa lifanye angalau vikao vichache kisiwani Pemba, lakini ikashindikana kutokana na Ukumbi wa Baraza kukosa kiwango, na hivyo kuendelea kufanya ukarabati katika majengo na Ukumbi wa Baraza ulioko Pemba.

Je, ni lini Serikali itajenga jengo jipya la Baraza la Wawakilishi Pemba badala ya kuendelea kukarabati majengo ya kurithi.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais** – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 24 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kweli katika miaka ya nyuma palikuwa na utaratibu wa kufanyika kwa Vikao vya Baraza la Wawakilishi katika Kisiwa cha Pemba. Lakini utaratibu huu kwa muda sasa haujafanyika kutokana na hali ya jengo letu la Pemba kutoridhisha kutokana na hali halisi ya uchakavu.

Mhe. Naibu Spika, napenda ifahamike kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, haina dhamira ya kuondoa vikao vya Baraza hili Tukufu kufanyika Pemba, bali ni kutokana na ukumbi wa Baraza uliopo Wete Pemba kukosa viwango vinavyohitajika kwa sasa, unahitaji ukarabati mkubwa ili kukidhi mahitaji hayo.

Mhe. Spika, hata hivyo serikali ina mpango wa kulifanyia ukarabati mkubwa jengo hilo pamoja na kuweka samani na vifaa vya kisasa kwa ajili ya shughuli za Baraza kisiwani Pemba.

Mhe. Naibu Spika, serikali imechukua hatua za kufanya makisio ya ukarabati wa ukumbi huo, ambapo jumla ya shilingi 370,648,620/- zitahitajika kwa ajili ya ukarabati huo, mara zitakapopatikana fedha hizo kazi itaanza. Kwa sasa tayari tumeweza kufanya ukarabati wa ofisi za watendaji wa Baraza huko kisiwani Pemba.

Mhe. Naibu Spika, serikali haina mpango wa kujenga jengo jipya, bali nia na dhamira ni kulikarabati jengo liliopo sasa, ili lifikie viwango vinavyohitajika kwa ajili ya shughuli za Baraza la Wawakilishi.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu muafaka ya Mhe. Waziri dhamana wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, nichukue fursa hii kumpongeza.

Mhe. Naibu Spika, kumbukumbu zinaonesha ni vikao vingi tu vimefanyika katika jengo hilo hilo. Je, ni viwango gani vimekosekana hadi jengo hilo kupoteza sifa kutotumika na kusababisha kutoleta sura nzuri iliyowekwa na serikali, kufanyia baina ya visiwa vyetu viwili vya Unguja na Pemba. Hilo moja.

Pili, kwa kutokufanyika vikao Pemba kunapunguza mzunguko wa fedha kwa wananchi wa Kisiwa cha Pemba, na ni haki yao ya msingi ukizingatia kufanywa vikao Baraza la Wawakilishi kule Pemba. Ni lini hizo shilingi 350 milioni zitapatikana kutoka serikalini ili kupatikana mzunguko wa fedha kule katika Kisiwa cha Pemba.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema awali, sababu kubwa iliyopelekea kupoteza viwango vya jengo letu ni uchakavu wa jengo lenyewe, na vifaa vilivyokuwemo ndani na vifaa vile vya mawasiliano vya kusikilizia. Kwa sababu Mhe. Naibu Spika, unajua kabisa kwamba Baraza linahitaji kuwa na vifaa vya mawasiliano hasa kwenye upande wa Hansard, vikalio kwa ajili ya Wajumbe wenyewe na jengo lenyewe kuwa zima.

Kwa sasa jengo linahitaji ukarabati mkubwa, hata paa lake linaonesha kuvuja na baada ya sisi kulitembelea tukaona hali hiyo, tukaridhika kabisa kwamba kwa hali ile haitofaa kufanyiwa vikao vya Baraza.

Lakini uamuzi wa serikali ni kwamba jengo hilo lifanyiwe ukarabati mara moja, ili liweze kukidhi viwango na liweze kutumika kwa shughuli za Baraza Kisiwani Pemba. Tunaujua umuhimu wake, lakini kama unavyojua Mhe. Naibu Spika, na Waheshimiwa Wajumbe, mwaka huu ni mwaka wa uchaguzi, kuna mahitaji mengi ya kiserikali. Kwa hivyo, bajeti zetu nyingi za kimaendeleo zimepunguzwa ili kukidhi haja iliyo mbele yetu. Lakini mara zitakapopatikana fedha, basi ujenzi utaanza Kisiwani Pemba, ili jengo hili lilioko Pemba liweze kutumika kwa ajili ya shughuli za Baraza letu Tukufu.

**Mhe. Subeit Khamis Faki:** Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa na mimi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa utaratibu huu wa kufanya vikao Unguja na kufanya vikao Pemba, ni mzuri na ulikuwa unaleta haiba kwa nchi yetu na kujenga pia mshikamano wa nchi yetu baina ya Unguja na Pemba.

Kwa kuwa jengo letu ni la zamani, na Mhe. Waziri anasema kwamba linahitaji kufanyiwa ukarabati, kwa kuwa jengo hili ni la zamani na hadhi yake ya ukumbi kwa sasa hailingani na hadhi ya kufanyia mikutano kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Je, Mhe. Waziri haoni kama kuna haja ya kujenga upya ukumbi, sio kuufanyia ukarabati, kuujenga upya ili ukijengwa upya utaendana na hadhi na utaendana na majengo ambayo yatakuwa yanafanana na ukumbi wa Baraza la Wawakilishi, pamoja na maofisi zaidi ya Hansard na nyengine kuweka karibu, ili kuendana sawa na Baraza la Wawakilishi, kuliko kufanya ukarabati.

Kama hivyo ndivyo, ni lini hasa serikali imepanga kuufanyia ujenzi ukumbi huo, ili vikao viendelee kufanyika Pemba?

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba ni utaratibu mzuri sana wa kujenga Baraza letu Unguja na Pemba pale ambapo inatokea haja ya kufanya hivyo. Hakuna asiyeona umuhimu huo na sote humu ndani tunapenda vikao vyetu hivi vifanyike katika ukumbi wa kule Wete Pemba.

Lakini kama nilivyosema awali Mhe. Naibu Spika, kwamba kutokana na hali halisi ya jengo, imebidi tusimamishe vikao vyetu kwa muda, mpaka pale tutakapofanya ukarabati mkubwa kwa ajili ya jengo lile.

Mhe. Naibu Spika, ukarabati ambao tunakwenda kuufanya ni mkubwa, kiasi ambacho niseme ni kujenga upya, kwa sababu sio tu tutakarabati, lakini pia tutaongeza kuta, kwa sababu paa lile liko chini nia yetu ni kupandisha zaidi ukuta na kuweka paa jipya na kufanya marekebisho kila pale ambapo panahitaji marekebisho, ili sura yake irudi kuwa ya upya kabisa. Sio kwamba ukarabati wenyewe ni wa juu juu, na kwa sababu jengo lenyewe chini ni madhubuti sana, wataalamu wetu wamelifanyia uchunguzi wa kutosha, wakaona umadhubuti wake.

Mhe. Naibu Spika, mimi mwenyewe, Spika, Katibu na watendaji tulikwenda huko tukaliangalia na tukaona umuhimu kwamba unapolifanyia ukarabati kwa utaratibu ambao wataalamu wametwambia, basi haiba na sura ya jengo letu lile litarudi upya na litatumika vizuri. Naamini utakuwa ni ukumbi mzuri kuliko huu ambao sisi tumo leo.

**Mhe. Omar Ali Shehe:** Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi nikauliza swali moja la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais au Baraza la Wawakilishi sasa hivi linamiliki kumbi tatu. Huu tulionao sasa hivi, ule wa Mnazi Mmoja pale ambao tulitoka mwaka jana na ule wa Wete ambao tunauzungumza hapa kwa Kisiwa cha Pemba.

Mhe. Naibu Spika, Taifa linahitaji kuwa na kumbi katika kuendesha shughuli zake mbali mbali za kitaifa, ambazo sasa hivi tutakubaliana kwamba ukiachia mbali ukumbi huu, ukumbi wa Mnazi Mmoja na ukumbi ule wa Wete hauwezi ukatumika katika shughuli za kitaifa.

Sasa na kwa kuwa vile vile mbali ya shughuli za kitaifa, Zanzibar tuna matatizo ya ukumbi hata kwenye shughuli za kijamii. Bajeti yetu hii ya Makamu wa Pili wa Rais ilitwambia kwamba moja kati ya mapato yaliyotegemewa ni kutokana na ukumbi wa Mnazi Mmoja ambao hayakupatikana kwa sababu ya uchakavu.

Sasa je, hivi serikali haioni kwamba kuzidharau kumbi hizi itakuja kupelekea kama vile kuanguka kwa jengo lile ambalo kumbi tulikuwa tukiutumia wa Chachani ambao sasa hivi unaanguka.

Lakini pili, katika bajeti ya mwaka huu programu imeingiza angalau shilingi ngapi katika kuona angalau tunazifanyia *first aid* kumbi hizo mbili, angalau kuja kuzifanya zisigeuke ule ukumbi maarufu wa Chachani ambao sasa hivi unaporomoka kwa kasi kubwa.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Naibu Spika, ni kweli kabla ya kuhamia hapa Baraza hili liliazimwa ukumbi na serikali katika ukumbi wa Mnazi Mmoja. Ukumbi ule hasa haukuwa wa Baraza la Wawakilishi, isipokuwa ulikuwa ni ukumbi wa serikali ukawaazima Baraza la Wawakilishi kutumia kwa ajili ya shughuli za Baraza, na baada ya kuhamia Chukwani ukumbi ule ulirudishwa serikalini.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa kuna mazungumzo yanaendelea kati ya Baraza na serikali, ili kuona nani atakuwa mmiliki rasmi wa ukumbi ule, lakini kwa sasa mwenye kumiliki ni serikali. Hapo tutakapomaliza kukubaliana nani atamiliki, itakuwa ni utaratibu wa baadaye ambao tutakubaliana. Lakini jitihada za kuutengeneza ukumbi ule zipo, ili kama alivyosema Mhe. Omar Ali Shehe, uweze kuzalisha mapato ambayo yatakidhi kwa njia moja au nyengine haja ya kusaidia shughuli za kiserikali.

Kwa hivyo, utaratibu upo wa kufikiria kuutengeneza ukumbi ule, lakini kama nilivyosema awali, mwaka huu Mhe. Naibu Spika, ni mwaka wa uchaguzi na una mambo mengi yaliyotukabili katika kuyatekeleza. Kwa hivyo, katika programu zetu kwa kipindi cha mwaka huu kwa ukumbi ule hatukuweka fedha nyingi kwa ajili ya matengenezo, isipokuwa tumeweka fungu dogo la matengenezo madogo madogo kufanyia ukarabati, huku tukisubiri kupata mradi mkubwa wa kufanya matengenezo katika ukumbi ule wa Baraza la Wawakilishi la zamani, ili nao uwe katika haiba yake.

Hata hivyo, yapo mazungumzo ya Baraza hili Mhe. Naibu Spika, kutaka ukumbi ule ubaki wa kihistoria kutokana na matumizi yake yaliyofanyika ya Baraza hili. Kwa hivyo, baada ya maamuzi ya pamoja ndio hasa tutafikia uamuzi muafaka.

**Nam. 7**

**Kutolewa Elimu ya Utawala Bora**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub: (Kny: Mhe. Saleh Nassor Juma)** - Aliuliza:-

Utawala bora ni moja kati ya idara muhimu sana katika serikali, kwani ina jukumu la kutoa elimu ya uraia kwa wananchi wote wa Zanzibar, kupitia njia tofauti, kwani wamekuwa wakishindwa kupata haki zao za msingi kutokana na ukosefu mkubwa wa elimu hiyo.

Je, ni kwa kiasi gani Idara ya Utawala Bora imetoa mafunzo ya elimu ya uraia kwa wananchi, hususan wanawake na watoto katika kupambana na udhalilishaji wa

kijinsia na jinsi ya kutetea haki zao mahakamani wanazoendelea kuzikosa siku hadi siku.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora** - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 7 kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Utawala Bora imeweka utaratibu maalum wa kutoa elimu ya uraia na haki za binadamu kwa jamii. Katika utoaji wa elimu hiyo vipindi mahususi pia hugusia masuala ya udhalilishaji wa kijinsia wanawake na watoto. Aidha, Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto pia hutoa elimu kama hiyo kwa umma. Katika kupambana kikamilifu na uovu huu, serikali imeanzisha kamati za kupambana dhidi ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia katika ngazi ya Taifa hadi shehia, pamoja na kuzijengea uwezo kamati hizo.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka 2014/15 pekee Idara ya Utawala Bora imetoa elimu ya uraia na haki za binadamu kwa kamati saba za Shehia za Kitope, Mbuzini, Mkokotoni, Upenja, Tunguu, Kizimbani na Muyuni.

Aidha, elimu kama hiyo pia imetolewa kwa wananchi wa Shehia 18 za Unguja na kurusha hewani vipindi 22 vya redio na vipindi 13 vya televisheni. Mipango imo njiani sasa kutoa elimu kama hiyo kwa Shehia za Pemba.

Ofisi yangu Mhe. Naibu Spika, inaendelea kufanya kazi kwa pamoja na Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto, pamoja na Wizara ya Katiba na Sheria, kwa lengo la kupambana kwa nguvu zote dhidi ya udhalilishaji wa kijinsia na jinsi ya kutetea haki zao mahakamani.

Aidha, serikali kwa kupitia Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto, imeandaa mpango wake wa kampeni ya kitaifa wa miaka mitano kuzuia udhalilishaji. Kampeni hii ambayo ilizinduliwa rasmi na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tarehe 06 Disemba, 2014 inaitwa, Ukatili na Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto Zanzibar sasa basi.

Mpango huu unavishirikisha vyombo mbali mbali, vikiwemo asasi za kiraia kama *ZAFELA* na Viongozi wa Dini, vile vile washirika wa maendeleo wakiwemo *UNICEF, UNFPA,* na *Save the Children* pia wameshirikishwa kikamilifu. Ahsante.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Tatizo kubwa la udhalilishaji

wa wanawake na watoto ikiwemo wa ubakaji, ni mfumo wa uchunguzi wa kesi na kukosekana uadilifu katika usimamiaji wa kesi na maamuzi. Je, serikali imechukua hatua gani za kuondoa rushwa na urasimu kwa vyombo vya kusimamia sheria, ili lengo la kuondoa tatizo hilo liweze kupatikana.

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Jaku Hashim Ayoub, rudia tena swali Mhe. Waziri hakufahamu, hakusikia kabisa.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Naibu Spika, tatizo kubwa la udhalilishaji wa wanawake na watoto ikiwemo ubakaji, ni mfumo wa uchunguzi wa kesi na kukosekana uadilifu katika usimamiaji wa kesi na maamuzi yake.

Je, serikali imechukua hatua gani kuondoa rushwa na urasimu kwa vyombo vya kusimamia sheria ili lengo la kuondoa tatizo hilo liweze kupatikana?

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora:** Mhe. Naibu Spika, kwanza namuomba sana Mhe. Jaku Hashim Ayoub tushirikiane katika suala hili. Hili sio suala la vyombo vya serikali na Mahakama peke yao. Kuna kesi nyingi sana zinazotokezea lakini wanasema tuyamalize wenyewe, sasa kidogo haipendezi. Ninachoomba sana mambo hayo yakitokezea basi vyombo vya sheria vifuate mkondo wake.

Lazima tuwapongeze *ZAFELA*. *ZAFELA* ni Jumuiya ya Wanasheria Wanawake au kwa kizungu wanasema *Zanzibar Female Lawyers Association*. Kwa kweli wao ni watetezi wakubwa sana, na wao wanatoa Mawakili bila ya malipo kutetea kesi hizi. Kwa hivyo kama kuna ubabaishaji ubabaishaji basi wanasheria hawa wanasimama na pia kuna wanaharakati nao wapo mstari wa mbele kuhakikisha kwamba udhalilishaji wa mambo kama haya yanazimwa mara moja na kuondosha kabisa matatizo hayo.

**Mhe. Shadya Mohammed Suleiman:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kuweza kunipatia nafasi hii na mimi kuweza kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Je, Mhe. Waziri, kwa elimu hii ya uraia nini maoni yako kuhusu vitendo vya udhalilishaji kwa watoto, vimepungua.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora:** Mhe. Naibu Spika, kwa ujumla kesi zinazoripotiwa kwa kweli zimepungua. Hata hivyo iko haja kubwa kwamba kama nilivyomjibu Mhe. Jaku Hashim, kwamba kesi zinazotokea mitaani wengine kwa sababu ya kuogopa suala la kunyanyapaa basi wanazimaliza

huko huko. Lakini mitaani tunapata habari kwamba vitendo bado vipo, lakini kesi zilizoripotiwa kwa kweli kwetu ni chache mno.

Nitatoa mfano kuanzia Januari mpaka Machi mwaka 2015 jumla ya kesi tano za udhalilishaji wa watoto kutoka katika Mahakama ya Watoto zimetolewa hukumu. Vile vile kwa kipindi hicho kesi zipatazo kama 85 zinaendelea kusikilizwa katika Mahakama tofauti za Wilaya. Kwa hivyo kiwango kinachozungumzwa au hatua zinazochukuliwa kwa kweli kesi zimepungua.

Pia naomba tuwapongeze sana Majaji na Mahakimu wetu, kesi zile zikija sasa hukumu wanazozitoa ni kali mno, kiasi cha kuwafanya hawa wanaofanya vitendo hivyo waogope. Kwa hivyo tunashukuru sana kwa hatua zao, waendelee na uzi huo huo.

**Mhe. Subeit Khamis Faki:** Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, kunipa fursa nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza lenye (a) na (b).

Mhe. Naibu Spika, suala la vitendo vya udhalilishaji wa watoto vinaendelea na bado havijasita katika nchi yetu. Sasa kwa kuwa hivyo ndivyo, kesi nyingi za udhalilishaji wa watoto zinakosa kuhukumiwa kutokana na kukosa ushahidi kwa wananchi wa Zanzibar kuwa woga na kukosa elimu ya kutoa ushahidi. Sasa Mhe. Waziri pamoja na majibu yake mazuri aliyosema kwamba kuna Shehia 18 za Zanzibar ambazokuwa zimepewa elimu.

a) Katika elimu hiyo ya Shehia hizo wanaopewa elimu wananchi kuwa na ujasiri wa kuunga mkono au kutoa ushahidi pindi inapotokea kesi ile. Kwa sababu moja ya kufeli kwa kesi ni kukosa ushahidi. Je, hilo limo la kuwaunga mkono wananchi kuwaelimisha ili kutoa ushahidi pindi inapotokezea kesi.

b) Kwa kuwa kesi hizi zikiripotiwa zinakwenda Polisi, na kuna baadhi ya askari polisi wanakuwa wanawasaidia wale wanaofanya vitendo vya udhalilishaji na ikifika kesi pengine askari polisi anaitoa huku na huku wakaitolea mlango wa nyuma. Je, kuna hatua gani zitachukuliwa kwa askari polisi aliyebainika akimsaidia mtu ambayekuwa amefanya udhalilifu na kumpa sheria ili kumuokoa na wakati akiwa ameshafanya udhalilishaji kwa wanawake au watoto.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora:** Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba watu wengi wamekuwa hawapendi kutoa ushahidi katika masuala haya, ndio lile suala nililolisema wengine zaidi wanakwepa ule unyanyapaa unaotokea baadaye wa kuoneshana vidole.

a) Kwa hivyo mimi nafikiri kama nilivyosema elimu yetu kwa kweli tuizidishe, na kama nilivyosema kuna mabaraza yale ya kwenye Shehia sasa mabaraza yale tutazidi kuyapa nguvu zaidi ili watu wetu washiriki ipasavyo na walifahamu kwamba tuna tatizo na inabidi sote tushirikiane tuliondoe tatizo hili. Hilo ndio suala la msingi na ningekuomba Mhe. Subeit Khamis kwa nafasi yako kama Mwakilishi tujumuike katika kuwashajihisha wananchi wetu, akina mama, akina baba na hasa vijana. Bado vijana ndio wanaotupa matatizo, japo zinatokea kesi nyengine ni za watu wazima lakini zaidi vijana.

b) Kuhusu polisi hili ni suala la uwajibikaji, kama wao wamepewa dhamana ya kusimamia na kutunza ushahidi, sasa wao ndio wanaoupotosha kwa kweli hapo sasa wanakhalifu sheria na inabidi na sisi sasa tuwaandame kwa vikali kabisa, na pindipo wakipatikana wanaofanya hayo basi hatua kali wachukuliwe dhidi yao.

**Nam. 69**

**Utangazaji wa Zabuni Katika Eneo la Darajani**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub -** Aliuliza:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilitunga Sheria ya Zanzibar na Manunuzi ili kuweka msingi wa usawa na haki pale serikali inapotaka kukodisha au kuuza mali yake ili jambo hilo lifanyike kwa ushindani na uwazi na lengo ni kufikia misingi ya Utawala Bora.

a) Je, ni sababu gani zilopelekea Wizara kushindwa kufungua zabuni ya ukodishwaji wa duka la Vioo la darajani hadi sasa licha ya watu kujitokeza kwenye zabuni hiyo.

b) Kama kuna mtu aliyekuwa amekusudiwa kukodishwa duka hilo kwa nini serikali iliamua kutangaza tenda kwa ajili ya duka hilo kupitia gazeti la Zanzibar Leo.

c) Hatua ya serikali kuendelea kukalia maombi ya watu waliojitokeza kunaleta sura gani kwa utendaji wa serikali katika kuwatumikia wananchi wake.

**Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko -** Alijibu:-

Ahsante Mhe. Naibu Spika, napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam 69 kwa kuanza na maelezo yafuatayo:

Mhe. Naibu Spika, nataka nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kwamba serikali iliamua kutunga Sheria ya Manunuzi ya Mwaka 2015 ili kuweka msingi wa usawa na haki pale inapotakiwa kuuzwa au kununua bidhaa au huduma kwa lengo la kuwepo uwazi katika ushindani.

Aidha napenda kukiri kuwa Wizara ilitangaza zabuni kwa ajili ya ukodishwaji wa jengo la duka la Vioo lililopo Darajani Unguja ambayo ilikuwa na nambari MTIM/2014/2015/MC/11 ya tarehe 04/01/2015.

a) Mhe. Naibu Spika, napenda kulifahamisha Baraza lako kuwa Wizara ya Viwanda na Masoko haijashindwa kufungua zabuni, bali imesita kufungua kwa sababu serikali imeandaa mpango maalum wa kulitumia eneo la Darajani kibiashara ambao utakuwa na matakwa maalum ya ujenzi wa eneo hilo.

b) Mhe. Naibu Spika, wizara ilikuwa na nia thabiti ya kukodishwa kwa duka hili kwa njia za zabuni ili kutoa ushindani, hata hivyo wale wote walioomba katika zabuni hiyo wamearifiwa na wizara kuhusiana na uamuzi wake huo wa kusitisha kufungua zabuni hiyo.

c) Mhe. Naibu Spika, maombi yaliyowasilishwa na wanazabuni hayajakataliwa, ila kutokana na sababu nilizozieleza hapo awali ndizo zilizopelekea kusimama kwa zabuni hiyo.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri kutokuwa na afya wala kiwango, ambacho naweza kuthubutu kusema siyo kweli katika Baraza hili kwa ushahidi niliokuwa nao, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo.

Naomba nikuulize maswali mawili tu madogo sana ya nyongeza.

a) Serikali ilitangaza zabuni na watu wakajitokeza. Utaratibu wa zabuni upo kwa mujibu wa sheria. Kwa nini zabuni itangazwe halafu ishindwe kufunguliwa mpaka sasa, inaleta picha gani katika msingi wa utawala bora ambao tumejibiwa sasa hivi na Mhe. Waziri kuhusu Utawala Bora Mhe. Dokta Mwinyihaji, hasa ukizingatia sera ya haki sawa, na ukizingatia Wizara hii inaongozwa na Naibu Katibu Mkuu wa CUF, haki

sawa kwa wote. Ni lini mtafungua tenda hii, muda umeshakuwa mkubwa, wananchi wanaendelea kusubiri, na kuna hatari ya kupelekwa Mahakamani, hilo moja.

b) Kwa vile lile jengo ni la kihistoria na la aina yake, na hali yake haliridhishi hivi sasa. Msimamizi wa mitaji ya umma Mhe. Waziri wa Fedha mimi nafikiri angetusaidia hili swali la pili kujibu yeye kutokana na jengo lilivyo mchakato wake.

   Ni jengo la kihistoria limejengwa na marehemu Rais Abeid Amani Karume. Jengo la kihistoria na mazingira yake hayaridhishi. Ni lini litafanyiwa ukarabati kutokana na hali yake na watu wameshajaza tenda kujitokeza, huo ndio utawala Bora Mhe. Naibu Waziri, lini zitafunguliwa tenda hizo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko:** Mhe. Naibu Spika, nimesema katika jibu mama ni kwamba, kweli Wizara ilitangaza zabuni lakini pakatolewa maagizo kutoka serikalini kwamba kuna mpango maalum wa kuendeleza eneo lote la Darajani. Ni utaratibu wa kawaida Mhe. Naibu Spika, kama kuna suala jengine la maendeleo limepangwa kufanyika katika eneo fulani basi tunasitisha utaratibu uliokuwepo ili kusubiri utaratibu ulioandaliwa.

Mhe. Spika, kwa maana hiyo zabuni hizo hazijafunguliwa kwa sababu ya utaratibu huo.

**Mhe. Nassor Salim Ali:** Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, katika majibu ya Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba serikali imeandaa mpango maalum wa kulitumia eneo la Darajani kibiashara. Je, mpango huo taratibu zake zimeshaanza, na kama hazijaanza ni lini taratibu zake zitaanza ili kuliendeleza eneo hilo la Darajani kibiashara.

**Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko:** Mhe. Naibu Spika, kwa taarifa yake Mhe. Naibu Spika, na kwa taarifa ya Baraza lako hili Tukufu kwamba utaratibu tayari umeshaanza na michoro imeshaanza kuandaliwa ili kuendeleza eneo lote lile la Darajani.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana na kwa vile mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha ambayo Kamati yangu inatumikia Wizara ya Biashara naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, serikali imesema kwamba imeandaa mpango maalum ili kuendeleza shughuli za biashara pale Darajani. Lakini wakati serikali inaandaa mpango huo wananchi wameshuhudia majengo kadhaa yakijengwa. Hivi ninavyozungumza yapo majengo yanaendelea kujengwa lakini kwa jengo la Vioo serikali ina mpango maalum ambao unasubiriwa utekelezwe.

Hivyo Mhe. Naibu Waziri hatwambii kwamba Wizara yake ina mpango lenye sehemu (a) naomba nitoe maelezo yafuatayo:-

a) wa siri.
b) Hivyo ushindwe kutekeleza sheria Nam. 9 ya manunuzi ya 2005 wakati unajua serikali ina mpango maalum wa kuendeleza eneo la Darajani kibiashara. Ni kwa nini walitangaza, hivyo Wizara hawaoni kwamba walikurupuka.

**Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko:** Mhe. Naibu Spika, wakati majengo yale yanaanza kujengwa ilikuwa bado serikali haijaja na utaratibu huu mpya wa kuendeleza eneo lote la Darajani.

Lakini kwa kuwa utaratibu huu mpya umeshakuja majengo mengine hayatoibuliwa tena katika ujenzi mpya ila yatasubiri utaratibu huu mpya ulioandaliwa na serikali.

## Nam 12

## Kuzuiwa kwa Uwindaji wa Ndege Katika Mashamba ya Mpunga

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub Kny(Mhe. Saleh Nassor Juma) -** Aliuliza:

Kwa kuwa katika Jimbo langu la Wawi, batamaji (salile) ni miongoni mwa ndege wanaoathiri sana zao la mpunga na hatimaye kuathiri kipato cha wakulima kwa kiasi kikubwa. Aidha, wananchi hukodi au kuazima magobore kwa ajili ya kuwawinda ndege hao waharibifu tendo ambalo huwafariji sana wakulima wa eneo hilo pamoja na familia zao.

a) Je, ni sababu gani za msingi zilizopelekea baadhi ya viongozi katika ngazi ya Shehia kuzuia wananchi uwindaji wa ndege hao hata kile kipindi cha mpunga unapofumua.

b) Je, tendo la kuzuia uwindaji wa bata maji, adui mkubwa wa zao la mpunga na hatimaye kuendelea kuathiri zao hilo huku ni kuwaondoshea wananchi wetu umasikini au kuwaongezea.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako na kabla ya kumjibu Mheshimiwa swali lake Nam. 12 Mhe. Naibu Spika, hakuna kumbukumbu zinazoonesha kwamba mabata salile wanakula mpunga, kwani salile ni ndege wanakula kwa kuchuja yaani *(filter feeds)* kama walivyo mabata wengine.

Aidha salile ni ndege wanaohifadhiwa kwa mujibu wa kifungu Nam. 73 cha Sheria Nam. 10 ya mwaka 1996 ya Zanzibar, Sheria ya Uhifadhi na Usimamizi wa Rasilimali za Misitu.

Viongozi na wananchi wana jukumu la kulinda na kusimamia sheria hiyo. Hata hivyo kuna baadhi ya wananchi wanaowawinda ndege hawa kwa ajili ya kitoweleo, lakini huwawinda kwa kisingizio cha uharibifu wa mazao.

Mhe. Naibu Spika baada ya maelezo hayo mafupi, sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama hivi ifuatavyo:

a) Mhe. Naibu Spika, baada ya kufuatilia hoja au swali lililoulizwa na Mhe. Mwakilishi katika shehia ya Jimbo alilolitaja imebainika kwamba hoja aliyoiwasilisha kwamba haijawahi kujitokeza katika maeneo ya shehia hiyo.

b) Suala la Sheha kuzuia uwindaji wa bata maji ni wajibu wake kulingana na sheria ya uhifadhi na usimamizi wa rasilimali za misitu.

**Nam 54**

**Madai ya Malipo ya Mfuko wa Hifadhi kwa Wafanyakazi wa Kampuni ya *MECCO* Pemba**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub Kny:(Mhe. Saleh Nassor Juma) -** Aliuliza:-

Kampuni ya Ujenzi wa barabra ya *MECCO* ambayo inafanya kazi ya ujenzi wa baadhi ya barabara za Kaskazini Pemba, wafanyakazi wake wanakatwa makato ya hiari kwa ajili ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (*ZSSF*) tangu wapate ajira hadi leo hii. Baada ya uchunguzi kuna taarifa kwamba fedha hizo ni za mwaka mmoja tu zilizoingia kwenye mfuko huo tangu wafanyakazi hao waajiriwe hadi leo hii.

a) Je, taarifa hizi ni za kweli.
b) Kama za kweli, uzembe huu umetokana na watendaji wa *ZSSF* au ni utapeli wa makusudi unaofanywa na uongozi wa Kampuni ya *MECCO*.

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Alijibu:

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa naomba kujibu swali la Mhe. Saleh Nassor Juma Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Wawi lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

a) Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba Kampuni ya Ujenzi wa Barabara *MECCO* ambayo inajenga barabara katika Mkoa wa Kaskazini Pemba inadaiwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar malimbikizo ya mchango ya wafanyakazi wake.

b) Mhe. Naibu Spika, kiutaratibu muajiri ndiye anayepaswa kuwasilisha mchango wa muajiriwa wake kwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar yaani *ZSSF* kwa mujibu wa sheria ya *ZSSF* kila mwezi kabla ya tarehe 15 ya mwezi unaofuata.

Kuchelewa kufanya ni kosa na hupaswa kuchukuliwa hatua, kisheria adhabu ya kosa hilo ni tozo la asilimia 5 ya mchango uliokuwa haujalipwa. Kampuni ya *MECCO* imekuwa ikichelewa kuwasilisha michango ya wafanyakazi wake au kutowasilisha kabisa kwa baadhi ya miezi. Mwenendo huu wa Kampuni ya *MECCO* umeifanya *ZSSF* kuifungulia mashtaka *MECCO* lakini Kampuni ya *MECCO* waliomba suala hili litatuliwe nje ya Mahkama.

Mhe. Naibu Spika, Kampuni ya *MECCO* ilikuwa inadaiwa michango ya wafanyakazi wake tokea mwezi wa Januari, 2013 hadi Aprili, 2015. Baada ya kikao cha pamoja na *ZSSF*, michango ya kuanzia Januari, 2013 hadi Februari 2014 yenye thamani ya shilingi 26,854,361 imelipwa. Aidha *ZSSF* iliendelea kufuatilia michango ya wafanyakazi wa *MECCO* ya kuanzia mwezi Machi, 2014 hadi Novemba 2014 nayo tayari imeshalipwa tokea tarehe 15 Januari, 2015. Jumla ya shilingi 20,654,361 pia walilipa pamoja na adhabu. Kwa sasa *ZSSF* inafuatilia deni la michango kuanzia Disemba 2014 hadi mwezi wa Aprili, 2015 lenye thamani ya jumla shilingi 11,564,250 pamoja na adhabu yake.

Mhe. Naibu Spika, watendaji wa *ZSSF* wamechukua kila juhudi kuhakikisha kuwa fedha za wafanyakazi wa *MECCO* zinapatikana kwa wakati na kuhifadhiwa kwa ajili ya mafao ya uzeeni kwa wafanyakazi hao.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu muafaka kabisa ya Mhe. Waziri ninaomba kumuuliza swali moja dogo la nyongeza. Huoni *MECCO* kuchelewa kupeleka fedha hizi kutokana na sababu kuwa Serikali Kuu wanaidai.

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Mhe. Naibu Spika, ni kweli *MECCO* wanaidai Serikali Kuu, lakini sababu ya kutokuwasilisha michango ya wafanyakazi wake kwa *ZSSF* si sababu kwamba wanaidai Serikali Kuu, kwa sababu fedha zile si za Serikali Kuu, fedha zile ni za wafanyakazi. Kwa hivyo *MECCO* ana wajibu wa kuwasilisha michango ya wafanyakazi kwa *ZSSF* na sisi Serikali Kuu tuna ratiba ya kulipana na *MECCO*.

**Mhe. Subeit Khamis Faki:** Ninakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, kunipa fursa nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza. Kwanza ninamshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri, na ametueleza kwa ufafanuzi na tumefahamu vizuri. Lakini napenda nimuulize Mhe. Waziri. Kwa kuwa Kampuni hii ya *MECCO* ni ya ujenzi wa barabara, na ujenzi wa barabara unakuwa na muda wake na ukomo wa kumaliza kujenga barabara. Na kwa kuwa wananchi wetu wameshakatwa fedha zao katika mishahara yao kwa ajili ya kupelekwa *ZSSF*, na wakati *MECCO* wanamalizia kujenga barabara watakunja virago warudi sehemu yao. Je Serikali au kupitia *ZSSF* itakuwa ndio dhamana wa fedha zile za wananchi, na kama sio dhamana, je, wananchi fedha zao watazipata kwa kuelekezwa misingi gani ili wapate haki yao ambao wamekatwa.

**Mhe. Waziri Fedha:** Mhe. Naibu Spika, kwanza nataka nikuhakishie Mhe. Subeit na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu, hakuna fedha ya mfanyakazi yeyote ambayo itapotea kwa sababu tu kuna Kampuni haijawasilisha michango yake kwenye *ZSSF*. Serikali ina utaratibu wake na *MECCO* hawezi akaondoka bila ya kumaliza hizi fedha ambazo anadaiwa na *ZSSF*. Kwa hivyo ninakutoa wasiwasi tu wala usiwe na wasiwasi, sisi tunaendelea kumbana *MECCO*, na *insha Allah* ukitizama jibu langu la msingi nimesema tokea mwaka 2013 alikuwa anadaiwa. Angalia sasa tulivyombana *MECCO* imebakia miezi 5 tu deni, na hili *insha Allah* atalilipa katika kipindi kifupi kinachokuja.

**Nam. 70**

**Ukosefu wa Maduka ya Kilimo katika Maeneo ya Vijijini**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub – ** Aliuliza :-

Tangu Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kutangaza Mpango wa Mapinduzi ya Kilimo wananchi wengi

hasa Vijana wameanza kujitokeza katika shughuli za kilimo, lakini wanakabiliwa na usumbufu wa kufuata masafa marefu huduma ya pembejeo zikiwemo dawa za magugu, mbolea, mbegu kutokana na kukosekana kwa maduka katika maeneo wanayoishi.

(a) Ni lini Serikali itafungua maduka kwa ajili ya kutoa huduma hizo katika kila Jimbo Unguja na Pemba.

(b) Kwa kuwa Kilimo ndio uti wa mgongo, Serikali imechukua hatua gani za kuondoa tatizo la upatikanaji wa mbegu hasa ya Mpunga ikiwemo mbegu ya Nerika.

(c) Kwa kuwa mvua za mwaka huu zimeleta matumaini makubwa. Je, Serikali ina mpango gani wa kuimarisha bajeti ya Kilimo baada ya vijana wengi kuvutika na harakati za kilimo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili –** Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa heshima yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub wa Jimbo la Muyuni swali lake namba 70 kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, jukumu la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kutayarisha Sera pamoja na kuhamasisha na kuwaelekeza wafanyabiashara kufungua maduka ya pembejeo karibu na maeneo yanayolimwa mpunga ili kuwapunguzia usumbufu wakulima wa kufuata pembejeo katika masafa marefu. Hata hivyo, Serikali kupitia mradi wa kuendeleza Kilimo *(PADEP)* kwa kushirikiana na wakulima wamefungua maduka ya *(PADEP)* katika maeneo ya Kilombero, Fuoni, na Dunga Pale na wafanyabiashara wamefungua maduka katika maeneo ya Amani na Mwanakwerekwe.

b) Mhe. Spika, kwa sasa tatizo la upatikanaji wa mbegu halipo, kwa sababu tangu Serikali ianze kutoa ruzuku pia inanunua mbegu kutoka kwa wakulima ikiwemo mbegu ya Nerika ambapo jumla ya kilo 234 za mbegu ya Nerika imenunuliwa kwa wakulima (Msimu wa Vuli 2014). Wizara ya Kilimo na Maliasili inaendelea na tafiti za kutafuta mbegu bora nyengine zinazohimili ukame, maradhi na zenye uzazi mkubwa.

c) Mhe. Spika, bajeti za Mawizara ikiwemo Wizara ya Kilimo na Maliasili zinapangwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, katika upangwaji wake huwa na vipaumbele, na kwa mwaka huu 2015/2016 vipaumbele vyake ni Elimu, Afya na Miundombinu. Hata hivyo, Serikali kwa kushirikiana na

Washirika wa maendeleo itaendelea kuinua hali ya kilimo hasa cha mpunga kupitia *program* na miradi yake.

**Utaratibu**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Naibu...

**Mhe. Naibu Spika:** Wewe kwa niaba sio swali lako, umeuliza kwa niaba, kwa hivyo mimi nina uamuzi.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** La msingi uangalie *order paper* Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Naibu Spika:** Samahani sana Mhe. Jaku.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa utiifu wako. Pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo ya kusikitisha na kukatisha tamaa hasa kwa wakulima wa kilimo cha mpunga ni kitu cha aibu kilicho juu hivi sasa. Mbegu ya mpunga ya Nerika imeletwa na Serikali na imeonesha matumaini makubwa kwa wakulima. Leo Serikali imejipanga vipi kutafuta angalau mabonde mengine kuweka akiba kwa mbegu hii ya Nerika. Leo mbegu hiyo inakwenda kwa wakulima ni kitendo cha aibu, hilo la mwanzo.

Kwa kuwa maduka ya kilimo yapo mbali na wakulima ndio wanaosumbuka, Serikali ina mpango gani wa kuwapelekea huduma hizo karibu kwa maeneo wanamoishi kama utekelezaji wa mpango wa matumizi ya Kilimo kufikia lengo la Rais wetu Dkt. Ali Mohamed Shein.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, swali lake la mwanzo sikumfahamu naona katoa maelezo tu.

**Mhe. Naibu Spika:** Swali la mwanzo rejea Mhe. Jaku.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, mbegu ya mpunga ya Nerika imeletwa na Serikali na imeonesha matumaini kwa wakulima, inasikitisha kuona inaadimika kiasi kwamba Serikali sasa inafuata mbegu hiyo kwa wakulima. Ina maana wataalam wa kilimo hawana mashamba ya mfano wa kilimo bora wakati wao ndio wanaotegemewa kwa mfano katika sekta ya kilimo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, mbegu ya Nerika Idara kazi yake kufanya utafiti na mbegu ya Nerika, ilipoletwa kwanza ilifanyiwa utafiti na baada ya kufanyiwa utafiti mbegu bila shaka tuna mashamba yetu ya kufanyia utafiti Bambi, na mbegu ya Nerika sawa sawa na mbegu

nyengine. Mbegu zilizopita *Super Beacon India* zote zilifanyiwa utafiti, ikishafanyiwa utafiti mbegu ile imekwisha, inakuja suala la wakulima kutumia jinsi wanapenda mbegu gani.

Kwa hivyo suala la Nerika si kama mbegu hii imepotea, ipo, na mbegu ya Nerika inalimwa, na mbegu ya Nerika imo katika vituo vyetu vya Kilimo. Kwa hivyo kununua mbegu kwa wakulima ambao waliohamasishwa kutumia mbegu ile ndio wazalishe halafu sisi tununue. Kwa hivyo mimi nasema bado mbegu ya Nerika haijapotea.

Swali lake la pili kuwasogezea pembejeo wakulima karibu, kama nilivyosema wizara inapeleka pembejeo hasa mbegu katika vituo, kila kituo inapelekwa mbegu kwa wakulima. Kwa mfano Cheju kuna kituo inawekwa mbegu pale wakulima wanafuata pale. Kilombero kuna kituo chao inafuata pale na sehemu nyengine hivyo hivyo.

**Mhe. Panya Ali Abdalla:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri lakini na mimi nina swali la nyongeza. Kwa kuwa kilimo ni uti wa mgongo wa Taifa letu na kinamama wako mstari wa mbele katika kuitikia wito huu kwa kulima mazao mbali mbali ikiwemo muhogo, mpunga, mahindi, mtama na mazao mengine.

Lakini katika upatikanaji wa mbolea kinamama wanasumbuka sana katika kuipata mbolea kwa ajili ya kuimarisha mazao yao na wanaendelea kulima kilimo kile kile cha zamani ambacho hakipati mbolea na kinakuwa na tija ndogo. Je, ni utaratibu gani kinamama hawa na wao wautumie ili waweze kupata mbolea kwa ajili ya kuimarisha kilimo chao na waweze kupata tija kwa wingi.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Malilasili:** Mhe. Naibu Spika, pembejeo zetu hususan zikiwemo mbolea tunaagiza kwa mujibu wa bajeti tunayoipata na tukishapata pembejeo hizi nazo zinagaiwa kwa mujibu wa utaratibu uliopo. Utaratibu uliopo hasa hasa kwa kilimo cha mpunga. Kwa mujibu wa taratibu zikishatoka Wizarani inapelekwa Mawilayani, Mawilayani kuna kamati zinazokutana zinasambazwa katika vituo kwa mujibu wa taratibu zilizokuwepo katika sehemu hizo kila shehia. Kwa hivyo hasa hasa mbolea tunatumia katika sehemu za kilimo cha mpunga.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kuweza kunipa nafasi ili kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri nina moja, mbili, tatu. Katika majibu yako mazuri sana Mheshimiwa utakubaliana na mimi na hasa kutokana na wakulima wetu wa kisasa ambao wamejishahijisha vizuri kwa

kupitia mabwana shamba, lakini ukosefu wake kuwa vifaa havifiki kwa wakati unaotakiwa. Hilo ni Moja.

Lakini pili Mheshimiwa, hivi sasa hivi imejitokeza Kampuni ambayo iko tayari kuisaidia Serikali ili wananchi wakaweza kilimo cha kuweza kupata tija, ambacho tunaondokana na kilimo cha kukipata mtu mwenyewe binafsi, je wizara yako mtu kama huyo uko tayari kumpa mashirikiano kwa nguvu zote.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili:** Mhe. Naibu Spika, kwanza sikubaliani kwamba vifaa vya kilimo havifiki kwa wakati, kwa msimu huu mbolea imefika kwa wakati,dawa imefika kwa wakati.

Swali la Kampuni, swali la Kampuni Mhe. Naibu Spika, hatuna tatizo na Kampuni hii. Tatizo la Kampuni kuwasaidia wakulima lazima wapite kwa wakulima wakae pamoja wakubaliane, waridhike wakulima. Kwa hivyo sisi hatuna tatizo na hilo, ridhaa itoke kwa wakulima wenyewe.

**Nam. 11**

**Ukosefu wa Maji Vijijini**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub: (Kny: Mhe. Saleh Nassor Juma)** – Aliuliza:

Kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika awamu hii ya saba inayoongozwa na Dkt. Ali Mohamed Shein imefanya juhudi kubwa kuwapatia wananchi wake maji safi na salama ambapo kwa miradi mingi ya maji katika maeneo ya vijijini na mjini imefanyiwa uzinduzi katika maadhimisho ya miaka 51 ya Sherehe za Mapinduzi, ikiwemo ule wa mchina visima vya Vikunguni na Vitongoji katika Jimbo la Wawi.

Je, ni sababu gani za msingi zilizopelekea wananchi wa vijiji vya Matungu, Gemalao hadi Kibokoni kukosa kabisa maji pamoja na kuunga bomba kwenye visima hivyo.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati** - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kujibu swali Nam. 11 la Mhe. Saleh Nassor Juma kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, vijiji vyote hivi vilivyotajwa viko katika eneo la Vitongoji na huduma ya maji inapatikana bila ya mgao katika maeneo hayo.

Mhe. Naibu Spika, maeneo hayo tayari maji yanapatikana baada ya visima vyake kuondolewa Umeme wa Tukuza na wananchi 40 washaunga maji na wanapata maji bila ya matatizo. Suala kubwa kwa vijiji hivi ni wananchi kuunga maji majumbani ambapo fursa ipo hata kwa mkopo kwa wananchi kuunga maji katika mabomba mapya yenye maji ya kutosha.

Mhe. Spika, Mamlaka ya Maji inachokifanya ni kuweka mtandao wenye maji ya kutosha na suala la kuunga maji majumbani ni gharama ya mwananchi mwenyewe kama ilivyo huduma ya umeme.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mafupi ya Mhe. Waziri amesema huduma hizi za maji zinapatikana kwa wananchi wa Vitongoji katika shehia hizi, ni lini Waziri atafuatana na Mwakilishi kwenda kuhakikisha hili suala kwa kweli yanapatikana maji katika shehia alizotaja Mhe. Mwakilishi. Hilo la kwanza.

Pili, suala hili la msingi linafuatana na suala la maji katika Jimbo langu la Muyuni ikiwemo Muungoni, Jozani, Kitogani leo wiki nzima imekosa maji, pamoja kuwa nimeripoti mimi mwenyewe binafsi hii wiki ya pili hakuna hatua iliyochukuliwa mpaka muda huu.

Je, anawaambia nini wananchi hawa wa Jimbo la Kitogani, Muungoni na Jozani na vile vile ninataka kumwambia Mhe. Waziri kuna ukosefu mkubwa sana Wizarani kwake wa mafundi afanye jitihada za kuongeza mafundi kutafuta ajira katika fani hii.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Naibu Spika, maofisa wangu baada ya kuridhika kwamba suala hili katika maeneo haya liko vizuri, walipoandika jibu la awali walisema hili ambalo Mhe. Mwakilishi amelisema, kwamba wako tayari kufuatana nyumba kwa nyumba wakaulize kama maji yanapatikana au hayapatikani. Waliandika neno hilo lakini mimi nikaona si heshima kumwambia Mwakilishi neno hilo nikaliondoa, lakini kwa kuwa Mhe. Mwakilishi amelileta basi maofisa wangu wako tayari kwenda kuoneshana kila nyumba kutizama maji kama yapo. Hilo moja.

La pili suala la Kitogani, Muungoni na kwengineko kama amesema wiki moja nakubali inaweza kuwa wiki moja kwa sababu suala la mitambo ni suala la kuharibika, *pump* inaweza ikaungua, umeme unaweza ukaleta shoti mahala pengine popote, bomba linaweza likapasuka. Kwa hiyo, naweza kukubaliana naye kwamba kweli wanaweza kuwa watu wamekosa maji katika wiki hiyo, kinachotakiwa ni matengenezo, na matengenezo yanategemea kupatikana kwa vifaa ambapo wakati ule yanafanyika yale matengenezo yaliyokusudiwa.

Mhe. Naibu Spika, suala la mafundi ni kweli ninao wachache lakini nikipata nafasi za ajira niko tayari kuongeza maana mafundi najua hawapatikani mbali, ni Mbweni tu hapo wanaosoma ufundi huo tukiwapata kuna Mbweni, kuna Mkokotoni hatuna matatizo sisi ya kuajiri katika maeneo hayo.

**Mhe. Nassor Salim Ali:** Mhe. Naibu Spika, ahsante na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri, na katika majibu yake alisema kwamba fursa ipo hata kwa mkopo kwa wananchi kuunga maji katika mabomba mapya yenye maji ya kutosha.

a) Swali langu ni kwamba je, gharama za kuunga maji kwa wananchi hao wa vijijini je ni shilingi ngapi kuunga maji hayo.
b) Ni taratibu gani ambazo zinachukuliwa ili wananchi kuweza kupunguza au kuondoa ukiritimba wa watendaji wetu huko vijijini.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Naibu Spika, gharama ya kuunga maji ni shilingi elfu 50,000 lakini zinaweza zikaongezeka shilingi 50,000 kwa sababu hutegemea masafa, kuna suala la mabomba na baadhi ya vifaa ambavyo kama *ZAWA* watakuwa hawana watataka agharamie, hilo suala ni kwenda pale *ZAWA* na kuomba kuungiwa maji na ukajaza baadhi ya fomu pale watu wakaja wakaunga maji katika sehemu yako.

Mhe. Naibu Spika, suala la ukiritimba tusaidiane mimi na Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu, maana mimi siwezi nikajua kwamba fulani kafanyiwa ukiritimba lakini nina hakika tukipata wawili tu au watatu na tukawaadhibu basi ukiritimba utaondoka.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Naibu Spika, ahsante pamoja na majibu yake mazuri Mhe. Waziri naomba kidogo niongeze na uzuri wake hasa katika utendaji. Mhe. Naibu Spika, kwanza nampongeza sana Mhe. Waziri pamoja na Mkurugenzi wake wa *ZAWA* kwa kuhakikisha kipindi hiki kuwa wananchi wanapata maji hasa maeneo yaliyokuwa hayajafika maji, kwa ushahidi mimi mwenyewe nimeona maji yamefika. Suala langu liko hapa Mheshimiwa hivi karibuni mlitwambia mlipata msaada wa visima kama 62 hivi au 60 utaniweka sawa Unguja na Pemba. Je, Mheshimiwa Pemba walipata visima vingapi na Unguja walipata visima vingapi na visima hivyo vipi ushahidi tosha kuwa tayari maji yanapatikana.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Naibu Spika, visima tulivyovipata kwa msaada wa Kampuni ya Ras Al Khaimah vya awali vilikuwa 50, katika hivi 32 vimechimbwa Unguja na 18 vimechimbwa Pemba. Hivi sasa tayari

Ras Al Khaimah wamelewa nyongeza nyengine ya visima 50, hivi viko katika utaratibu wa kugaiwa. Katika visima hivi 50 kwa bahati tumefanikiwa visima 48 vimekuwa na maji, tumekuwa na matatizo ya visima viwili ambavyo hivyo ni vikavu, yaani baada ya kuvipiga *pump* havikuweza kuchukua muda mrefu vimekauka. Lakini hata hivyo tunafanya utaratibu na hivyo viwili kuvitafutia mahala pengine tuchimbe ili navyo vipate maji. Visima hivi bado havijaungwa katika mitandao isipokuwa vichache sana, kwa sababu ya upungufu wa hivyo vifaa vya kuunga kutoka kwenye visima mpaka kwenda katika huduma za wananchi.

Wizara yangu pamoja na *ZAWA* tunajitahidi kuona msaada tutaoweza kuupata kwa ajili ya kuvitumia visima hivi kupeleka kuwa katika *system* ya maji ili wananchi waweze kufaidika na maji yanayotokana na visima hivi. Lakini vichache nimesema kama Welezo tumeanza kukitumia na katika maeneo mengine viko visima tumeanza kuvitumia.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 - Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, majadiliano yanaendelea nina majina ya Waheshimiwa 16 tunaomba tuchangie kwa mchana huu jioni tuanze majumuisho na kupitisha vifungu. Kwa hivyo, tunaomba sana tusirejee humo kwa humo.

**Mhe. Fatma Mbarouk Said:** Mhe. Naibu Spika, ahsante na mimi kunipa fursa hii asubuhi hii ya leo kuchangia machache katika hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Kwanza na mimi sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kuendelea kujaalia nchi yetu ikawa katika amani na utulivu. Pia nimshukuru Dkt. Ali Mohamed Shein kwa uongozi wake mahiri na usimamizi mzuri wa shughuli za serikali.

Mhe. Naibu Spika, pia na mimi nichukue fursa hii adhimu ya kukupongeza wewe pamoja na Spika wetu vile vile na Wenyeviti wetu kwa kusaidiana kwa pamoja katika kuendesha Baraza letu hili.

Mhe. Naibu Spika, na mimi nirudie vile vile kama Makamu wa Pili wa Rais alipokuwa akitoa hotuba yake hii kwamba mwaka huu tuna mambo mawili

muhimu ambayo ni uchaguzi mkuu pamoja na Katiba yetu inayopendekezwa. Na niwaombe wenzangu kwamba Katiba hii inayopendekezwa basi pale itakapofika muda basi tuipitishe kwa kura zote za ndiyo.

Chimbuko la Katiba hii ni kwamba baada ya kuona *amendment* zilizofanywa kwa miaka tofauti tofauti na kumithilisha Katiba ile ikawa kama ni nguo iliyojaa viraka. Kwa hivyo, ukaanza ule mchakato kuanzia kwa Tume ile ya Jaji Warioba na baadae tukaenda kwenye maoni ya wananchi tukatoa maoni yetu na vile vile kwenye Mabaraza na hadi kufikia Bunge la Katiba.

Kwa kweli Mwenyezi Mungu ametuumba sisi wanadamu, kwa hivyo ni lazima tushukuru neema zile ambazo Mwenyezi Mungu ametupa, na ukikufuru neema moja ya Mwenyezi Mungu basi utakuwa wewe mwenyewe hukujitendea haki. Kwa hivyo, mimi nasema kutokana na mchakato wote ule ambao ulipita, basi kuna haja ya kutathmini namna ya fedha za umma zilivyotumika kutokana na michakato ile ambayo ilikwenda, na lazima tuzingatie *value for money*. Fedha zile naamini kulikuwa na matatizo mengi ya wananchi wetu tukitizama kwenye mahospitali kuna mapungufu, kwenye maskuli kuna mapungufu na sehemu mbali mbali za jamii. Kwa hivyo, lazima nichukue fursa hii kupitia Baraza lako Tukufu Mhe. Naibu Spika kuwashawishi wenzangu kwamba hili ni jambo muhimu na lazima tulitekeleze pale inapofika.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea kwenye mchango wangu kupitia kitabu hiki kwanza nikianza na hili jambo la uchaguzi kwanza niishukuru Tume ya Uchaguzi kwa kuendelea na kazi zake muhimu za kuwaelimisha wapiga kura na ikifika wakati Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar itaendelea katika uboreshaji wa daftari la kupiga kura. Hilo ni jambo la msingi, na wananchi wote wanatakiwa wahakikishe kwamba wameingia katika lile daftari la kupigia kura.

Mhe. Naibu Spika, nikienda katika kitabu hiki nimeona nianze na hii hali ya uchumi wa Zanzibar ambayo napata faraja kusikia kwamba kwa kipindi cha miaka mitano uchumi wa Zanzibar umeonesha mwenendo mzuri na umekuwa kwa kiwango cha kuridhisha cha wastani wa asilimia 6.5%. Ukuaji huo wa uchumi ulitokana na kuimarika kwa sekta ndogo za ujenzi, fedha na bima, usafiri, habari na mawasiliano na sekta ndogo za utawala wa umma.

Mhe. Naibu Spika, pia nimeona kwamba kwa upande wa pato la Taifa kwa mwaka 2014 pato halisi lilikuwa kwa kiwango cha wastani wa asilimia 7 ukilinganisha na wastani wa 7.2 mwaka 2013, hiyo ni faraja kwangu, lakini pia kuimarika kwa sekta ya huduma ambayo imekuwa kutoka asilimia 4.6 mwaka 2013 hadi 9.8 mwaka 2014. Yote haya ni mambo ambayo serikali yetu kutokana na hali ya utulivu wa

kisiasa wa nchi yetu basi kuna mambo hayo ambayo yamefanikiwa kwa kiasi fulani. Kwa hivyo, tuendelee kudumisha amani na utulivu wa nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, kwenye huduma za jamii niipongeze sana serikali kwa kutangaza elimu ya msingi kuwa ni bure, na vile vile nimshukuru Mhe. Rais kwa uamuzi wake huo ambao unawajali sana wananchi. Na niseme ili tufanikiwe na hili basi ni lazima serikali yetu ile keki yetu tunayopata basi tuhakikishe kwamba inapelekwa kwa kiasi kikubwa, kwani isiwe maneno ya humu kwenye vitabu tu na tumuenzi Rais wetu tusimuangushe ili kile kinachopatikana basi kielekezwe kwenye elimu hiyo ya msingi.

Mhe. Naibu Spika, kwanza niishukuru serikali kwa kufanya kwa makusudi kuweka mfumo wa bajeti kupitia programu, mfumo wa bajeti ambao ni mgawanyo wa rasilimali za serikali unaofanyika kwa njia ya programu. *PBB* ni mfumo unaoenda sambamba na utekelezaji wa MKUZA ambao unajumuisha mipango yote ya wizara ikiwemo matokeo ya muda mrefu.

Mhe. Naibu Spika, vile vile napata faraja serikali kuweka mazingira mazuri ya kuwawezesha wanafunzi wa vyuo mbali mbali ndani na nje ya nchi kwa kuwapatia mikopo wale wote wanaokidhi vigezo vya kupatiwa mikopo hiyo. Serikali itaendelea kutoa mikopo ya elimu ya juu ili kufikia lengo la kuwa na wataalamu wazalendo katika fani mbali mbali. Isipokuwa nitoe ushauri kwa wale waliopata mikopo basi ni vizuri kurejesha ili tutoe nafasi ya wengine kuweza kukopa.

Mhe. Naibu Spika, kwenye sekta ya afya pia nimeona kitabu hiki kimeeleza mambo mbali mbali na niishukuru serikali kwa kipindi kirefu ilikuwa hakuna mahala pa kutosha pa wagonjwa mahututi, lakini sasa nimeona kwamba kumejengwa jengo zuri. Tunachoomba ni utunzaji wa yale majengo, kwa kweli kuna msemo wa Kiswahili unaosema kwamba "*kitunze kidumu*" iwe kila tunachokipata kuna ujenzi mkubwa na ujenzi mdogo kwa hivyo lazima kila mara pale panapoonekana athari ndogo tu inapotokea basi ni vizuri pakafanyiwa ukarabati wa haraka kwani "*usipoziba ufa utajenga ukuta*". Kwa hiyo, tuepukane na yale mambo yakuja kufanya ujenzi na tukatumia fedha nyingi, pale pale jambo linapoonekana tu limeleta athari basi wakati ule ule jambo lile lifanywe marekebisho kwa haraka.

Mhe. Naibu Spika, kwenye sekta hiyo ya afya nimeona kwamba kuna madaktari ambao wameongezwa na vile vile kuwasomesha, hili ni jambo la msingi kabisa kupata madaktari wazalendo.

Vile vile maji ni uhai, na ninaona humu serikali pia imechukua juhudi za kuwapatia wananchi huduma bora ya maji safi na salama katika kutimiza malengo

yale waliyojiwekea. Na mimi nishukuru hasa wizara hii kushirikiana na viongozi wa majimbo kwamba sasa hata kule jiomboni kwangu tatizo la maji limeondoka kutokana na mradi ule wa SEMUSO. Kwa nguvu kubwa za Wawakilishi na Wabunge wa majimbo yetu matatu, ni kwamba sasa hivi faraja ya maji inapatikana kwa wingi sana.

Mhe. Naibu Spika, bado naendelea kwenye kitabu hiki nimepata faraja pia kuona kwamba kuna umuhimu unaonekana kupatiwa wananchi makaazi bora, na kuanzishwa kwa sheria ya Shirika la Nyumba la Zanzibar mwaka 2014 ambayo tumepitisha hapa. Lakini ningeomba kitu kimoja kwamba kama nilivyosema, huku kwenye *ICU* kwa kweli kuwe na uhifadhi au mambo endelevu ambayo yatayafanya majengo haya yawe mazuri na yaonekane katika mtazamo uliokuwa mzuri kabisa, kwani nasikitika sana kwa majengo ambayo yalijengwa kwa pesa nyingi, kwa imani ya Rais wetu Marehemu Mzee Abeid Amani Karume pale Mtemani. Kwa kweli yale majengo sasa hivi yanatia hofu, kuna jengo moja pale mara nyingi tunakwenda na Kamati yangu ya *PAC* naona namna gani majengo yale sasa hivi ni tishio, badala ya kuwapatia makaazi mazuri sasa imekuwa ni hatari kwao. Majengo yale sasa hivi yamewekewa miega, hivyo ningeiomba serikali ikafanya juhudi ili kuyakarabati majumba yale mara kwa mara.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye masuala ya mtambuka, nimeona hapa kuna utunzaji wa mazingira.

Mazingira ni jambo muhimu sana, nchi zote duniani zinatoa kipaumbele katika suala hili la maendeleo endelevu na kupunguza umasikini. Kwa hivyo, suala la mtambuka ni jambo la kulititilia mkazo na uhifadhi wa mazingira vile vile ni jambo la msingi kabisa, na lazima kuwe na ushirikiano baina ya zile taasisi zinazohusika na kutunza mazingira. Nimeona ni namna gani ukaguzi sasa hivi unakwenda kupitia mazingira, tunaona kitabu cha Mdhibiti na Mkaguzi ambacho anakwenda moja kwa moja kwenye kukagua maeneo mbali mbali kupitia ripoti zake na kuona mazingira yanachafuka kutokana na kukatwa mikoko vile vile uchimbaji wa mawe.

Kwa hivyo, ni lazima juhudi za lazima zichukuliwe ili pale inapotokea athari, kwa sababu lazima mambo haya yatatu-*cost.* Kwa hivyo kwanza zile taasisi zinazoshughulika kwenye mambo haya ya uwekezaji basi ni lazima wakae pamoja na watathmini ile athari na namna gani ya kutoa *solution* ili yale maeneo yasiathirike.

Mhe. Naibu Spika, niendelee tena kumshukuru Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuzindua rasmi kampeni ya kitaifa kuhusu udhalilishwaji wa wanawake na watoto na hii kauli ya "*sasa basi"* iwe basi kweli.

Udhalilishwaji wa kijinsia uko tafauti tafauti, unaweza kudhalilishwa kwa sababu ya ujanajike pia, hilo ni tatizo mbele ya mwanamme ukaonekana mwanamke huna maana, lakini nasema kwamba ukimuelimisha mwanamke mmoja ni sawasawa na kuelimisha jamii, na wanawake tunaweza bila ya kuwezeshwa, wenyewe tu tunaweza.

Mhe. Naibu Spika, rushwa ni adui wa haki na nimeona namna gani unapotoa rushwa akanyimwa mtu haki yake. Kwa hivyo ni lazima vyombo hivi vya kisheria kwenye mihimili na hasa Mahakama ijilazimishe au ifuate utaratibu, sheria zifuatwe ili kila mtu apate haki yake.

**Mhe. Naibu Spika:** Mheshimiwa bado dakika tano.

**Mhe. Fatma Mbarouk Said:** Ahsante sana kwa kunikumbusha kwamba nimebakiwa na dakika tano na nitazitumia vizuri.

Sasa niende kwenye Idara ya Upigaji Chapa nasema ni idara yangu, Waswahili wanasema: "*Mchamago hanyele huenda akawia tena*". Nilikuwa mfanyakazi, kwa hivyo naamini kwamba ninaweza nikarudi tena huko na nikafanya kazi za utendaji wangu.

Idara ya Upigaji Chapa na Mpiga Chapa wa Serikali ni idara muhimu sana na sasa hivi imefanywa kama ni Shirika, ina maana itakuwa inatakiwa ijiendeshe wenyewe.

Katika kutimiza malengo yake moja ni kuweka mazingira mazuri ya kazi za idara kwa ununuzi wa vifaa vya ofisini na samani, lakini pia kuna kutangaza huduma za kiwanda kwa ajili ya kuongeza idadi ya wateja na mapato.

Mhe. Naibu Spika, hapa ni lazima tutilie mkazo. Tunakumbuka kwamba nyuma huko ilikuwa Idara ya Upigaji Chapa karibu *equipment* zote zilikuwa zinapatikana pale, ni kuiwezesha zaidi ili iweze kuleta hayo mafanikio.

Zamani wizara zote za serikali mambo ya *stationery*, mambo ya *printing machine,* hata zamani kabla hatujaingia kwenye teknolojia hizi *type writer* hizo zote tulikuwa tunachukua Idara ya Upigaji Chapa, na iwapo kama hutaki kununua kule au kutakuwa na jambo lolote kama wao wenyewe hawatakuwanavyo vile vifaa basi lazima itoke *nonstop certificate* ili kukuwezesha wewe kwenda kuchukua nje.
Kwa hivyo, kama kweli tunataka shirika hili lifanye kazi vizuri basi ni lazima tulipe bajeti ya kutosha ili iweze kufanya hayo.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo kwanza nakushukuru, na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Amani naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

**Mhe. Panya Ali Abdalla:** Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwanza kabisa nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu (*S.W)* ambaye ametuwezesha kufika hapa asubuhi hii ya leo katika utekelezaji wa majukumu yetu.

Pia nichukue fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipatia na mimi nafasi hii ili niweze kuchangia machache katika Hotuba hii ya Makadiro ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mwaka 2015/2016.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa nichukue fursa hii kumpongeza kwa dhati kabisa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa uwasilishaji wa hotuba yake mwanana kabisa, ambayo aliiwasilisha jana, lakini aliiwasilisha vizuri ambapo sisi Wajumbe humu ndani tulifarijika kwa kumsikiliza lakini hata wananchi waliomsikia basi wameweza kumfahamu vizuri, hongera Mhe. Makamu wa Pili.

Pia hongera hizi nizipeleke kwa Mhe. Rais wetu wa Zanzibar, Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kumteua yeye Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kuwa kiongozi wetu wa shughuli za serikali katika Baraza hili Tukufu, jinsi anavyoweza kufanya kazi zake vizuri na ambavyo utendaji wake unavyoonekana kwa uwazi kabisa.

Pia nichukue fursa hii kumshukuru Waziri ambaye anafanya kazi katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Mohamed Aboud pamoja na watendaji wake wote ambao wanashirikiana katika kumsaidia Makamu wa Pili wa Rais, ili kuweza kufanikisha kazi zake vizuri, tunawapongeza kwa majukumu hayo makubwa waliyonayo na Mwenyezi Mungu ameweza kuwafanikisha kuweza kuyafanya hayo kwa vizuri kabisa.

Mhe. Naibu Spika, nianze mchango wangu katika hali ya kisiasa. Kwanza nichukue fursa hii kushukuru kabisa kwamba bado tuko katika hali ya amani na utulivu jambo ambalo tungepaswa kushukuru neema za Mwenyezi Mungu alizotuneemesha, na isingekuwa busara kwetu kuibeza neema hii.

Sote tungepaswa kufikiria kwa makini kabisa juu ya amani na utulivu tulionao, na kumuomba Mwenyezi Mungu kila mmoja wetu kwa imani yake, aweze kumuomba Mwenyezi Mungu atuvushe salama katika kipindi hiki kigumu cha uchaguzi.

Pia nimuombe Mhe. Makamu wa Pili wa Rais basi aweze kukaa na viongozi wetu wa taasisi za kidini, ili awashauri katika kuzungumza na wafuasi wao kuwa waihubirie amani yetu hii na utulivu ambayo tunayo kwa kuomba dua, basi katika

imani zao katika misikiti hata katika makanisa, ili kuweza kuhakikisha amani hii tuliyonayo tunaendelea kuwa nayo. Kwani mipango mizuri, maendeleo ya nchi yetu, biashara zetu, kilimo chetu, ibada zetu, hazitafanyika itakapokosekana amani katika nchi yetu. Hivyo, niombe sana kwamba, tuendelee kuidumisha amani hii tuliyonayo.

Mhe. Naibu Spika, niendelee na mchango wangu katika Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar. Kwanza nichukue fursa hii kuipongeza kwa kazi nzuri ya kuendeleza daftari la kudumu hali ambayo kila mtu atapata haki yake kwa mujibu wa sheria.

Niombe sana Ofisi ya Makamu wa Pili kuhakikisha Tume inapatiwa fedha ilizopangiwa katika kutekeleza majukumu yake ziweze kupatikana kwa wakati ili Tume iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi mkubwa, hali ambayo itaifanya Tume hiyo kutolalamikiwa na kufanya uchaguzi huu uweze kuwa huru na wa haki.

Mhe. Naibu Spika, wito wangu kwa wanasiasa wenzangu kuiacha Tume iweze kufanya kazi zake bila ya kuingiliwa kati, tukiingilia kati maana yake tutaikosesha huo uhuru ambao tumeweza kuipa kwa ridhaa kisheria.

Mhe. Naibu Spika, naiomba sana Tume kutoa elimu kwa wapiga kura wakati ukifika ili waweze kuchagua viongozi wao kwa umakini mkubwa. Pia itoe elimu kwa wale wanaolalamika kukoseshwa haki zao lakini kumbe wanalazimisha kuandikishwa katika sehemu ambazo hawajakamilisha sifa za kuandikishwa mahala hapo.

Mhe. Naibu Spika, niendelee na mchango wangu katika Baraza la Wawakilishi. Baraza ni chombo kikubwa pia ni muhimili mwengine ambao unapaswa kujitegemea wenyewe, kutokana na majukumu yake makubwa na ninamuomba sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais yeye anajua uzito wa chombo hiki, na kwamba wananchi ndio chombo chao wanachoweza kuwakilishwa.

Kwa hiyo, ni vyema mswada ule ambao tunaupigia kelele kila siku basi serikali iweze kufikiria kulifanya, Baraza liweze kujitegemea ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Naibu Spika, pia niipongeze serikali kwa hatua kubwa iliyofikia katika kuimarisha huduma za afya kwa wananchi wake kwa kutengeneza wodi ya wagonjwa mahututi *(ICU),* jambo ambalo lilikuwa ni kilio chetu cha muda mrefu.

Vile vile huduma ya upasuaji wa vichwa na uti wa mgongo jambo ambalo tulikuwa hatuna kabisa huduma hii. Tulikuwa tunapata tabu ya kuwasafirisha wagonjwa kwenda Muhimbili na kwengineko, hali ambayo ilikuwa inachukua gharama

kubwa kwa wananchi wetu na tukiangalia ni wanyonge kabisa. Kwa hiyo, naipongeza serikali kwa hatua hiyo.

Mhe. Naibu Spika, niendelee na mchango wangu katika mapambano dhidi ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia. Napenda kuungana na Mhe. Makamu wa Pili katika hotuba yake hii ya kupiga vita mambo haya ya udhalilishaji wa kijinsia wanawake na watoto, wanaopatikana na hatia hizi au vitendo hivi vya udhalilishaji basi wapatiwe adhabu iliyo kali, kwa sababu inaonekana bado adhabu wanayopewa haijalingana na ule ukatili wao wanaoufanya. Kitendo wanachokifanya ni cha kinyama kabisa, kwa hiyo adhabu iongezwe ili iweze kuwa funzo kwa wenzao wengine.

Mhe. Naibu Spika, niende katika Idara ya Maafa. Idara hii kwanza maafa yanapotokea huwa hayapigi hodi ni jambo la kushtukizia tu. Kwa hiyo, niiombe sana serikali iwe makini katika ujenzi wa miundombinu, kuhakikisha tunapata wakandarasi wazuri ili kujiepusha na yale ambayo tunaweza kuyaepuka.

Pia niwaombe tu wenzangu tusiilalamikie serikali na kuitupia madongo sana, kwa sababu tuelewe pia haya yanaletwa na nguvu za Mwenyezi Mungu, hakuna anayeweza kulizuia jambo ambalo Mwenyezi Mungu amelishapanga lifanyike, tunaona mifano nchi mbali mbali ambazo za wenzetu zenye miundombinu mizuri lakini mafuriko yanakuja na yanachukua majengo mbali mbali.

Kwa hivyo sisi tuwe makini kumuomba Mwenyezi Mungu atusaidie katika ujenzi wetu, lakini pia tusisahau uwezo wa Mwenyezi Mungu upo.

Mhe. Naibu Spika, mwisho mimi nimalizie kwa kutoa wito kwa wananchi wa Zanzibar. Kuangalia kwa makini kabisa juu ya utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ambayo imetokana na CCM. Ni nini iliahidi na nini imeweza kutekeleza na imani yangu imetekeleza mambo kwa kiasi kwa asilimia kubwa sana. Kwa hivyo, niwaombe wananchi wote kuhakikisha tunalinda amani na utulivu ili tuweze kufikia hayo mengine mazuri yote ambayo tumejipangia kuyafanya.

Pia katika shukurani zangu kwa Serikali juu ya utendaji wa kazi zake niseme pia changamoto zipo. Kwa sababu huwezi kuwa na mafanikio halafu kusiwe na matatizo. Pahala popote penye mafanikio na matatizo yapo. Sasa niombe Serikali kwa yale mapungufu ambayo tunayo na ninaiomba Serikali hii makini, kwa sababu inaona wala haijasema kama pale ambapo hawakufanikiwa wakasema tumefanikiwa, wanaeleza ukweli kwa lile ambalo wameweza kufanikiwa wanalieleza, na lile ambalo bado hatujaweza kufanikiwa wamelieleza. Kwa hivyo, mimi niiombe Serikali pale ambapo tuna mapungufu hatujaweza kufanikiwa basi

tuweze kuondosha changamoto hizo ili wananchi wetu waondokane na matatizo ya kijamii.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa niseme CCM itashinda kwa uwazi kutokana na sera zake madhubuti, sera ambazo zinatekelezeka, sera ambazo zinauzika kwa wananchi wake. Kwa hivyo CCM itashinda kwa uwazi na si kwa siri ya ushindi.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hotuba hii ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa asilimia mia. Ahsante sana. (*Makofi*).

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante sana Mheshimiwa tunakushukuru. Sasa nafasi tunampa Mhe. Omar Ali Shehe, afuatie Mhe. Mgeni Hassan Juma, Mhe. Mohammed Mbwana Hamad na Mhe. Wanu Hafidh Ameir.

**Mhe. Omar Ali Shehe:** Mhe. Naibu Spika, na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi hii walau kuweza kusema mawili matatu juu ya bajeti ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais.

Mimi sina budi Mhe. Naibu Spika, nimpongeze Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa namna alivyowasilisha bajeti yake hii ambayo ina maneno mazuri. Kama ukiyatafakari utaona kwamba ni dhahiri kuna mwelekeo mkubwa mbele kwetu. Lakini pia nimpongeze rafiki hapa, kaka yangu Mohamed Aboud kwa namna anavyomsaidia Mhe. Makamu wa Pili wa Rais katika kutekeleza majukumu yake. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, Ofisi hii ni ofisi muhimu sana, kwa sababu inasimamiwa na Makamu wa Pili wa Rais ambaye kwa mujibu wa Katiba yetu ni ndiye mmoja kati ya mshauri wa Rais.

Pili Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ina jukumu kubwa la kusimamia shughuli za utendaji wa Serikali katika Baraza la Wawakilishi. Tunaona kwamba muhimili wa Serikali katika Baraza namna gani kama upo makini au namna gani kama upo dhaifu, inavyoweza kupelekea Serikali yenyewe kwa kweli ikawa inayumba na haitekelezi vizuri zile ahadi pamoja na mambo ambayo wameahidi kwa wananchi. Kwa hivyo, kwa ujumla ofisi hii ni ofisi muhimu sana kwa vile inaongozwa na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais.

Mchango wangu leo hautokuwa mkubwa sana, lakini kwanza naomba niulizie na nielezee masikitiko yangu kwa namna Ofisi ilivyoshindwa kutekeleza ahadi. Tunakumbuka katika Mabaraza mawili yaliyopita Mhe. Naibu Spika, Serikali

katika Baraza hili iliahidi kuleta ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, zile ripoti ambazo zilikuwa zina ukaguzi maalum.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alifanya ukaguzi maalum wa kukagua mishahara hewa, lakini pili kukagua ile Kampuni ya *PHILTEX* kule Dubai. Sisi Wawakilishi kwa niaba ya wananchi wetu tulidai na hatimaye Serikali kwa kweli iliahidi. Mimi binafsi niliandika hoja binafsi na Mhe. Spika akanieleza kwamba hoja ile niiondoshe kwa sababu tu imeahidi kuleta ripoti zile Barazani.

Mhe. Naibu Spika, ninasikitika sana kwamba tunamaliza Baraza hili, baada ya Baraza hili litavunjwa na sidhani kama tutapata fursa nyengine ya kuzipata ripoti zile. Ni kitu cha masikitiko makubwa, kwa sababu imetukosesha sisi Wawakilishi tufahamu ukweli juu ya kilichomo katika ripoti zile.(*Makofi*).

Lakini la pili, limewakosesha wananchi fursa nzuri ya kujua kilichomo katika fursa ile. Mhe. Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa sana kwa kweli ninasikitika kwa nini Serikali ikashindwa kutekeleza ahadi yake katika chombo hichi. Na mimi ninasema kitendo cha Serikali kutokuleta ripoti zile ni kitendo cha Serikali kutudharau sisi Wawakilishi halali wa wananchi wa Zanzibar. Haikubaliki wala haipokeleki katika utawala huu ambao tunaosema ni utawala bora, haikubaliki! (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, lakini vile vile tunayo Kamati yetu ya *PAC*, na ninakumbuka kuna wakati fulani Mhe. Makamu wa Pili wa Rais tulimuomba kama Kamati, kwa sababu tunafahamu sote umuhimu wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Mahesabu ya Serikali na ambavyo inatakiwa ijengewe uwezo katika kuzitafsiri ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Tuliiomba Serikali kwamba Serikali pamoja na majukumu haya lakini tunaiomba Kamati yenu hii ipatieni mafunzo. Serikali ikaahidi, bahati nzuri tukapigwa na picha na masaini tukatia Wajumbe wa Kamati, purupuru kwamba kaeni tayari mkao wa safari. Ninasikitika kwamba tunamaliza Baraza hili keshokutwa linavunjwa ahadi ile hatukujua imefikia wapi. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, leo mimi kwa upande wangu ni siku ya masikitiko licha ya Makamu wa Pili wa Rais kufanya kazi zake vizuri lakini hilo limekuwa ni dosari. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka na hilo naomba niende kwenye Idara ya Maafa. Mhe. Naibu Spika, nchi yetu ni visiwa, na kwa sababu ni visiwa kwa kweli uwezekano wa kutokea maafa ni mkubwa sana. Tunakumbuka miaka katika awamu hii hatujasahau ilivyozama meli ile ya *MV. Spice Islanders*, tukatokea na ajali nyengine. Lakini vile vile ni juzi tu mafuriko ambayo kwa kweli yamewaacha wananchi wetu wengi ambao hawana makaazi na hawajui hatma yao kufuatia mafuriko hayo.

Mhe. Naibu Spika, Mwenyezi Mungu aendelee sisi kutuepusha na maafa mengine makubwa zaidi, lakini dhahiri ni kwamba tumepata maafa ya kuzama kwa meli, maafa ya mafuriko. Ni juzi tu wenzetu wa Kisiwa Panza walipata maafa makubwa kupitia upepo uliovuma.

Mhe. Naibu Spika, kwa wale wenye kuangalia vyombo vya habari na kufuatilia kwa karibu, juzi katika visiwa vya Vanuatu takriban nchi nzima ilihaghariki kwa ajili ya upepo; gharika ya upepo. Mwenyezi Mungu sisi atuepushe na hilo.

Mhe. Naibu Spika, lakini pamoja na yote baada ya kutokea yaliyotokea ndani ya nchi yetu, na baada ya kupata uzoefu katika nchi duniani kwa gharika hizi zinazotokea ambayo sehemu kubwa yanatokana na mwenyewe Mwenyezi Mungu, sababu mwenyewe Mwenyezi Mungu. Kwa vyovyote vile Serikali Mhe. Naibu Spika, ilikuwa katika bajeti ijidhatiti na ijipange sana katika kukabiliana na maafa haya. Bahati mbaya hali ilivyo sasa tunashuhudia kwamba Serikali bado kabisa haijajipanga. Tunasubiri maafa yatokee, wafanyabiashara wachangishwe, watu wengine waende wakapeleke vigodoro, sukari, mafuta ya taa na vitu vyengine mbali mbali. Mhe. Naibu Spika, jambo hilo ni jambo ambalo halitoi sura nzuri kwa Serikali hasa Serikali iliyo makini. Serikali iliyo makini Mhe. Naibu Spika, hujiandaa, hujipanga, hujitayarisha katika kukabiliana na maafa. Lakini hali ilivyo sasa kwa kweli inasikitisha sana kwa Serikali yetu.

Kauli ya Serikali katika bajeti hii mimi nimeifahamu na ina kauli nzuri kupitia Hotuba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kwamba imepanga kuimarisha mfumo wa kisheria na kitaasisi wa kujiandaa na kukabiliana na maafa nchini kabla, na hili neno kabla naomba likozeshee sana, *"kabla, wakati na baada ya maafa*", ni maneno mazuri sana na ni mipango mizuri sana kwa mujibu wa maelezo.

Mhe. Naibu Spika, lakini tumeambiwa kwamba ni lengo la Serikali kuijengea uwezo jamii katika kuhimili maafa. Haya ndiyo mambo tunayoyahitaji lakini tunataka haya yasiwe ni maneno, kwa sababu maneno unaweza ukasema utauza dagaa kwa helikopta, ni maneno mazuri na kila mmoja anafurahi kuona dagaa linauzwa kwa helikopta katika nchi hii, lakini je, uhalisia ukoje?

Mhe. Naibu Spika, uhalisia tuangalie bajeti. Maneno haya mazuri yametafsiriwa kibajeti. Katika kupekuapekua kwangu Mhe. Naibu Spika, nimeona kwamba Serikali imetenga katika mwaka huu wa fedha; jumla ya milioni mia nne na kumi, laki tisa na sabini elfu kwa mwaka huu, mia nne na kumi na saba. Lakini hata kwa *projection* kwa bajeti ya mwaka kumi sita na kumi saba imezidisha kidogo kama milioni mia nne ishirini na moja, nukta kidogo imeongeza.

Sasa Mhe. Naibu Spika, katika mchanganuo huo imeeleza kwamba mwaka huu katika uratibu wa shughuli itatumia mia tatu na sitini na saba, na katika mradi ule wa kujengea uwezo ni milioni hamsini.

Mhe. Naibu Spika, binafsi ninapata tabu sana, kwa sababu mategemeo yetu wananchi ni nini. Sisi wananchi tulikuwa tunataraji nini. Tunataraji mambo hayo lakini eneo gani.

Maafa mara nyingi yanayotokea ni katika upande wa bahari. Maafa katika kukabiliana na maafa katika upande wa bahari ni kuwa na meli za kisasa, tunashukuru meli ipo njiani inakuja itafika keshokutwa, eeh! Lakini je, pale inapotokea sasa bahati mbaya nini kifanyike. Ni mategemeo yetu wananchi kuiona Serikali inajiandaa katika suala zima linalohusiana na uokozi. (*Makofi*).

Suala zima linalohusiana na uokozi. Je, katika nukta hiyo uokozi sasa Serikali inatwambiaje. Na uokozi wa bahari tunaujua, si suala la kupishana na meli imeshachukua watu, ikaambiwa meli imeshazama nendeni mukateremshe watu murudi muje muchukue, hiyo haiwezekani. Maana yake tunachotaraji tuwe na chombo ambacho kipo *standby*, kwamba *anything happen* wakati wowote kina-*start* watu wanakwenda shughuli. Lakini na mazingira ya bahari.

Mhe. Naibu Spika, hivyo kweli hata helikopta, nikisema hata helikopta isionekane ni kitu kidogo, ninajua ni kitu kikubwa, lakini kwa nchi tunashindwa na helikopta. Hivyo kweli helikopta mpaka tukafuate Tanzania Bara, tuwapigie simu waje na helikopta, maana yake mazingira ya bahari kwa nyakati zote unapoweza kuangalia kitu cha baharini huwezi kuangalia ni lazima upate chombo kilichoko juu uangalie chini. Serikali ina mpango katika hili, kwa sababu sisi wananchi tunategemea tupate kitu kama hicho masuala mazima ya uokozi.

Kwa hivyo, kwa sababu bajeti mara hii imekuja na programu na bahari mbaya programu haichambui. Sasa mimi Mhe. Naibu Spika, kwa sababu siridhiki na hatua hii ninakusudia kutumia ile Kanuni ya 98 (6)(b), kwanza kwa sababu inahusiana na sera sikubaliani nalo. Sikubaliani na Serikali namna ilivyojiandaa katika kukabiliana na maafa.

Mhe. Naibu Spika, watu wanasema, *"Prevention is better than cure"*. Kukabiliana na maafa, maana yake ni kujikinga na baadae kukabiliana inapotokea ni jambo la msingi sana. Sasa kwa bajeti hii iliyotengwa Mhe. Naibu Spika, ninatangaza nia yangu ya kutoa shilingi mia ili kumtaka Mhe. Waziri aje anipe uchambuzi, kwa sababu hapa haikuchambuliwa, inatajwa fungu tu. Kwa hivyo fungu hili amelipanga kupata nini na nini, kwa sababu hofu yangu nini.

Hofu yangu kwamba pesa hizi ziishie kwenye semina. Maana yake inawezekana kwamba hii milioni mia nne ikaishia kwenye semina vitafunio tu. Kwa hivyo, ninamuomba Mhe. Waziri atakapokuja aje anipe uchambuzi juu ya matumizi ya fedha hizi milioni hamsini zinatakiwa nini, na hii milioni mia tatu na sitini na saba ni nini tukatumie tutapata angalau madau mawili. Madau maana yake meli, hatupati lakini madau tutapata eeh! ma-*life jackets* tutapata, mafuta je, yatakuwepo *standby*, yale mambo ya kutafuta wafanyabiashara wakafanya shughuli zao na kutupa vigodoro je. Kwa hivyo naomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa aje anipe uchambuzi juu ya hili ili baadae kama nitaridhika nitairejesha shilingi mia.

Mhe. Naibu Spika, niondoke kwenye maafa nije kwa Baraza la Wawakilishi. Mhe. Naibu Spika, Baraza la Wawakilishi kama Bunge letu Zanzibar ni chombo muhimu sana, na tunafahamu kwamba msingi wa maendeleo wa nchi yoyote ile ni kuwepo na Serikali madhubuti. Serikali madbubuti haiwezi ikatokea kama hakuna Bunge madhubuti. Bunge makini huzaa Serikali makini, na tunapokuwa na Serikali makini ndiyo msingi mkubwa wa utawala bora na ndiyo msingi mkubwa wa demokrasia na ndiyo msingi mkubwa wa maendeleo ya nchi yoyote duniani.

Tukiwa na Baraza makini, tutakuwa na Serikali makini na hapo maendeleo tutayapata maendeleo endelevu na ya muda mfupi. Sasa tatizo langu Mhe. Naibu Spika, ni kwamba Baraza letu bado lina uwezo mdogo sana katika shughuli za utendaji. Nikisema uwezo mdogo sikusudii uwezo mdogo wa Wajumbe, hapana, ninakusudia uwezo mdogo katika kuliwezesha Baraza kutekeleza kazi zake.

Katiba yetu imetwambia wazi wazi kwamba Baraza la Wawakilishi ndiyo chombo kikuu cha kusimamia utendaji wa Serikali. Sasa ikiwa Baraza hili lina mamlaka ya kusimamia utendaji wa shughuli za Serikali na tunafahamu pamoja na udogo wa Serikali yetu yenye Wizara kumi na sita, Maidara, Mashirika na vitu vyengine. Maana yake ni kwamba tunatakiwa tuwe na Baraza ambalo litakuwa na uwezo ambao sawa na uwezo wa Serikali katika kusimamia kwake.

Mhe. Naibu Spika, tumeshuhudia kwamba kwa mwaka huu wa fedha 2015/2016, bajeti yetu ilipungua ukilinganisha na bajeti ya mwaka jana. Bajeti ya mwaka jana pia ilipungua ukilinganisha na bajeti ya mwaka juzi. Maana yake nini. Maana yake *trend* ya bajeti ya Baraza la Wawakilishi Mhe. Naibu Spika, inapungua kila tukienda mbele, wakati tunataraji kwamba bajeti ya Baraza iongezeke.

Leo imekuwa ni kinyume chake na ukisema unapunguza bajeti ya Baraza, maana yake unapunguza shughuli za utendaji za Baraza, unapunguza uwezo wa Kamati kufanya kazi, unapunguza hata kufanyika kwa vikao havifanyiki. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, ni aibu. Leo Baraza la Wawakilishi Wajumbe hawa wanakopwa, leo tunakwenda kwa mikopo, ni aibu! Unalipwa leo vikao vya nyuma hulipwi, maana yake nini. Nina hofu kwamba tutaondoka hapa na madeni. Baraza hili litavunjwa tuna madeni, ni aibu, haiwezekani! Tutafanyaje sisi kazi katika mazingira ya kukopwakopwa, haiwezekani Mhe. Naibu Spika. Munatufanya hivi Serikali kwa makusudi ili tushindwe kufanya kazi zetu. (*Makofi*).

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, katika kuitafutia muarubaini wa suala hili, tulikuja na wazo kwamba na hata Rais, mimi binafsi nilikuwa ni mmoja kati ya Wajumbe waliokwenda kumuona Rais, na Rais wetu katwambia hamu yake kubwa ni kwamba lazima kabla ya kumaliza Baraza hili tayari Sheria ya Utawala wa Baraza iwepo. Ninataka nione sasa yale maneno Rais yameangukia wapi juu ya kuwa na sheria inayoongoza Baraza.

Mhe. Naibu Spika, haiwezekani lazima tuwe na sheria yetu. Hichi ni chombo kama muhimili ilivyo mihimili mengine, haiwezekani kwamba Baraza hili ligeuzwe kama vile Idara ya Misitu na ndivyo inavyokwenda sasa kama Idara ya Misitu tu. Ni Idara kama Idara nyengine ya Serikali na ndiyo lengo la Serikali kulifanya Baraza kama ni Idara.

Hatuwezi kuimarisha demokrasia, hatuwezi kuimarisha utawala bora, na hatuwezi tukapata maendeleo ya kweli kama chombo hichi kitabakia na sura iliyo sasa, haiwezekani!

Na kwa msingi huo naomba nishauri hata mfumo huu wa uundaji wa bajeti hizi programu Mhe. Naibu Spika, mimi ningefurahi kwamba walau tungekuwa na hizi *programmes* mbili, *okay*. *Programmes* zilizopo ni mbili lakini basi walau tungelikuwa na *sub-programmes* kwa sababu haiwezekani kwamba tukawa na *programme* ya utawala na uendeshaji, hiyo ni programu nzima. Lakini tukawa na programu inayohusiana na mambo ya vikao, mambo ya mafunzo na nini, angalau hizi zingechambuliwa kuwa ni *programs* ndogo na yakatengewa fungu yake yaliyo wazi tukayaona. Kwa sababu humu tumeshuhudia kwamba kuna idara tu au wizara ya serikali ina program na *sub program* nyingi, leo chombo kikubwa kama hiki mnakipa *program* mbili tu, wakati kuna masuala ya uendeshaji, kuna masuala ya vikao vya kamati, kuna masuala ya mafunzo, kuna masuala ya kuwawezesha Wajumbe na kuna ofisi Pemba kule. Kwa nini hizi musizichambue zikawa ni *sub programs* zile na mafungu yake yakaonekana yakawa wazi, maana yake hiyo ni katika kudhihirisha kwamba bado mnaendelea kulidhalilisha Baraza, mkalifanya lisiwe kama ni chombo huru kinachoweza kuisimamia serikali.

Mhe. Naibu Spika, naomba niondoke kwenye Baraza nihamie sasa kwenye Tume ya Uchaguzi.

Mhe. Naibu Spika, mwaka huu ni mwaka wa uchaguzi, kila mmoja wetu aombe amani na asiombe amani kwenye mdomo, kwa sababu ukiomba amani kwenye mdomo ni tatizo. Aombe amani kwenye *qalbi* yake, amani ina umuhimu sana Mhe. Naibu Spika.

Sisi ambao tulikuwepo katika chombo hiki kabla ya maridhiano haya tunafahamu nini kilitokea. Sisi wenyewe Wajumbe tulikuwa tukichungana humu, ukionekana unazungumza na mtu wa CCM tayari, wa CCM akionekana anazungumza na Omar Ali Shehe tayari, inakuaje. Pemba kule Wajumbe wakiondoka wanakwenda kwa kujificha ficha, hapa Unguja walikuwa wakijificha ficha.

Mhe. Naibu Spika, tuendelee kuwapongeza viongozi wetu waliotuletea hali hii ya maridhiano ni kitu kikubwa sana.

Suala la amani Mhe. Naibu Spika, hakuna isiyomfaa, kila mmoja humu anafaliwa na suala la amani na ikichafuka amani hakuna bingwa. Hata huyo Makamu wa Pili wa Rais, hata Rais, hata Makamu wa Kwanza wa Rais, wote wataathirika.

Mhe. Naibu Spika, nakumbuka siku moja pale Chake Chake katika kipindi kile cha kutokuwa na amani, alitoka Rais Ikulu anataka kwenda Uwanja wa Ndege. Rais anatoka Ikulu Tibirinzi pale anautaka Uwanja wa Ndege lakini ulimshinda. Rais hivyo, sio Omar Ali Shehe, hapana, Rais, ilibidi apitishwe Tenga kwenye soko la samaki kule, aikamate hospitali apitie Kichungwani Rais. Hivyo ndivyo amani inavyoharibika. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, naomba sana tena sana, na kwa hili tunalia, kwamba kipindi hiki jamani tuepukeni sana haya mambo.

Mhe. Naibu Spika, suala hili naomba niiambie Tume ya Uchaguzi. Tume ya Uchaguzi wana jukumu kubwa sana na wana dhima kubwa sana, wasimame Tume ya Uchaguzi kwa kweli kama Tume ya Uchaguzi, wasikubali maelekezo, kwa sababu mwisho wa siku wao ndio watakuwa mas-ul. Kama watatufuata sisi wanasiasa mwisho wa siku Tume ya Uchaguzi watakuwa ni mas-ul, kwamba wao ndio watakaowajibika na chochote kile kitakachokuja, na kama amani itaharibika, hii bajeti tukumbuke Waheshimiwa Wajumbe, kwamba bajeti hii asilimia kubwa inategemea mapato ya utalii, hivi mtalii gani atakuja hapa.

Mhe. Waziri wa Fedha ananiambia kwamba ili tuweze kuitekeleza aweze kukusanya maana yake sehemu kubwa tunategemea utalii. Ni mtalii gani kipindi hiki atakuja kabla ya uchaguzi ikiwa hali itaharibika, ni mtalii gani atakuja baada ya uchaguzi hatujui hata itachukua muda gani, Mwenyezi Mungu kwa kweli atuepushe na hilo.

Mhe. Naibu Spika, sasa naiomba Tume ya Uchaguzi wawe makini. Tume ya Uchaguzi wafanye kazi zao kwa uwazi kama walivyosema wajumbe wenzangu, lakini zaidi Tume ya Uchaguzi wafanye kazi zao kwa uadilifu wa hali ya juu na Mwenyezi Mungu atawasaidia.

Katika hilo naomba nimalizie kwa kuuliza swali moja tu, kwamba tuliambiwa hapa karibuni kulikuwa kuna uandikishaji wa mwisho ambao ulikuwa uanze tarehe 16, sasa uandikishaji ule utakuwa lini na ni sababu gani zilizopelekea uandikishaji ule usifanyike kwa muda ambao ulitakiwa. Nasema hili kwa hofu kwamba ikiwa muda utakwenda mbele, uandikishaji utamalizika lini na lini Tume wata-*display book* hili, maana yake kadiri tunavyokwenda sasa muda unavyokwenda ndivyo ambavyo kwa kweli ule uwezekano wa kupatikana kwa daftari ili kila mmoja akajihakikishia utakuwa ni mdogo. Sasa namuomba Mhe. Waziri atakapokuja aje anipe sababu, na hivyo hivyo aniambie kwamba ni lini uandikishaji utakuwa na utamaliza.

La mwisho je, wadau wa vyama, sisi wadau kama vyama, ni lini tutalipata daftari ili kila mmoja ajiridhishe, kwa sababu mwisho wa siku maana yake ni kila chama kama walivyofanya miaka ya nyuma, kila chama kipatiwe daftari, ili kila mmoja ajiridhishe na ndio huo uwazi tunaousema, huo ndio uwazi tunaousema, kwamba kila mmoja aridhike ndio uwazi huo.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, namalizia kwa kumpongeza tena Makamu wa Pili wa Rais, lakini vile vile nimpongeze Naibu wake, kwa kazi nzuri wanazofanya, na ni imani kwamba watafanya vizuri zaidi katika kuona kwamba wanalivusha jahazi letu katika kipindi hiki ili hatimaye Zanzibar sote tushinde katika suala hili. Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

**Mhe. Mgeni Hassan Juma:** Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi kuweza kuchangia katika hotuba ya Makamu wa Pili wa Rais.
Awali ya yote namtanguliza Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehma, aliyetupa uzima wa afya wa kuweza kuja hapa na kufanya shughuli zetu za kawaida.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru na wewe kwa kunipa fursa hii vile vile ya kuweza kuchangia katika hotuba ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Naibu Spika, nampongeza sana Makamu wa Pili wa Rais kwa kutuwasilishia hotuba ambayo ina muelekeo mzuri, hasa kwa kuzingatia mambo ambayo nitayataja.

Mhe. Naibu Spika, kama walivyosema wenzangu wengi, nampongeza sana Makamu wa Pili wa Rais pamoja na viongozi wetu wakuu wa kitaifa akiwemo Rais mwenyewe Dkt. Ali Mohamed Shein, pamoja na Makamu wa Kwanza wa

Rais Maalim Seif Sharif Hamad, kwa kuweza kulisukuma gurudumu hili na kuweza kushirikiana wote kwa pamoja katika kuhakikisha nchi hii inakuwa na amani na utulivu.

Mhe. Naibu Spika, maendeleo ya nchi yoyote hayaji bila ya amani na utulivu. Shughuli zozote za kiuchumi haziwezi kwenda bila ya amani na utulivu, lakini hata na sisi wananchi pale panapokuwa hapana amani na utulivu hatuwezi kuishi maisha ya kawaida.

Kwa hivyo, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ana jukumu kubwa katika kuhakikisha kwamba wananchi wake wanaishi kwa amani na utulivu, na katika uongozi wake amefanikiwa kwa hilo. Tumpongeze sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kwa kweli katika kipindi cha miaka mitano ameweza kutuletea amani na utulivu kama ndio kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, niseme tu kwamba kutokana na amani ambayo tumeipata tumeweza kufanikiwa katika kukuza uchumi wa Taifa letu, lakini tumeweza kufanikiwa katika masuala ya huduma.

Tumeona kwamba uchumi wetu umekuwa hasa katika sekta ya huduma kwa sababu tumekuwa na amani na utulivu, hilo lazima tulijue. Sekta ya huduma haiwezi kuwepo ikiwa hapana amani na utulivu. Kwa hivyo, hilo ni muhimu, lakini vile vile suala la usafiri, suala la mawasiliano, pamoja na mipango, sera na mikakati ya kuendeleza nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka nirudi nyuma katika hotuba aliyotoa Mhe. Waziri wa Fedha, ambayo alisema moja katika mikakati na mipango ya serikali ni kuhakikisha kwamba kutapatikana elimu bora.

Niipongeze sana serikali yetu kwa kweli kwa kuweza kulisimamia hili. Nasema hivi kwa sababu tumeona namna serikali ilivyoweza kujipanga, kwanza kuhakikisha kwamba tunaendelea kuwa na skuli nyingi zaidi ya hizi ambazo tulizonazo, lakini vile vile kuweza kuhakikisha kwamba watoto wetu wanapata madeski ya kukalia kwa ajili ya kupata elimu bora.

Mhe. Naibu Spika, jengine kubwa ambalo limefanyika na limetiliwa nguvu ni kuhakikisha kwamba walimu wetu wanaongezewa uwezo katika daraja mbali mbali. Lakini kubwa kabisa ni lile ambalo sote tumeliunga mkono ndani ya Baraza, kwamba Mhe. Rais ametangaza rasmi kufuta michango katika skuli za msingi, pamoja na michango ya mitihani katika skuli za sekondari.

Mhe. Naibu Spika, jengine ni kwamba kuna mambo mengi ambayo yamefanyika katika awamu hii, ikiwemo kuhakikisha kwamba wananchi wanapata afya bora. Tumeona kwamba kitengo cha *ICU* ndani ya Hospitali ya Mnazi Mmoja kimewekewa huduma za kisasa. Vile vile tumeona kwamba huduma nyengine ambazo zilikuwa zinahitajika ndani ya Zanzibar kuwepo.

Kwa mfano, kufanya *operation* ya vichwa pamoja na uti wa mgongo, kwa kweli zimeanza kufanyiwa kazi na tumeona kitengo hicho kimeanza rasmi. Kwa hivyo, lazima tuipongeze serikali yetu kwa kuchukua juhudi hiyo.

Jengine Mhe. Naibu Spika, ni lile la kusambaza maji. Tunajua kwamba maji ni muhimu sana katika maisha yetu, bila ya maji hakuna mtu ambaye anaweza kuishi, lakini serikali yetu imejitahidi imesambaza maji katika maeneo mbali mbali, licha ya kusambaza lakini imefanya ukarabati mkubwa wa kulaza mabomba na kuhakikisha kwamba wananchi wake wanapata maji.
Hali ilivyokuwa nyuma sivyo ilivyo sasa hivi. Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba kuna kasoro na hata hizo nchi ambazo zinaendelea basi kasoro zinajitokeza.

Mhe. Naibu Spika, jengine ambalo nataka kulizungumza, ni suala ambalo lilizungumzwa katika kitabu au katika hotuba hii ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ni suala zima la mazingira.

Mimi niipongeze sana serikali hii kwa kuhakikisha kwamba tunayaweka vizuri mazingira haya tuliyonayo na kuwashajihisha wananchi katika kuwapa elimu, ili vizazi vyetu vinavyokuja viweze kuishi katika mazingira mazuri.

Mhe. Naibu Spika, suala la mazingira ni suala la mtambuka. Kila mtu anafahamu kwamba mazingira yanaweza kusababisha majanga makubwa na tukiharibu mazingira basi tumeharibu maisha yetu.

Mimi niipongeze sana serikali hii kwa kuliona hilo, lakini niombe tuzidi kuwashajihisha wananchi wayalinde mazingira yao, kwa sababu leo tunaishi sisi, kesho tuwaachie na wengine waweze kuishi katika mazingira mazuri.

Mhe. Naibu Spika, suala la kupanda miti ni muhimu sana. Tumeona juzi tu maafa ya mvua namna ya baadhi ya nyumba zilivyoanguka, kwa sababu hazina vizuizi vya miti, zimeporomoka na maji kwa sababu hakuna kizuizi chochote cha kuweza kuifanya ile nyumba au ile ardhi iwe imara. Kwa hivyo, serikali iendelee na ijitahidi sana kuhakikisha kwamba inafanya hivyo ili kuhakikisha ustawi wa wananchi uko vizuri.

Mhe. Naibu Spika, wenzangu waliotangulia walizungumza suala la majanga. Kwa kweli ni muhimu sana tulizungumze hili, vile vile tujue kwamba elimu ni muhimu sana. Mengine yanafanyika kwa wananchi wetu kutokuwa na elimu.

Majanga ni suala ambalo kwa upande mmoja linaweza kudhibitiwa, lakini lazima wananchi wajue pale wanapofikwa na majanga wafanye nini.

Mhe. Naibu Spika, miaka kama minane iliyopita nilipata bahati ya kuonana na mmoja wa kiraia kutoka Europe, walikuja hapa wanaitwa *Women Without Borders* kabla sijaingia ndani ya Baraza hili nilikutana nao. Kwa kweli walipokuja hapa walizungumzia suala la elimu kwa watu wa Zanzibar katika masuala ya kuijua bahari vizuri ikiwemo kuogelea.

Mhe. Naibu Spika, nakumbuka wakati maafa yalipotufika ilipopinduka meli ile ya mwanzo, kulikuwa na abiria kutoka nje kama kumi, sina kumbukumbu vizuri, aliyepoteza roho ni mmoja, wengine walitoka salama, kwa sababu wenzetu wanaijua bahari. Lakini msingi unatokea wapi, msingi unatokea tangu wakiwa wadogo wanapewa mafunzo ya kuyajua mazingira yao, hilo ni muhimu sana, na mara nyingi ndio hapo tunapokosea hata katika mitaala yetu ya elimu, kwamba kwanza hatuyasomi mazingira yetu vizuri sana, na vitu vyengine ni *very practical* sio *theory* ambayo watoto wanasoma kwenye kitabu.

Wale wanawake wakaniambia kwamba inashangaza kwamba asilimia kubwa ya Wazanzibari ambao wanaishi ndani ya kisiwa lakini hawajui kuogelea, tunaweza kuliona ni jambo jepesi sana lakini ni jambo muhimu sana. Hebu sasa tujipange.

Mhe. Naibu Spika, hata hii mvua iliyokuja kwa hali iliyokuwepo katika maeneo mbali mbali, tayari kulikuwa kuna maji ya kuweza kutosha kusema kwamba imekuwa kama bahari, sasa kuna watu wamo ndani ya majumba yale watatoka vipi. Lazima wafahamu watu namna ya kujikinga na maafa yanapowakuta, elimu hiyo ni muhimu sana kuipata wananchi, au sivyo kila siku kutakuwa na kilio cha kupoteza maisha ya watu, pamoja na majeruhi wengi.

Mhe. Naibu Spika, nizungumzie hilo pamoja na lile la ajali za barabarani, pia tatizo ni kubwa sana, na hili kwa kweli linagharimu maisha ya Wazanzibari wengi. Aidha, wanapoteza maisha yao au wanakuwa walemavu. Naiomba sana serikali na hili janga jengine ambalo lina umuhimu wake kuangaliwa hasa katika sheria tulizonazo za barabarani, na hasa katika kuhakikisha kwamba sheria kweli zinachukua mkondo wake, hivi hivi bado tutakuwa tunapata majanga ambayo yatakuwa na gharama kubwa katika maisha ya Wazanzibari.

Mhe. Naibu Spika, niingie sasa katika Idara ya Uchapaji. Niipongeze sana Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kuweza kuipatia vifaa mbali mbali idara hii.

Nakumbuka mpango huu ulikuwa ni wa muda mrefu, lakini umetimia na mimi niipongeze sana sana wizara hii.

Vile vile niseme tu kwamba hii idara isiwe idara ambayo kila siku inapokea ruzuku kutoka serikalini. Mhe. Naibu Spika, tumeona bajeti za serikali namna zinavyopungua kila siku. Kubwa ni kwamba bado tuna mashirika ambayo yanategemea serikali. Lakini idara hii kwa uwezo iliyopewa hivi sasa basi iweze kuzalisha na iweze kujiendeleza wenyewe. Hilo ni muhimu sana Mhe. Naibu Spika, na serikali ina wajibu wa kuitangaza wizara hii kuhakikisha kwamba soko lake linakuwa kila siku.

Mhe. Naibu Spika, niingie katika Ofisi ya Faragha, niipongeze sana kwa hatua ambazo zimechukuliwa mbali mbali ikiwemo ya kurekebisha baadhi ya nyumba za Waheshimiwa. Lakini mimi suala langu liko pale pale na nililiuliza, lakini nikitizama hali halisi ya nyumba za Waheshimiwa yaani za viongozi wetu wakuu, zipo katika mazingira mabaya sana. Lini basi tutaanza kujipanga kuhakikisha kwamba viongozi wetu ndani ya Zanzibar lakini pamoja na Tanzania Bara wanapata makaazi bora. Inasikitisha ukiona kwamba nyumba zao kwa kweli nyingi ni mbovu, hazikaliki.

Sisi tunawathamini sana viongozi wetu watatu, tunawathamini sana. Na ni tabu ni ni aibu tunayoiona kuona kwamba wanawekwa katika mazingira yaliyokuwa hayastahiki. Sasa nakuomba Mhe. Naibu Spika, na naiomba serikali hili waliangalie.

Mhe. Naibu Spika, jengine ni la Baraza la Wawakilishi. Mimi niseme tu kwamba niwashukuru sana UNDP pamona na *UN Woman* kwa kutuwezesha sisi Wawakilishi katika kipindi chote cha miaka mitano kwa kweli wameweza kutupa uwezo na ndio maana leo ukaona asilimia 99 ya wajumbe wa Baraza hili wanaweza kusimama na kuchangia na kuweza kuiuliza serikali nini inafanya. Kwa hivyo hii ni jitihada kubwa ambayo imefanywa na washirika wetu wa maendeleo wa UNDP pamoja na *UN Woman*.

Nasema hivyo kwa fahari kabisa Mheshimiwa, kwa sababu hata na sisi wanawake *UN Woman* imehakikisha kwamba wamatupa uwezo wa kutosha, ndio maana leo unaona Wajumbe wote wanawake wanasimama akichangia wakiuliza maswali kwa kujiamini kabisa.

Mhe. Naibu Spika, niseme tu na naomba sana hili lifanyiwe kazi na Baraza la Wawakilishi, naomba sana kuhusu Kitengo cha Hansard, kimepitwa na wakati. Hali ya Kitengo cha Hansard inasikitisha sana. Ni kwamba mara nyingi sana ukienda katika Kitengo cha Hansard unakuta uwekaji wa zile *document*, hansard zenyewe haupo vizuri kabisa. Sasa hivi tunateknolojia tunaweza kuzitumia, sasa hivi tuna mambo mengi tunaweza kuyatumia lakini kitendo hiki bado hatujakitizama vizuri, kina umuhimu mkubwa.

Mheshimiwa nikwambie mara nyingi mimi nataka kupata hizi *clips* ambazo tunazichangia humu ndani na hivi karibuni walikuja waandishi wa habari kutaka *clips* zangu mbali mbali namna ninavyochangia waweze kuniweka ndani ya televisheni yao. Nasikitika sana, nafikiri wapo wengine hivyo hivyo wafatwa, nasikitika sana kwamba hazipo kabisa. Ukitafuta *reference* ya aina yoyote inayotokana na vikao vyetu hivi ya picha huipati. Hili ni tatizo kubwa lakini ni suala muhimu ambalo linatakiwa kufanyiwa kazi.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kusema kwamba sote tuna wajibu wa kujenga Taifa letu, sio serikali tu lakini na wananchi wafahamu kuwa wana wajibu mkubwa wa kujenga Taifa lao. Ningewaomba sana wananchi wenzangu kwamba amani na utulivu ya nchi yetu ni jukumu letu sisi wenyewe sio serikali peke yake. Hili ndio hoja kubwa hivi sasa, naomba sana tuhakikishe kwamba amani tunaipata, bila ya amani tutakuwa hatuna raha na hatuna pa kwenda. Tunaona Waburundi Watanzania tunawafukuza hatutaki waje na wengine wengi tunawafukuza na sisi tutafukuzwa kama wao, tusifike huko. Tunapoizungumzia amani ni kitu chenye thamani kubwa kwetu sisi. Kila mmoja ana jukumu kwa upande wake kwa kuitunza amani hii.

Nimuombe Mwenyezi Mungu atujaalie tuishi katika amani katika uchaguzi huu, tuwe na amani na utulivu utakaotupelekea kuingia katika awamu nyengine ya Dkt. Ali Muhammed Shain ambaye atatuongoza katika umoja na mshikamano wa taifa hili na hatimaye kuleta maendeleo ya uchumi wa watifa hili. Nikushukuru Mhe. Naibu Spika, lakini niseme kwamba naiyunga mkono hotuba ya Makamu wa Pili wa Rais kwa asilimia mia moja. Nakushukuru sana.

**Mhe. Naibu Spika:** Asante tunakushukuru Mhe. Mgeni, Mhe. Mbwana nikuombe kidogo, Mhe. Ali Salim anajisikia homa na anataka kidogo achangie akimbilie hospitali. Kwa hivyo nampa Mhe. Ali Salim, utafuatia wewe, baadaye Mhe. Wanu Hafidh na mwisho Mhe. Muhammed Haji Khalid na wengine nitawataja baadaye.

**Mhe. Ali Salum Haji:** Mhe. Naibu Spika, nikushukuru kwa ombi langu kwa kunikubalia kwa sababu hali yangu ya kiafya leo sio nzuri. Mhe. Naibu Spika, nitazungumza machache sana na kwa ufupi sana.

Kwanza kabisa nichukue fursa hii kumshukuru Mhe. Makamo wa Pili wa Rais nazungumzia hotuba yake ya Makadirio na Matumizi ya Mwaka huu wa Fedha 2015/16. Mheshimiwa sote tunafahamu tunaelewa jitihada za kiongozi wetu huyu hamna anavyotekeleza mambo yake kwa ufanisi kabisa.

Mhe. Naibu Spika, nataka kujaribu kuzungumza kwa kifupi kabisa na kutoa pongezi zaidi kwa namna serikali hii ilivyojitahidi katika kipindi hichi na miaka minne na nusu. Sote ni mashahidi na wanadamu wanasema kwamba "*Qullu haq walaukana muruwa*" Sema kweli ingawa inauma, hatuna kigugumizi, wala hatutaki kuwa na makengeza, katika kuona jitihada za serikali hii katika awamu hii ya Mhe. Dkt. Ali Muhammed Shein namna ilivyopita hatua katika taasisi zake mbali mbali, kama tutaanza kuchambua wizara moja baada ya nyengine, basi muda utakuwa mrefu na nafikiri itakuwa kazi yetu kupongeza tu, hakuna asiyeelewa.

Mhe. Naibu Spika, mtu ambaye ameondoka miaka miwili mitatu ambaye alikuwa akitumia uwanja wa Ndege wa Air Port namna ya kuona mabadiliko na hali halisi ilivyo. Hakuna ambaye atakuwa anabisha mtu ambaye alizoea kwenda maofisi ya serikali lakini leo hii atapoteza mafuta ya serikali kuona namna serikali ilivyojitahidi kutengeneza maofisi yalikuwa katika hali inayoridhisha. Karibuni tunategemea Mhe. Abubakar naye ataingia miongoni mwa majengo hayo ambayo yanaridhisha katika utendaji wa kazi.

Lakini naseme maeneo ni mengi, ukenda katika kiwanda cha upigaji chapa tulikwua tumeshazoea tulikuwa tunapiga kelele nyingi kiwanda watu wanaelea wanapokwenda maruhubi lakini serikali imepiga hatua na leo kiwanda tunakiona namna ambavyo serikali imepita hatua. Nasema haya ni maeneo mengi all most karibuni yote. Ukenda hospitali tulikuwa tuna mazoea hapa ya kuja kupiga kelele (ICU) haifai hakuridhishi lakini sasa hivi Alhamdulillah. Tulikuwa tunapiga kelele katika masuala mazima ya Wizara ya Elimu, vijana wanakaa chini, lakini namna serikali ilivyoandaa mazingira ya kutoza kodi ya Sh 1000/- sasa hivi *Alhamdulillah* hatu za madeski katika mashule yetu yanaonekana.

Mhe. Naibu Spika, *almost* niseme kwamba jitihada au mafanikio yaliyopatikana katika miaka minne na nusu haya kwa serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar ni mambo makubwa na yanapaswa yapigiwe mfano na tuendelee kumuunga mkono Rais wetu na Chama chake, ili mwaka 2015 upatikane ushindi wa kishindo. Nataka niingie ndani kidogo katika kitabu niwapongeze kitengo cha TASAF kwa namna walivyotuletea TASAF III kwa nia njema ya mpango wake wa kunusuru hali ya umasikini.

Ni jambo jema limeanza kuleta faraja kwetu na vijana wao wanakwenda vizuri, mimi basi niwaombe tu kwa dhati ile dhamira njema walioianza watendaji waendelee nayo kufanya kazi kwa umakini na kwa ujasiri bila ya upendeleo wa aina yoyote. Tuangalie watu wanaostahiki kupata haki zao za msingi katika TASAF III basi haki zitolewe kwa misingi iliyokuwa mizuri bila ya kujali ubaguzi wa aina yoyote iwe wa kivyama au jambo la kidini au jambo jengine. Kila mwananchi wa nchi hii ana haki ya kupata fursa iliyo sahihi.

Mhe. Naibu Spika, jengine ambalo ninalotaka kulizungumzia ni suala zima la jeshi la polisi. Kama ninavyosema kwamba tulipiga kelele sana lakini kuna mambo mengi wamejitahidi lakini pamoja na mambo mengine, lakini bado kuna baadhi ya mambo hayajafikia pale yanavyostahiki, sasa tuiyombe serikali yetu kulipitia Ofisi ya Makamu wa Pili kuona yale ambayo yana kasoro ndogo ndogo basi tujitahidi kuyafanyia kazi na kuyamaliza kwa haraka.

Tulipiga kelele juu ya jeshi la Polisi katika suala zima la kupata vitendea kazi tunashukuru, tumepata gari na *escort*, lakini tunashukuru jitihada zimeanza katika masuala ya kutumia redio call za kisasa lakini bado katika suala la jeshi la polisi kuna tatizo la makaazi ya askari wetu pale Ziwani, majengo hayapo katika hali ya kuridhisha.

Kwa kweli yanatarisha maisha ya usalama ya wale Polisi ambao wanakaa Ziwani. Basi niiyombe serikali jitihada walizozifanya katika kusaidia kupata yale maeneo mengine basi nalo hili waliangalie ili nalo liweze kupatiwa ufanisi wa haraka sana, *otherwise* vijana wetu watafanya kazi katika mazingira mafumu sana na mtu anapofanya kazi katika mazingira magumu kwa kweli hafanyi kazi kwa ufanisi kamili.

Mhe. Naibu Spika, eneo jengine ninalotaka nilizungumzie katika eneo la Ofisi ya Faragha, kama kitabu kinavyoelezea malengo ya kuimarisha Makazi ya Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais ni jambo jema. Hapa mimi nataka nimpongeze sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, nimpongeze kwa dhati ya nafsi yangu kwamba ni kiongozi ambaye anaonyesha zaidi kutokujali maslahi yake lakini zaidi anajali maslahi ya wananchi.

Mhe. Naibu Spika, bajeti iliyopita hapa nilipiga kelele sana juu ya makaazi ya nyumba ya Boznia na nikapewa sababu za msingi, nikapewa sababu tele, nikapewa maneno tele, kupitia Waziri wake wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwamba pale hapastahiki, sijui nyumba hairidhishi. Lakini nachukua fursa hii kumpongeza Makamu wa Pili kwa kutokujali kutumia pesa nyingi za walipa kodi na kuamua kwenda kuishi katika nyumba ile ya serikali. Hili ni jambo la kupongezwa, ni

jambo la kupigiwa mfano, hawa ndio viongozi wanaojali kutokutumia pesa za wananchi pasipokuwa na msingi uliokuwa mzuri.

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa najenga imani baada ya kutokezea kwa matatizo ya nyumba ambayo Mhe. Makamu wa Rais alikuwa anakaa tulitegemea labda Makamo wa Rais angesema basi nataka nikakae Serena kwa sababu nyumba ya Boznia tayari imeelezwa kwamba inakasoro mpaka ndani ya Baraza.

Kwa ushupavu wake, kwa imani yake kwa wananchi wake ameona bora asitumie pesa za serikali ovyo na aende akaishi katika nyumba ile. Nimpongeze sana lakini bado niombe kwamba kuna haja basi makaazi haya wizara kuweza kuyaboresha zaidi ili yaweza kuvutia na yalingane na hadhi ya viongozi wetu ambao tunawaweka katika nyumba hizi.

Mhe. Naibu Spika, jengine ambalo nataka nilizungumze hichi kitengo cha kukabiliana na maafa. Mheshimiwa Wajumbe wengi hawakuingia katika kitabu cha makadiri ya mapato na kwa sababu ya kutokuingia ni namna ya mfumo ulivyokuja. Aidha mfumo huu unaleta tabu wakati mwengine kuweza kuchangia kwa namna ulivyo kwa sababu umefunga kila kitu lakini aidha wameona kwamba hakuna haja ya kuingia zaidi kwa sababu zaidi kimependekeza kuingiziwa fedha, kufanya matumizi, baadaye kuja kuhoji mwakani namna gani ya matumizi tulivyoyatumia.

Mimi Mhe. Naibu Spika, nataka niingie katika eneo moja tu ambalo tutakapokuja kufanya majumuisho basi nije nisaidiwe katika kitabu hichi  katika ukurasa wa 164, katika utaratibu wa shughuli za serikali SO1 kukabiliana na maafa. Mhe. Naibu Spika, utaratibu huu wa shughuli za kukabiliana na maafa pametengewa shilingi 355,775,000. Hapa kidogo Mhe. Naibu Spika, mimi nilikuwa napata wakati mgumu kwa kuangalia kima kilichotengwa hapa katika hii taasisi.

Mheshimiwa lazima tukiri katika miaka ya karibuni nchi yetu Mwenyezi Mungu amekuwa akitupa majanga mbali mbali ya maafa kwa miaka mitatu mfululizo. Yanapotokezea maafa taasisi hii inashindwa kufanya kazi zake kwa ufanisi, kwa sababu ama kukosa uwezo wa fedha ama kukosa uwezo wa vitendea kazi vilivyokuwa bora katika kuokoa wananchi wa nchi hii pale wanapopata majanga ya maafa.

Mhe. Naibu Spika, tumeshuhudia katika majanga ya meli lakini tumeshuhudia pia katika majanga ya mvua ambayo imejitokeza hivi karibuni. Hatimae inafikia pahala inakuwa tunatumia muda mrefu sana au tunatumia nguvu kubwa ya kuomba misaada kwa wafanyabiashara ama wafadhili wengine katika kukabiliana au kuwaondoshea matatizo wananchi hao.

Hofu yangu Mheshimiwa katika kitengo hichi nina wasi wasi kwa hivyo nije nielezwe au nichambuliwe, kwa sababu hapa kiki kitengo kitakuwa kina mambo mengi, kuna masuala mazima ya mishahara na mambo mengine, yaani kuna mambo ya utawala mengi. Sasa hiki kilichotengwa katika suala zima la ununuzi wa vifaa, katika suala zima la kuimarisha zana ambazo tunaweza tukakabidhiana maafa yatakayotokea zinatosheleza na kama hazitoshelezi, nini wizara imejipanga katika kuona namna mmoja au namna nyengine tunaweza kutafuta vitu ambavyo pale ambapo linatakapokuja kutokea janga basi inaweza serikali hii ikamudu kuweza kulitatua lile janga kwa haraka sana.

Mhe. Naibu Spika, kitengo hichi kinahitaji zana nyingi sana, tulizungumza hapa wakati mwengine tunapata majanga ya baharini. Janga la baharini kuhusika kwenda kuokoa watu kwa urahisi ni vyema tukapata herkopta ili kuwafikia watu kwa haraka na kuona namna gani tunaweza kuwaokoa. Lakini tukasema herkopta hatuna lakini basi hata kuwa na boti za *speed* kasi kuweza kukimbilia kwa wale watu watu ambao wanaweza wakapata maafa yale je, wizara imejipanga vipi katiak hili. Ndio maana nikasema kwamba kila nikiangalia kwenye kitabu hichi pesa ambazo zimepangwa kwa namna ambavyo idara hii katika miaka mitatu maafa yanayotupata bado nahisi ni ndogo na halimtoshelezi kuweza kukisaidia kitengo hichi ili pale yanapoweza kutokezea matatizo kuweza kuwasaidia wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, namalizia dakika zangu katika hii kurasa ndogo kabisa katika michango ambayo wajumbe wote wamejaribu kuielekeza katika suala zima la Tume ya Uchaguzi. Mheshimiwa Tume ya Uchaguzi ni chombo ambacho kimeundwa kwa mujibu wa sheria na sisi ndio watunga sheria. Mimi ningeomba sana Mhe. Naibu Spika, tuwache kupiga kelele, tuwache kukinyooshea kidogo hichi chombo, chombo hiki tukiache kifanye kazi zake kwa mujibu wa taratibu za kisheria. Pale ambapo kitafanya makosa basi tunahaki ya kukisimamia na kukielelekeza namna gani ya kuweza kufanya.

Mhe. Naibu Spika, lugha ambazo jana zilitaka kutumika na nakushukuru sana na nikupongeze wewe Mhe. Naibu Spika, kwa kuzuia lugha zile zisiendelee kutumika ndani ya chombo hiki, lugha ambazo hazina ushahidi, lugha ambazo hazina ukweli. Sasa hivi Mhe. Naibu Spika, tunapata tabu mpaka sisi wana siasa pale ambapo tunapata misiba mara nyingi huwa tunajaribu kwenda kuwaomba wenzetu wa taasisi za kiserikali tupatiwe magari kwenda mazikoni, lakini sasa hivi gari la jeshi likionekana limepakiwa watu wanakwenda mazikoni basi mara utaona kwenye mitandao, gari la jeshi limeonekana linakwenda Chwaka limepakiwa watu wanakwenda kupiga kura.

Sasa watu wamekuwa wanazungumza maneno ya ovyo kabisa, watu hawana *evidence* ya aina yoyote katika vyombo hivi. Sasa tunasema maneno haya Mhe. Naibu Spika, yanafikia pahala baada ya kujenga nchi tunaweza tukachochea.

Mwanasiasa akisema wafuasi wanakuwa wanafatia na kuunga mkono hoja za wanasiasa. Sasa hiki chombo Mhe. Naibu Spika, sote tunaelewa kwamba suala zima la Tume ya Uchaguzi mamlaka tuliyowapa na nini cha kufanya wamepanga utaratibu uliokuwa wazi nchi hii inaongozwa kwa demokrasia, nchi hii inafuata utawala bora, tuwachilie wenye chombo tuliyowapa mamlaka wafanye kazi zao. Kazi za Tume ya Uchaguzi Mhe. Naibu Spika, tusizifanye sisi wanasiasa baada ya kuwaachia wao ambao tumewapa na sisi tunatakiwa tuwasimamie kwa yale ambayo tumewatuma na kuwaelekeza.

Mhe. Naibu Spika, hilo ndio lililokuwa la kumalizia kwangu mimi nina imani sisi sote tuna imani na Tume ya Uchaguzi na Tume ya Uchaguzi tunajua inafanya kazi zake itaandikisha watu na muda utakapofika walioandikishwa watawekwa hadharani ili kuwajua na kama kuna tatizo basi wananchi au mwenye kujenga kwa yule mtu atakwenda kutoa ushahidi wake Tume ya Uchaguzi.

Mhe. baada ya hayo ninakushukuru sana, naunga mkono hoja hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka wa Fedha wa Bajeti inayotumia programu kwa mwaka 2015 hadi 18. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwahani ninaunga mkono asilimia 100 ninakushukuru sana. Ahsante sana.

**Mhe. Mohammed Mbwana Hamad:** Mhe. Naibu Spika, awali ya yote na mimi ninachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia kuwepo mchana huu katika Baraza lako ili kutekeleza majukumu yetu ya kila siku. Mhe. Naibu Spika, nikupongeze wewe kunipa fursa hii ya angalau na mimi nikachangia machache katika hotuba iliyopo mbele yetu.

Mhe. Naibu Spika, niendelee kutoa pongezi zangu kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa jinsi alivyoiwasilisha hotuba hii kwa umakini wa hali ya juu. Mheshimiwa bila kupoteza muda nianze mchango wangu katika ukurasa wa 10 juu ya suala la mapambano dhidi ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia.

Mhe. Naibu Spika, suala la udhalilishaji na ukatili kwa kweli ni suala gumu sana katika visiwa vyetu hivi vya Unguja na Pemba. Kwa hivyo mimi niiombe Serikali ijipange kwa nguvu zake zote takriban katika kupambana na janga hili ambalo ni kubwa. Janga la udhalilishaji na ukatili wa kijinsia linaweza likatupotezea nguvu kazi ya baadae. Kwa sababu vijana wadogo wadogo wengi wanafanyiwa ukatili lakini pia wanafanyiwa udhalilishaji, vijana hawa ndio tegemeo la taifa keshokutwa.

Mhe. Naibu Spika, niiombe Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais suala hili kwa hali yoyote kama kuna sheria ambazo zina kasoro zirekebishwe ili

kuwatia hatiani kwa urahisi mno wanaofanya matendo haya ya udhalilishaji wa kijinsia katika visiwa vyetu.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu niende ukurasa wa 11 ambao unazungumzia mapambano dhidi ya rushwa. Mhe. Naibu Spika, naomba ninukuu:

"Mhe. Spika rushwa imekuwa donda ndugu na ni adui mkubwa kwa maendeleo ya nchi yetu na ustawi wa jamii mpaka mwisho wa *paragraph*".

Mhe. Naibu Spika, neno donda ndugu ni neno zito sana ni lile donda ambalo halipoi kwa sasa tunaita *cancer* lakini Mhe. Naibu Spika, ikiwa amekuwana *cancer* katika mkono au mguu, mguu unakatwa. Kwa wanaokula rushwa hukata mguu wao au mkono wao ni kuwaondoa katika sehemu zile ambazo wanazifanyia kazi ikiwa kuna maafisa ambao wanatoa huduma lakini hawakamilishi huduma yao mpaka wapewe chochote, ukipatikana ushahidi tosha basi dawa ya kulikata donda ndugu hili ni kumuondoa katika nafasi yake.

Jengine, Mheshimiwa niiombe Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais itoe taaluma ya kutosha kwa wananchi wetu juu ya kutoa na kupokea rushwa, rushwa ni adui wa haki, rushwa inaweza kulipeleka taifa letu katika hali ya umaskini. Mhe. Naibu Spika, haki itendeke bila ya rushwa kwa sababu rushwa inaweza ikawaangamiza wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu nataka niende moja kwa moja mpaka ukurasa wa 33. Ukurasa wa 33 kwa 34 nakwenda katika bajeti kwa mwaka wa fedha 2015/2016 kwamba Serikali inaendelea kufanya mageuzi ya bajeti ikiwa ni sehemu ya mageuzi ya utawala na udhibiti wa fedha za umma.

Niende katika ukurasa wa 34 programu ya 2, uratibu wa shughuli za Serikali. Mhe. Naibu Spika, niende katika programu ndogo ya 1, uratibu wa shughuli za kukabiliana na maafa. Mhe. Naibu Spika, hii imechangiwa na wajumbe takriban wote waliochangia lakini kwa sababu ya umuhimu wake basi kila mjumbe anaweza kuichangia kutokana na umuhimu wa kulizungumzia suala hili.

Mhe. Naibu Spika, kwanza mimi niwape pole wale wote wananchi wetu ambao wamefikwa na maafa katika kipindi hiki. Ushauri wangu kwa Serikali hivi sasa tunaona kwamba watu wengi wanajenga majengo yao bila ya kuzingatia utaratibu mzima wa mipango miji. Kwa hivyo niiombe Serikali katika kukata viwanja basi ikate viwanja kwa umakini mkubwa kwa sababu miongoni mwa maafa yanayotokea katika visiwa vyetu hivi ni maafa ambayo tunayakaribisha wenyewe.
Kuna baadhi ya maeneo yalikuwa yanatiririsha maji kwenda katika sehemu nyengine, lakini kwa sababu ya ujengaji wa kiholela sehemu zile maji yanatuama

na kufanya mto na mvua zinapokuwa kubwa maji yanaingia katika majumba ya watu maskini.

Mhe. Naibu Spika, ninaiomba sana Serikali katika hili iangalie vizuri namna gani ya ujenzi unavyojengwa katika miji yetu ili kupunguza maafa yanayotokana na mvua. Tunaposema kwamba Zanzibar imeingia mafuriko mimi ninamuomba Mwenyezi Mungu ajaalie yasiingie mafuriko katika nchi yetu. Mafuriko ni mambo makubwa sana na ni mabaya sana yanaweza yakaigharikisha nchi muda mfupi sana. Yanayotokea kwetu si mafuriko bali ni maji ambayo yanazuilika kwenda katika sehemu zake za kawaida yanazuilika kwa sababu ya ujenzi holela.

Ninavyoamini mimi mariko Mhe. Naibu Spika, ni yale maji ambayo Mwenyezi Mungu anayatoa chini ya ardhi kwa njia ya chemchem lakini maji yanayovamia katika nchi yetu ni maji ya mvua ambayo yanakosa pahali pa kwenda. Kwa hivyo ninamuomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais pamoja na taasisi zinazohusika suala zima la majengo liangaliwe kwa umakini mkubwa, vyenginevyo nchi yetu inaweza ikaelekezwa na mabalaa ya namna hii mara kwa mara.

Mhe. Naibu Spika, suala la ujenzi ni suala muhimu na wala lisibezwe nchi yetu ni visiwa, eneo letu ni dogo bila ya kuzingatia majengo basi kila unapofika msimu wa mvua hali hii inaweza ikajitokeza siku hadi siku.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu niende katika ukurasa wa 36 katika programu ya 4 Mipango na Utawala. Niende katika programu ndogo ya 1 naomba ninukuu:

"Mhe. Naibu Spika, programu hii ndogo ina lengo la kuimarisha na kusimamia utendaji kazi katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, matokeo yanayotarajiwa ni matumizi bora ya raslimali, wafanyakazi wenye ujuzi na uzoefu na ufanisi katika utendaji kazi. Huduma zinazotolewa ni kutoa huduma za utumishi na uendeshaji ikiwemo stahiki mbali mbali na kuwapatia mafunzo na vitendea kazi wafanyakazi".

Mhe. Naibu Spika, hili lengo ni zuri sana lakini tulipotaja stahiki za wafanyakazi au stahiki mbali mbali za wafanyakazi naomba hili lipewe nafasi kubwa kwa sababu kuna wafanyakazi wengi stahiki zao zinachelewa kufika. Kwa mfano kuna wafanyakazi unafika muda wao wa likizo wanachelewa kupewa likizo lakini kuna wafanyakazi wanachelewa kupewa overtime, lakini kuna wafanyakazi ambao wanamaliza masomo wanatarajiwa kurekebishiwa malipo yao yanachelewa kurekebishwa. Kwa hivyo niiombe Ofisi kwa jitihada kubwa ihakikishe kwamba inawaimarisha wafanyakazi wake kwa ufanisi zaidi ili waweze kufanya kazi kwa moyo mmoja katika kulijenga taifa.

Mhe. Naibu Spika, niende katika ukurasa wa 38 Baraza la Wawakilishi. Baraza la Wawakilishi ni chombo miongoni mwa vyombo vikubwa ambavyo vipo katika nchi yetu ya Zanzibar. Baraza la Wawakilishi limekabiliwa na changamoto kadhaa, changamoto ambayo nataka niizungumze mimi ni udhaifu wa jengo ambalo liko pale kisiwani Pemba.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu ambayo yalijibiwa na Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais asubuhi kuhusiana na uimarishaji wa ujenzi wa ofisi ile lakini na mimi katika mchango wangu ni lazima nioneshe na mimi hisia zangu za kwamba jengo lile kuimarisha kwake kutakuwa na umuhimu wa hali ya juu kabisa.

Mhe. Naibu Spika, niiombe Ofisi ya Makamu wa Pili suala zima la kulishughulikia jengo la Ofisi ya Baraza la Wawakilishi Pemba ni muhimu na ni muhimu sana. Kwani kufanyika kwa vikao katika Baraza la Wawakilishi pale Pemba kutaleta sura nzuri ya wananchi wetu wa pale Kisiwani Pemba angalau kusikia moja kwa moja michango ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi bila kusikia katika vyombo vya habari.

Mhe. Naibu Spika, vile vile kuwepo kwa Baraza la Wawakilishi pale Pemba kuendelea na vikao kutaleta faida kubwa kwa wafanyabiashara wetu mbali mbali. Kwa hivyo ule mzunguko wa fedha utakuwa unazunguka katika kisiwa kile cha Pemba katika kipindi chote ambacho Baraza la Wawakilishi nalo litakuwepo pale.

Mhe. Naibu Spika, baada ya mchango wangu huo kimuhtasari niende katika hali ya kisiasa Zanzibar. Hili limezungumzwa na waheshimiwa wengi na ni vyema kwamba kila Mheshimiwa kuligusa kutokana na umuhimu wake.

Mhe. Naibu Spika, nataka ninukuu katika kitabu cha hotuba ya Makamu wa Pili wa Rais ya Bajeti ya mwaka 2011/2012 alivyoelezea kuhusu habari ya hali ya kisiasa. Kwa sasa nchi yetu iko katika utulivu mkubwa na umoja ambao chanzo chake kinatokana na maridhiano yaliyofikiwa na vyama viwili vya CCM na CUF, hali hiyo imejenga utamaduni wa kuvumiliana kisiasa. Hatua hii pia imejenga sura ya Zanzibar mpya yenye umoja, maendeleo na matumaini mapya.

Mhe. Naibu Spika, na katika kitabu cha mwaka huu ambacho tunakiendeleza hivi sasa katika kukitolea maelezo, maelezo yake yanafanana na haya ya bajeti iliyopita ya mwaka 2011 na bajeti ya 2012/13 pia maelezo ya hali ya siasa yanaonesha kwamba ni matumaini yetu mazuri kwamba hali ya kisiasa ni nzuri. Wito wangu kwa vyombo vinavyohusika na kusimamia chaguzi, mikutano na vyenginevyo viwe vinatenda haki ili wananchi wetu wapate utulivu wa kutosha.

Mhe. Naibu Spika, bila ya vyombo hivi kuvitumia kwa uadilifu nchi yetu ya Zanzibar ni ndogo tutakuja kuiweka katika mazingira magumu, mazingira ambayo tutakuja yajutia baadae. Kila kiongozi ni mchunga na kila mchunga ataulizwa namna gani alivyowachunga anaowaongoza. Tuwachungeni tunaowaongoza kwa haki, uadilifu na amani.

Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunivumia dakika mbili tatu hizi na mimi niseme kwamba niunge mkono hoja.

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa tumebaki na wachangiaji wanane tumebaki na saa moja. Bahati mbaya wawili hawapo, kwa hivyo sita waliokuwepo kila mmoja dakika 10. Ninawataja kwa jumla mjijue. Ataanza Mhe. Wanu, afuatie Mhe. Mohammed Haji Khalid, Mhe.Mwanajuma Faki Mdachi, Mhe. Bikame, Mhe. Viwe na mwisho Mhe. Jazira. Kwa hivyo tunaanza Mhe. Wanu, tusirejee twende kwenye *point* moja kwa moja.

**Mhe. Wanu Hafidh Ameir:** Mhe. Naibu Spika, kabla ya yote na mimi niungane na wenzangu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutukutanisha hapa leo ili kuendelea na majukumu yetu ya kila siku. Lakini pili Mhe. Naibu Spika, nikushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii na nitajaribu kadri iwezekanavyo kufata maelekezo yako ili kuona kwmaba na wenzangu nao wanapata muda wa kuchangia.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuanzia nami niungane na Mwenyekiti wangu wa Uwawazana wajumbe wengine kwa kumpongeza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa uwasilishaji wake mzuri na wa ufasaha, lakini pia nimpongeze Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais baba yangu Mohammed Aboud kwa kazi nzuri anayoifanya ya kumsaidia Mhe. Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Naibu Spika, hongera za pekee ziende kwa watendaji ambao wapo hapo juu ambao wao ndio watendaji wakuu wa Wizara hizi na bila ya wao Mhe. Naibu Spika, hii leo Mhe. Makamu wa Pili wa Rais asingeweza kuwasilisha hotuba yake pale mbele.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuanzia naomba nianze katika hali ya kisiasa na hapa naomba niungane na kauli ya Makamu wa Pili wa Rais kwanza kwa kuwapongeza viongozi wote wale ambao wamechaguliwa katika chaguzi za Chama cha CUF lakini sio pongezi kwa kuchaguana tu, lakini kuwapongeza kwa kuchaguana kwa utulivu na amani bila kunyukuana.

Mhe. Naibu Spika, ni imani yetu kwamba utulivu ambao wamechaguana katika chama chao tutaungana mwezi wa Oktoba, kwa utulivu ule ule na amani ile ya kuchagua viongozi wetu wa kitaifa. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Rais wakati

anakabidhiwa nchi hii alikabidhiwa ikiwa katika amani na utulivu na nimpongeze sana kwa kazi nzuri ambayo ameifanya mpaka hii leo ameweza ku-*maintain* amani na utulivu ambayo alikabidhiwa wakati anakabidhiwa nchi hii.

Mhe. Naibu Spika, ushauri wangu wa bure kwa Rais sitaki kuchukua kazi za watu za kushauri Rais lakini kazi zetu Baraza kushauri na kuielekeza Serikali. Ushauri wangu Mhe. Naibu Spika, Mhe. Rais afanye analoweza kama mkuu wa nchi hii kuona kwamba amani na utulivu wa nchi hii inaendelea kama ilivyo. Asikubali *in anyhow* kuona kwamba amani na utulivu wa ndhi hii inavunjwa katika mikono yake. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, niseme hayo na nimtakie kila la kheri asiwape nafasi wale wote wenye nia ya kuvuruga amani na utulivu wa nchi hii.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa muda ni mdogo sana ambao tumepewa naomba niongee mambo ya jumla na kwa kuanzia nitaanza kuingia katika masuala ya mtambuka.

Mhe. Naibu Spika, wajumbe hapa wamezungumzia mambo mbali mbali kuhusiana na masuala ya mtambuka. Kuna mambo ya mazingira, mambo ya udhalilishaji na ukatili, kuna mambo ya rushwa na mambo mengine mengi ambayo yamezungumzwa.

Mhe. Naibu Spika, mimi sitaki kukubaliana na hotuba ya Makamo kwamba mambo haya sasa yamekuwa yameshamiri, lakini pia mambo haya yamekuwa donda ndugu. Mhe. Mohammed Mbwana ameelezea vizuri jinsi ya donda ndugu linavyokuwa. Sasa na mimi sitaki kuamini kwamba mambo haya yamekuwa donda ndugu kwa sababu tunaona serikali inachukua jitihada mbali mbali ya kuyatatua mambo haya, lakini bado kuna wachache ambao kwa makusudi wanaendelea kufanya mambo haya, na wanaendelea kwa nini? Ni kwa sababu sheria zipo watu hawataki kutii sheria, lakini watu hawatii sheria kwa sababu gani? Kwa sababu usimamizi ni mdogo, usimamizi wa sheria ni mdogo Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, mambo ambayo yametajwa hapa maafa, maafa tatizo watu hawafati sheria wanajenga mabondeni na wanatupa taka mitaroni. Maafa sheria za barabarani hazifuatwi, Kisiwapanza kinazama, lakini kwa sababu uharibifu wa mazingira watu wanakata miti ovyo sheria zipo hawafati, lakini pia udhalilishaji hapa hata sheria za Mungu watu wameziweka pembeni na mambo mengine rushwa.

Sheria za uadilifu na uwajibikaji zipo lakini zinavunjwa na zinaendelea kuvunjwa kwa sababu gani? Kwa sababu watu wanavunja sheria usimamizi hamna kila mmoja anafanya anavyotaka, wanaofanya hawachukuliwi hatua. Kwa hiyo, Mhe.

Naibu Spika mimi niseme kwamba mambo haya sio sugu, serikali ikijikita kidhati hasa kuyafanyia kazi yanaweza kufanyiwa kazi na mambo haya yakaisha.

Mhe. Naibu Spika, ni jambo la kawaida hata mtu anayechunga mifugo akiona inaenda *anyhow* anapitisha bakora kidogo kukaa sawa, sisemi watu wapigwe bakora lakini serikali lazima ichukue hatua kuona kwamba inarudi katika mstari kusimamia sheria, sheria zipo hapa kila siku tunatunga, kila kukicha asubuhi tunatunga sheria na ni nzuri tu kabisa.

Tatizo ni kwamba usimamizi unakuwa mdogo watu wameshakuwa *rackless* mtu hamjali anafanya anavyotaka anaona hafanywi kitu na ndio maana mambo haya yanaendelea. Kwa hiyo, Mhe. Naibu Spika, niseme tu kwamba ushauri wa bure kwa serikali ni kwamba usimamizi wa sheria, sheria zisimamiwe ipasavyo ili kuona kwamba mambo yanaenda kama yalivyopangwa.

Mhe. Naibu Spika, naomba nikimaliza hapo katika masuala ya mtambuka niingie katika Ofisi ya Faragha ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais. Katika Ofisi ya Faragha moja ya majukumu yao ni kuratibu ziara za ndani na nje za Mhe. Makamo wa Pili wa Rais. Sasa nilikuwa nasoma katika utekelezaji hapa ofisi imeratibu ahadi 23 zilizotolewa na Mhe. Makamo wa Pili wa Rais katika mambo mbali mbali kati ya hizo ahadi tisa tayari zimetekelezwa.

Mhe. Naibu Spika, ahadi 23 na ahadi 9 tu ambazo zimetekelezwa ni kidogo sana, niiombe sana serikali zile taasisi ambazo zinahusika kwa sababu maelezo yanasema kwamba ahadi zilizokuwa hazijatekelezwa zinaendelea kufanyiwa kazi na taasisi mbali mbali zinahusika. Kwa hiyo, tuwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe wamesema hapa kwamba hiki kipindi cha lala salama. Sasa lala salama hatutaki Makamo wetu wa Pili wa Rais aje kuhukumiwa *just because* kuna ahadi ambazo hazikutimizwa.

Kwa hiyo, niombe sana zile taasisi ambazo zinatakiwa kutimiza ahadi hizi zitimize ili kuona kwamba zile ahadi ambazo Mhe. Makamo wa Pili wa Rais ameahidi zimechukuliwa hatua. Sote tunajua kwamba kuna watu huko wananyemelea ahadi zilizokuwa hazijatimizwa tu kwa hiyo msipotimiza hii kama taasisi mjue kwamba kuna watu watazitimiza, na wakizitimiza mjue imekula kwenu.

Mhe. Naibu Spika, nikimaliza na Ofisi ya Faragha kuna mapato…

**Mhe. Naibu Spika:** La mwisho hilo.
**Mhe. Wanu Hafidh Ameir:** Ndio Mhe. Naibu Spika, la mwisho.

Mhe. Naibu Spika, kuna mapato yale mapato ambayo yanatokana na malipo ya watafiti wanaofanya tafiti katika Taasisi ya Nyaraka.

Mhe. Naibu Spika, kwa maelezo ya Taasisi ya Idara ya Nyaraka kwamba mapato haya kawaida yanalipwa katika Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, na nikiangalia kitabu sijaangalia sana Mhe. Naibu Spika, lakini niliangalia kwa haraka haraka sikuona sehemu yoyote ambapo mapato haya yameainishwa na bajeti za nyuma nimekuwa nikisema sana kwa sababu nikisema katika wizara ambayo Idara ya Nyaraka ipo naambiwa kwamba mapato haya yapo kwenye Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais.

Hebu naomba waziri akija aje atuelezee hapa haya mapato yanaingia wapi, kwa sababu katika bajeti za nyuma pia mapato haya ilikuwa hayaoneshi. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Mhe. Waziri akija aje atoe maelezo kuhusu hayo.

Mhe. Naibu Spika, naheshimu sana muda wako na baada ya kusema hayo naunga mkono hotuba hii ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, asilimia mia.

**Mhe. Mohammed Haji Khalid:** Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi kupata muda mfupi kuchangia hotuba hii ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais.

Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa tena nafasi hii, Mhe. Naibu Spika, nisema kwamba Mhe. Makamo wa Pili wa Rais ameona mara hii huu ni ukuni wa mvua hatumwi mtoto, ndio maana akaamua kuja kusoma bajeti yake yeye mwenyewe badala ya kusomewa na waziri wake, nimpongeze kwa hilo.

Mhe. Naibu Spika, nianze mimi katika huduma za kijamii na nianzie kwenye elimu.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na vyote serikali inavyoeleza kuhusu elimu kwa kuondoa ada mbali mbali na mambo mbali mbali lakini kwa mtazamo wangu mfumo wa elimu uliopo au sera ya elimu iliyopo badala ya kukuza elimu kwa uono wangu mimi tunaidumaza elimu. Nitoe mfano Mhe. Naibu Spika, mwaka huu watoto wa madarasa ya msingi, darasa la saba na la sita wote wanafanya mitihani ya kuingia darasa la tisa (*form one*) sijui kuna madarasa mangapi ya sita katika skuli, kuna madarasa mangapi ya saba katika skuli ambao kwa ujumla wote hawa wataingia *form one*.

Kwa hiyo, kutakuwa na mrundikano madarasa ni machache pengine watakwenda skuli baada ya mikondo miwili iwe ni mitatu. Kwa hivyo, badala ya kupatikana elimu kamili itakuwa masomo yanayopatikana ni machache mno. Kwa hivyo, mfumo huu badala kuona kuwa tunakuza elimu lakini ilikuwa tunaididimiza elimu

na analiyefikiria sera hii alifikiria kuwa Zanzibar ikose elimu bora. Kwa hivyo, mimi mfumo huu wa elimu kwa kweli siungi mkono hata kidogo, kwa sababu baada kukuza unadidimiza.

Mhe. Naibu Spika, mfumo huu walimu tulionao pamoja na kuwa serikali inasema ina walimu wa kutosha lakini kuna maskuli kadhaa ambayo watu wanagawana masomo na mengine yanabakia hayana mwenyewe. Kwa hivyo, serikali ichunguze mle mwahala ambapo walimu hawatoshi ama waajiri au watoe uhamisho pahala ambapo walimu wamerundikana.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu afya ni kweli serikali imejitahidi kueneza vituo vya afya kila pahala, lakini je huduma zipo? Wingi wa vituo sio muhimu, muhimu ni kutokana na huduma kwa watu wanaokwenda katika vituo hivyo. Kwenda hospitali *nurse* au daktari akakuandikia halafu akakwambia nenda kanunue bado hapo huduma ya serikali haijakuwepo, ni sawa sawa ni kuwa daktari anakupiga bao ukatafute mganga akugange. Kwa hivyo, kwa kuwa huduma ni chache bado mfumo wetu wa matibabu ni mbovu na serikali ina haja ya kuutazama upya.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu udhalilishaji hili ni jambo baya na serikali ina kila njia ya kupiga vita kwa nguvu zake zote ili kuwaokoa watoto wetu pamoja na wanawake katika janga hili baya.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu rushwa ushahidi wa kupatikana rushwa kwa kweli ni mgumu mno, na Mhe. Naibu Spika watu rushwa si ya kulipa fedha tu inayotumika lakini wengine wanatumia hata kuwadhalilisha kijinsia watu wanaomba nafasi au watu wanaomba haja zao muhimu serikalini wakataka rushwa, wengine wanataka rushwa ya pesa, wengine wanataka rushwa ya aina nyengine.

Masuala haya lakini yote kupatikana ukweli wake ni mgumu, kwa sababu rushwa imekaa kama zinaa na uislamu. Kuthibitisha zinaa katika uislamu ni kazi kubwa kwa sababu kuna ushahidi unaotakikana upatikane na rushwa hivyo hivyo mtoaji na mpokeaji kuwathibitisha ni jambo gumu sana, lakini jambo ambalo lipo ni kwamba serikali isimamie ili kuondoa rushwa isiendelee au isiwepo kabisa.

Mhe. Naibu Spika, nije kidogo katika jengo hili la Baraza la Wawakilishi na niligusie hili jengo wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, jengo hili pamoja linavyoonekana halina kiwango, ni jengo bovu sana linashambuliwa vikali sana na mchwa na mna sehemu linavuja. Kwa hivyo, serikali ichukue juhudi za makusudi ya kulishughulikia jengo hili ili liweze kutoa huduma zake kikamilifu na watu waweze kukaa humu ndani bila ya hofu yoyote.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu ripoti mbali mbali za Kamati Teule zinazoundwa nasikitika kuwa hakuna hatua madhubuti zilizochukuliwa kuhusu ripoti hizi za Kamati Teule zinapowasilishwa. Serikali bado imekaa kimya bila ya kutoa majibu ya pale pahala ambapo wameonekana wahalifu wapo. Ripoti ya mwisho Mhe. Naibu Spika, ni ile iliyochunguza upotevu wa nyaraka.

Mhe. Naibu Spika, nyaraka zilizopotea nyengine ni za taasisi na majengo muhimu sana ya serikali. Kwa hivyo, wito wangu ikiwezekana serikali ifanye juu chini nyaraka hizi zirudi ili majengo yale na taasisi zile za serikali ziwe zina ushahidi katika nchi, na wale ambao watabainika kwamba wana kosa wachukuliwe hatua za kisheria.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie mchango wangu mfupi katika hali ya kisiasa. Nishukuru kwamba katika miaka hii minne na nusu iliyomalizika hali ya kisiasa haikukorogeka sana katika visiwa vyetu tumekwenda vizuri. Kwa hivyo, hili ni jambo zuri na ni jambo la kupigia mfano. Kwa hiyo, ningeomba kwamba utulivu huu, amani hii iendelee hasa katika kipindi kinachofuata cha kukabiliana katika uchaguzi ambapo ndio mara nyingi hali ya hewa inapochafuka.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Makamo wa Pili alipowasilisha ripoti yake alitaja juu ya Katiba inayopendekezwa kwamba ikifika wakati wake watu waipigie kura. Mimi nasema nawaomba Wazanzibari kwa nguvu zao zote Katiba hii wasiithibitishe, wasiipigie kura ya ndio na waipigie kura ya hapana. Ahsante sana.

**Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi:** Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi hii kuweza kuchangia *time* hizi za adhuhuri hotuba hii ya makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mhe. Naibu Spika, niseme kama walivyotangulia wenzangu na mimi sina budi kumpongeza Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwa hotuba yake hii ya mwaka 2015/2016 jinsi alivyoiwasilisha hapa Barazani. Lakini pia nimwambie Mhe. Makamo wa Pili wa Rais hotuba hii ya fedha ayaangalie maeneo ambayo tayari yameachwa hayajafanyiwa kazi ili ayape kipaumbele kwa bajeti inayokuja ili kutengeneza maeneo yale na kuwapa wananchi kuwa katika imani bora.

Mhe. Naibu Spika, pia nimpongeze Mhe. Makamo wa Pili kwa ujasiri wake wa kuwasilisha hotuba hii bila ya wasi wasi lakini na mimi nimuombe kwamba katika hotuba yake hii nimuombe kwa dhati na kwa imani yake aiangalie barabara ya Kangani kuelekea Kuukuu, kibarabara hiki ambacho tangu 2005 ambacho kinatiliwa bajeti, 2010 kimeingiziwa bajeti lakini kibarabara hiki bado hakijatengenezwa na hivi sasa ingawaje nasikia imepelekwa katika kilimo.

Hata hivyo, naomba Mhe. Makamo wa Pili unitilie msukumo zaidi kwa sababu kijiji kile ni hali mbaya na sasa hivi wananchi wanashindwa kutoka kwa mvua kubwa ambayo imenyesha kwa kipindi hiki.

Mhe. Naibu Spika, nikiingia katika kuchangia ukurasa wa 7 niende katika huduma za kijamii, lakini hasa zaidi nitaingia katika elimu. Mhe. Naibu Spika, kidogo niseme hivi karibuni serikali imetangaza rasmi kufuta kwa malipo ya elimu kwa wanafunzi. Hili niipongeze serikali kutokana na suala hili kama walivyosema wenzangu. Lakini Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba kuona suala la walimu wastaafu linacheleweshwa kulipwa hili naomba Mhe. Makamo wa Pili aliangalie sana pamoja na kutoa msamaha wa kulipa malipo kwa wanafunzi lakini aliangalie suala la wastaafu ambao wanastaafu kupewa mafao yao kamili kabla hawajakuwa na tabu katika vijiji, kwa sababu hili wanalitegemea pale wanapofika ndio kianzio chao cha maisha na watoto wao, aliangalie sana suala hili.

Mhe. Naibu Spika, lakini jambo ambalo linawasikitisha sana walimu hao hutegemea wapate mafao hayo, ili waanzie maisha na watoto wao. Kwa hiyo, naiomba serikali iliangalie suala hili kwa makini.

Mhe. Naibu Spika, vile vile kufutwa kwa michango kwa wanafunzi shuleni za msingi na kuondoa malipo ya mitihani. Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba bado suala hili halijakuwa la kuboresha kiwango cha elimu, lakini isipokuwa Mhe. Naibu Spika, elimu inaboreshwa kutokana na umakini wa walimu na ufahamu wa wanafunzi. Kwa hiyo, naiomba serikali au niseme je serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha kiwango cha elimu kinaboreka hapa Zanzibar? Na pia serikali imejipanga vipi kuimarisha kiwango cha elimu ya sayansi maskulini.

Mhe. Naibu Spika, nije katika sekta ya afya ukurasa wa 8 inasema kwamba kwa upande wa sekta ya afya serikali inaendelea kuimarisha huduma za kinga na tiba katika mahospitali. Niseme kwanza nimpongeze Mheshimiwa kwa hotuba yake hii na kipande hiki ambacho kinasema hivyo. Lakini pamoja na hayo serikali vipi inatoa elimu kwa afya kuhusu maradhi ya mripuko hasa wakati huu wa mvua za Masika.

Vile vile kwani tumeshuhudia wakati wa mvua hizi za Masika zinaponyesha huwa nyumba nyingi zinafurika na vyoo hufurika ndio chanzo kikubwa cha maradhi. Je, serikali imejipanga vipi kuona mambo haya hayatokei ili kunusuru wananchi na miripuko ya maradhi ya aina kama hii. Vile vile niseme katika Hospitali ya Abdalla Mzee na katika suala langu hapa nililochangia kuhusu sopitali ile sijui hatua ile imefikiwa au haikufikiwa, nimuombe Mhe. Makamu wa Pili aliangalie hasa suala la Hospitali ya Abdalla Mzee.

Hospitali hii ingawaje iko katika matengenezo lakini iko hospitali ya *temporary*, hii iangaliwe kwa makini pale Mhe. Makamu wa Pili pana tatizo la umeme ambao ni mdogo, damu salama mpaka iwekwe Hospitali ya Wete. Je, anakuja mzazi pale kujifungua hana damu, damu hiyo itapatikana wakati gani, tuliangalie suala hili kwa umakini na Mhe. Makamu wa Pili namuomba aliangalie suala hili kwa makini.

Vile vile upungufu wa maji watu wanapojifungua au wagonjwa pia mtu atoke na ndoo kwa majirani alete maji pale kwa mzazi wake au kwa mgonjwa wake, kusafisha hali ya mwili wake. Hili naliomba Mhe. Makamu wa Pili aliangalie hususan umeme na uwekaji wa damu salama pale.

Mhe. Naibu Spika, nije katika mazingira kifungu cha 9. Utunzaji wa mazingira ni suala muhimu katika maendeleo ya nchi yetu. Ni kweli na mimi naamini hivyo, kwa sababu hivi karibuni tu niliona hali ya Kisiwapanza, tulikwenda pale na kamati tukaiangalia hali ya Kisiwapanza ilivyo. Lakini niseme kwa kuwa serikali inajua suala la mazingira ni kupanda kwa maji katika nchi kavu, lakini vile vile suala la mazingira ni kupanda miti ili kuzuia matatizo yasitokee.

Mimi nasema kwamba katika hali hii inakuwa ni tatizo sugu zaidi kwa wananchi kwa sababu wengine hawaelewi nini uharibifu wa mazingira. Kwa hiyo, Kisiwapanza niseme kwamba ni suala ambalo linatakiwa lichukuliwe hali ya juu kisiwa kile kimo hatarini na siku nyengine unaweza kusema kwamba mtu anakata miti pale lakini si kweli, inaweza kukatwa miti Makunduchi, Nungwi, lakini kwa jinsi kisiwa kile kilivyokuwa kiko chini na kimeinama mafuriko yale yataelemea kijiji kile cha Kisiwapanda.

Kwa hivyo, naomba itoke elimu kubwa zaidi ya kuwaelimisha watu sio Kisiwapanza tu na hata vijiji vyengine. Kwa sababu Kisiwapanza iko bondeni maji yanateremka bondeni na yanapotokea mafuriko ndio kisiwa cha mwanzo ambacho kinafikiwa na hatua hiyo.

Mhe. Naibu Spika, pia niseme je, Mhe. Makamu wa Pili analijua eneo la Ngazimia? Nikuulize Mhe. Makamu wa Pili, eneo hili linatumiwa na watu wengi kufany amazoezi lakini ukiliangalia limeathirika kwa kiasi kikubwa hasa kwa mmong'onyoko wa ardhi, hasa pale maji yanapopiga katika sehemu zile za mchanga kwa kupanda juu kwenye ardhi. Je, serikali inalijua hilo? Je, serikali inachukua hatua gani kwa kuweza kudhibiti kwa kujenga ukuta katika eneo hilo na lisiweze kuathirika.

Vile vile niseme kilio kikubwa kama nilivyokisema kiko katika kijiji cha Kisiwapanza, hili nalo aliangalie vizuri. Pia aidha niseme kwamba mikoko inaweza

kukatwa katika kijiji hicho kama nilivyosema, lakini kuna zaidi ya vijiji vyengine nacho vimeathirika. Kwa mfano Kiuyu, kijiji kile kimeathirika maji tayari yanaingia mpaka misikitini. Naomba hili litolewe elimu kwa wananchi ili waweze kujielewa na waweze kulipanga vizuri.

Mhe. Naibu Spika, nije katika mapambano zidi ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia. Mheshimiwa anasema kwamba tatizo la ukatili na udhalilishaji wa kijinsia zidi ya wanawake na watoto bado linaendelea kushamiri. Nasema hilo kama alivyosema mwenzangu Mhe. Wanu Hafidha Ameir hili halishamiri, hili limelalia hasa. Namuomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais aliangalie hasa suala hili kwa sababu hivi sasa hawaathiriki watoto tunaathirika na sisi wazazi pia.

Kwa hili nawaomba wazazi wenzangu waheshimiwa mjitahidi kuwa pamoja na watoto wetu hasa wanapokwenda skuli tuwe pamoja nao, wanaporudi tuwe pamoja nao na tutapokuwa nyumbani tuwe pamoja nao. Kwa sababu hili ni suala ambalo sasa hivi halina dawa kwa kweli tukiliangalia dawa yake kubwa ni kuwadhibiti watoto wetu, tuwenao pahala pamoja kutokana na suala hili.

Mhe. Naibu Spika, vile vile tuseme kwamba hawa wanaofanya visa hivi ni watu ambao tayari wameshalaanika na wameshalaaniwa na Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Makamu wa Pili tukae kitako kuomba dua, tufanye dua ya pamoja ili kuweza kuwalaani wale ambao wanatufanyia vitendo hivi vya udhalilishaji kwa watoto wetu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo nasema nakushukuru ahsante.

**Mhe. Bikame Yussuf Hamad:** Mhe. Naibu Spka, nakushukuru kwa kuweza kunipa fursa hii na mimi nikatoa mchango wangu mdogo sana katika hotuba hii ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kunijaalia afya njema na uzima na nikaweza kusimama hapa kutoa maoni yangu kwa ofisi hii ya Makamu wa Pili wa Rais. Lakini niipongeze ofisi hii pamoja na watendaji wake kwa shughuli zao wanazozifanya na majukumu makubwa sana. Kwa hiyo, nawaombea mafanikio mema na mimi naiunga mkono bajeti hii sina tatizo nayo.

Mhe. Naibu Spika, mchango wangu kwanza nitauanza kwenye huduma za jamii, tumeona ndani ya kitabu hiki tumeelezwa kuwa serikali imechukua hatua mbali mbali katika kuendeleza huduma za jamii. Ni kweli tunashukuru kwa hilo kuwa serikali imechukua hatua mbali mbali katika kuendeleza huduma hizi za jamii, lakini wasikatae kwamba miongoni mwa ndani ya huduma hizo za jamii basi bado kuna kasoro ndogo ndogo zinatakiwa kufanyiwa marekebisho.

Kwanza suala la afya, kweli wananchi wetu wamepunguziwa kiasi fulani masafa marefu ya kufuatia vituo ni kweli tumeliona. Tumeshuhudia katika vijiji vyetu vingi, vituo vya afya vimejengwa lakini bado huduma hazijapatikana kiukamilifu hasa katika masuala mazima ya kupata madaktari katika vituo hivyo.

Kwa hivyo, tuombe ofisi hii iweze kuliona hili na kuweza kulitatua tatizo hili, ingawa vimeshapatikana vituo hivyo lakini bado upatikanaji wa madaktari ungali na matatizo na upatikanaji wa huduma nzuri bado una matatizo na kupelekea watu kufuata hospitali ambazo wanajua wana uhakika wakienda kule japo panadoli anaweza akapewa.

Hivi karibuni Mhe. Waziri wa Afya alikuwa akipiga kelele sana kuhusu Hospitali ya Mnazi Mmoja kuwa kuna msongamano wa watu lakini hakujua watu walichokuwa wakikifuatia kule ni nini. Lakini pia katika suala la elimu tunashukuru majengo mengi ya skuli yamejengwa kwa nguvu za wananchi, lakini bado majengo hayo yako mpaka leo mengine hayajaezekwa yana miaka kumi.

Kwa hiyo, majengo yako lakini bado kuna kilio cha walimu wa skuli kutoezekewa majengo yale wakati mikataba baina ya wao na serikali watakapofika hatua ya kuezeka basi serikali itachukua juhudi za kuezeka majengo hayo. Kwa hivyo, tunaiomba ofisi na serikali kwa jumla hili walione na kwa sababu mara hii elimu ni moja ya kipaumbele iliyopewa kwenye bajeti, basi tunadhani kuwa hatua kubwa itachukuliwa katika uezekaji wa skuli hizo.

Pia nisiwe mwinzi wa fadhila niipongeze serikali kwa jumla pamoja na Mhe. Rais kwa kututangazia hiyo kufuta michango yote iliyokuwa ikitolewa kati ya wanafunzi wanaopelekwa lakini na watakaofanya mitihani.

Tunashukuru kwa hilo ingawa tunatafunwa huku tunavungiwa ndio mambo tunashukuru na tunaomba Mwenyezi Mungu atujaalie iwe ni siku zote hili la milele wajukuu zetu na vilembwe vije vipate mafanikio hayo.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine niende kwenye suala la mtambuka kuna athari hapa, ofisi imesema kuwa athari ya mafuriko yanayoibuka nchini mwetu mara kwa mara kwa kiasi kikubwa inatokana na uharibifu wa mazingira ikiwa uchimbaji wa mchanga kiholela, ujenzi wa nyumba katika maeneo ya mabondeni kwenye njia za maji na mvua na utupaji wa taka kiholela.
Mimi nakubaliana nayo hayo, lakini pia nailaumu serikali kwa sababu serikali haiko juu tu, serikali imo mpaka kwa balozi wa nyumba kumi wamo na wao hawa wanalipwa na serikali hii hii ni kazi gani wanazozifanya huko waliko hata kufika watu kuwaruhusu kujenga katika maeneo ya mabonde na kusababisha athari kama hizi.

Mhe. Naibu Spika, hizi ni mvua za kawaida za masika zinazonyesha hutokea kipindi kikakaa miaka sita, miaka mitano hazijanyesha mvua kama hizi, lakini hizi ni mvua za masika na bado si mafuriko. Mvua za masika hufika pahali mvua zikanyesha lakini kuna miongo yake ambayo kuwa huanguka kilimia inategemea kitakavyootea, kitaotea jua au kitaotea mvua. Kwa hiyo hili bado halijawa ni mafuriko bali ni mtiririko wa mvua za kawaida. Sasa tunapokuwa tumezikosa mvua hizi hujisahau.

Jambo jengine lakini la kushangaza watu kama hawa wanakwenda Halmashauri kuchukua vibali vya ujenzi hivi vibali utampaje mtu kibali cha ujenzi wakati humjui anapokwenda kujenga?

Ina maana kazi yao wao kukaa kule ofisini wakasubiri malipo ya vile vibali yao yamewaishia, huu sio usimamizi mzuri wa serikali, lazima mtu unampa kibali cha kujenga akakuoneshe anapokwenda kujenga. Lakini sasa unampa mtu kibali humjui anapokwenda kujenga hata kama anakwenda kujenga wapi, ama ingekuwa mwekezaji basi mngekuwa mnamfuatilia lakini watu hawa wa kawaida anachukua kibali anapewa na Halmashauri kwa sababu keshapewa pesa keshatia mfukoni yeye anakaa ofisini kwake hajui mtu yule anakwenda kujenga wapi, hatimaye matatizo yakitukuta hudai kama ni mafuriko kama ni majanga, kumbe majanga tunayasababisha sisi wenywe kwa mikono yetu. Niiombe sana serikali, niiombe iwe makini mambo mengine tusijichangie.

Halafu nataka aje anieleze Mhe. Waziri hawa wasiotokewa na matatizo haya tayari serikali imeshachukua juhudi ya kuwahifadhi sasa hivi lakini itupe mwelekeo hapa, hapa watawahamisha kwenye mabonde au watafanyaje? Lakini pia sababu hizi zinasababishwa na ujenzi mbaya wa barabara, ziangalieni barabara zinazojengwa barabara hazina mitaro ya kupitia maji kweli maji si yatasambaratika yende kwenye majumba, hayana pa kwenda na maji yakija yanatafuta njia ya kwenda. Sasa tuambiwe hii badala ya mashughuliko haya kwa sababu ni mvua hizi mimi nasema kuwa ni mvua za kawaida hayajawa mafuriko haya.

Mhe. Naibu Spika, naomba sana ofisi hii ya Makamu wa Pili wa Rais iwe makini sana au serikali kwa ujumla wasiwaruhusu watu kujenga wanavyotaka wao halafu tukiendelea kuleta mambo yaliyokuwa yanavunja moyo kiasi fulani, wao wanatoa vibali lakini wanashindwa kwenda kukagua maeneo fulani anataka kujenga wapi.
Mhe. Naibu Spika, suala jengine nichukue fursa hii kuipongeza hii Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali kwa usanifu wao wa miradi hii waliyoiendeleza hapa, lakini miradi hii pia ina ujenzi wa tuta ambao unazuwia maji ya chumvi.

Mhe. Naibu Spika, niipongeze serikali kwa hili kwa juhudi wanazozichukua katika ujenzi huu wa matuta ili kuzuwia maji ya chumvi kutoingia. Lakini

ninachowashauri yale matuta yasiachwe kama ni matuta, matuta yale wale wanaojenga wahamasishwe mule juu ya lile tuta mpandwe miti vyenginevyo matuta yale ikiwa yatapandwa majani basi watu watafunga ng'ombe wao na itafika pahali yaje yaporomoke.
Kwa hiyo, nashauri hapa kuwa katika matuta haya basi washajihishwe wale waliojenga matuta katika kijiji kile waweze kupanda miti ambayo itazuia ule mmong'onyoko, ikiwa ni majani watu watawatia ng'ombe halafu yale matuta yataporomoka.

Jengine jana Mhe. Makame Mshimba Mbarouk alivyokuwa akichangia alizungumzia suala zima la Polisi Jamii ambalo kwa kiasi kikubwa bado serikali haijahamasisha kwa kiasi fulani. Polisi Jamii ingeisaidia sana serikali katika mambo madogo madogo hasa yalioko katika vijiji, lakini tunaona kama ni watu wa aina gani tu na tunaona kama yale mambo wameyaanzisha wao labda kwa ruhusa yao.
Kwa hiyo niiombe serikali au ofisi inayoshughulikia masuala haya hawa Polisi Jamii waweze kuwaendeleza siku nyengine wakiwapa angalau mafunzo wakawatia moyo kidogo, kwa sababu sasa hivi tayari matatizo yanaanza kutokea.

Kuna maeneo ya skuli nyengine Skuli ya Kinowe tayari pale pana uharibifu wa wizi wa viti na meza, sasa ukiitaka serikali kuwa basi inapoajiri walimu ajirini na mlinzi wanasema hatuna uwezo huo na ni kweli, kwa sababu skuli ni nyingi hawana uwezo wa kuajiri mlinzi. Lakini sasa yale ni masuala ambayo kila anayekwenda Dar es Salaam anakatwa pesa kwa ajili ya kupelekwa katika Wizara ya Elimu na kushughulikia masuala haya.

Sasa ukisema uwaambie Polisi Jamii hawa hawajashajihishwa kwa chochote si rahisi na skuli zetu za vijini nyingi ziko maeneo yaliyo mbali na watu. Kwa hiyo hawa wakiwezeshwa angalau kuwapatia mafunzo basi wanaweza wakashajihishika ili wakaweza kutekeleza yale mambo madogo madogo yaliyomo katika maeneo yao. Nawaombeni sana Mhe. Waziri hilo suala liangaliwe na lionekane kuwa ni jambo muhimu na waweze kushirikishwa na mambo mengine.

Suala jengine pia niipongeze Tume ya Uchaguzi kwa kuweza kushughulikia mambo yao lakini pia kwa kutoa ushirikishwaji wa makundi maalumu. Naomba niipongeze sana na naomba niwaambie kuwa watu wa makundi maalum wako wa aina mbali mbali kwa hiyo waendelee kuwahamasisha na kuwaona vipi watafika katika vituo vyao vya kupigia kura.

Pia Idara ya Sherehe na Maadhimisho nao niwapongeze kwa jitihada yao kubwa waliyoifanya katika ukusanyaji wa mapato, kwa kweli wameonesha moyo mzuri

na hatua nzuri kutoka shilingi milioni mbili lakini mbili na hamsini mpaka kufikia shilingi milioni kumi na moja ni jambo la kupewa pongezi sana.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo nakushukuru na naunga mkono bajeti hii.

**Mhe. Viwe Khamis Abdalla:** Mhe. Naibu Spika, ahsante na mimi kwa kunipatia fursa hii ya kuweza kuchangia machache kwenye hotuba hii ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Nichukue fursa hii nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuisimamia vyema Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Naibu Spika, nichukue fursa hii nimpongeze Mhe. Makamu wa Pili na watendaji wake wote. Nianze na mchango wangu nikianzia na Idara ya Maafa. Nataka nichukue fursa hii niipongeze Idara ya Maafa kwa jitihada zake walizozichukua wakati wa janga hili la maafa. Lakini pamoja na misaada mikubwa waliyoitoa wakati wa janga hili bado serikali ifanye jitihada za makusudi za kuweza kuwapatia maeneo ambayo kuwa maeneo haya hayataleta matatizo kwa wananchi wetu wa Zanzibar. Kwa sababu wakati wa maafa watu hao wanaopatwa na maafa wanahama kwenye majumba yao baada ya kupita mvua wanarudia nyumba zile zile.

Mhe. Naibu Spika, serikali watenge maeneo maalum ya kuweza kuwapatia wananchi hawa waliofikwa na majanga ya maafa.

Mvua za mwaka jana tuliona vijana wetu wanafunzi wadogo wa skuli wamepoteza maisha na kipindi hiki cha mvua kuna vijana wetu wadogo pia wamepoteza maisha, niiombe serikali wakati wa mvua kubwa watoe tamko maalum la kusitisha kwenda skuli au kuzuwiwa skuli kwa kipindi cha wiki moja mpaka mvua hizi za masika ziweze kukatika ili kuondosha matatizo yanayowakumba watoto wetu wakati wa mvua kubwa za masika.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende kwenye udhalilishaji wa kijinsia unaongezeka siku hadi siku. Tatizo hili Zanzibar halitoondoka kama hatukuweka hukumu, tena hukumu yenyewe kubwa sana. Kwa sababu sasa hivi tunasema kama mtu anafungwa miaka thalathini, akishakufungwa miaka thalathini anatoka, anarudi pale pale mtaani.

Mhe. Naibu Spika, tunaambiwa kama sijui kesi hizi hazipati ushahidi wa kutosha. Sasa Mhe. Naibu Spika, kunatakiwa ushahidi gani, wakati ushahidi upo na mtoto yule anaonekana kama mtoto huyu tendo kafanyiwa, watu wanataka ushahidi gani hasa.

Sasa niiombe Serikali na hichi kipimo kinachoambiwa kama kipimo hichi mpaka leo hakijanunuliwa, hebu tuambiwe na Serikali kipimo ni kiasi gani mpaka mushindwe kukinunua, kama kweli munataka kulishughulikia janga hili. Lilipotokea janga la meli Serikali walipunguza fedha kwenye Idara zote au Wizara zote za Serikali. Je, hili si muhimu katika nchi hii, watoto wetu wanaendelea kudhalilisha siku hadi siku, vijana wanaendelea siku hadi siku. Baadae vijana hawa wakishakudhalilishwa wanapoteza mwelekeo, wanapoteza dira ya maisha, wengine wanakuwa walemavu kabisa. Hebu Serikali itwambie ni lini kipimo hichi au lini chombo hichi kitanunuliwa.

Mhe. Naibu Spika, nichukue fursa hii niipongeze Serikali kwa kuweza kurejesha ile huduma ya elimu bila ya malipo. Kama alivyotamka Marehemu Mzee wetu Abeid Amani Karume na nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar na yeye kwa kuona umuhimu huu wa kuweza kuirejesha elimu kule kule ilikokuwepo.

Mhe. Naibu Spika, sasa hivi Zanzibar tupo tumeingia kwenye mfumo watoto waanze kufanya mtihani darasa la sita. Watoto wa darasa la sita ni wadogo, tena ni wadogo sana. Mtoto unapomwambia afanye mtihani darasa la sita anamaliza pale skuli ni mdogo sana. Mhe. Naibu Spika, mpaka mwezi wa nne vitabu hivi vya kufanyia mtihani darasa la sita bado vilikuwa havipo maskulini.

Na leo sasa hivi keshokutwa watoto wanafanya mtihani wa darasa la sita. Hebu Serikali kabla hawajakaa wakaamua kwanza wajidhatiti kwa makusudi wapange mipango yao hasa kwa hii mitaala ya mitihani, isiwe kuwa wanajiamulia tu na kuwasumbua walimu. Maana kufanya hivi ni kuwasumbua walimu.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kwa hayo machache niunge hotuba hii ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa asilimia mia. (*Makofi*)

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante sana Mhe. Viwe. Sasa nafasi ninampa Nassor Salim Ali.

**Mhe. Nassor Salim Ali**: Mhe. Naibu Spika, ahsante na mimi kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwezesha kunifikisha ndani ya Baraza lako Tukufu na kuweza na mimi kunipa nguvu ya kuchangia kidogo hotuba hii. Lakini Mhe. Naibu Spika, nimpongeze pia Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kazi yake nzuri anayoifanya pamoja kwa kushirikiana vyema na Makamu wa Pili wa Rais katika kutekeleza vyema ilani ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi cha miaka mitano ambacho tunamalizia viongozi wetu wamefanya kazi vizuri na wanastahiki sifa, wametatua matatizo mengi na kuendeleza miundombinu ya barabara, maji, kununulia mpya ya kisasa, kufanya kazi nzuri ambayo muasisi wetu kama vile kujenga upya kiwanja kile cha Kariakoo na kukifanyia ukarabati kile kiwanja cha Pemba, kwa kweli ni kazi nzuri hata ukizingatia kwamba mambo haya waliyoyafanya yako katika ilani ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nije katika kuratibu shughuli hizi za maafa. Mhe. Naibu Spika, na mimi nizungumzie kidogo suala hili kwa sababu ni suala ambalo linawagusa wananchi na mara nyingi huwa linatokea, basi wananchi wamekuwa wakipata matatizo makubwa na sote tumekuwa mashuhuda katika vipindi hivi vya miaka mitatu.

Matatizo haya Mhe. Naibu Spika, sote tuelewe kwamba haya ni mmbo ya Mwenyezi Mungu hayasababishwi na Serikali, lakini ipo haja ya kuzingatia kwamba tunafanya mikakati ya kuweza kukabiliana nayo pale yanapotokea. Nimuombe sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais katika kuweka mipango mizuri katika kukabiliana na matatizo haya. Kujenga uhimili mzuri katika jamii kwenye kukabiliana na maafa pale yanapotokea.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo nije katika hali ya kisiasa. Mhe. Naibu Spika, kwa kweli niseme ukweli na niwaombe sana Waheshimiwa wenzangu kwamba tuwe tunasema hapa mambo ya ukweli. Kwa sababu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kazi wanayoifanya ni kazi kubwa na ya kusifiwa. Mhe. Naibu Spika, utamkuta Mwakilishi anasimama hapa anasema kwamba Serikali hii kazi yake ni ya kukopa tu, hee! jamani kuna Serikali gani ambayo haigopi.

Serikali ulimwenguni zinakopa na wacha Serikali hata sisi Wawakilishi, Wabunge tunakopa mikopa mbali mbali, humu ndani sote tumekopa humu, wafanyabiashara wanakopa katika kutekeleza biashara zao na sisi tunakopa kwa kutekeleza mambo yetu ndani ya majimbo. Sasa Serikali kukopa isiwe ajabu. Sasa niwaombe sana tuipongeze Serikali kwa nzuri wanayoifanya hata kama inakopa lakini inafanya kazi nzuri. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kuhusiana na suala la Katiba inayopendekezwa. Kuna mwenzangu pale amesimama amesema kwamba haungi mkono Katiba hii inayopendekezwa na kuwaomba wananchi kutoipigia kura Katiba hii. Lakini mimi niwaombe sana wananchi wa Zanzibar waisome na kuielewa vyema Katiba hii inayopendekezwa na kutoa maamuzi yaliyokuwa sahihi ya kuipigia kura Katiba inayopendekezwa. Kwa sababu Mhe. Naibu Spika, Katiba hii imebeba maslahi makubwa ya Wazanzibari. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, ndani ya Baraza lako Tukufu baadhi ya Wajumbe wamekuwa wakizungumza kwa hisia kali kuyapigania kuyaleta mafuta ili yawe ndani ya mikono ya Serikali ya Zanzibar. Mafuta yapo, mambo ya kujiunga katika Jumuiya mbali mbali imo. Sasa tumefanya maamuzi yale kuipendekeza Katiba ile kwa maslahi ya Wazanzibari. Kwa hivyo mimi niwaombe Wazanzibari wakae waisome, waielewe na watoe maamuzi yaliyo sahihi kwa maslahi yetu sote. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, hali ya uchumi inategemea amani na utulivu. Bila ya amani, bila ya utulivu wa nchi yetu kutakuwa hakuna maendeleo katika nchi yetu. Niwaombe sana Wazanzibari na Watanzania kwa ujumla tudumishe amani na utulivu tulionao na tuunge Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika uongozi wake bora, katika kujenga na kutuwekeza katika mambo ambayo yanaweka nchi hii katika hali ya amani na tuwapige vita viongozi ambao hawaitakii mema nchi hii. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kuna baadhi ya viongozi wenzetu hawaitakii mema nchi hii kwa kusema maneno ambayo yanatugawa wananchi. Sote ni wamoja, si Mpemba, si Muunguja, si Mtumbatu, si Mmakunduchi, si Mkengeja, si Muwambe, sote ni wamoja. Tujenge nchi yetu katika kujenga maendeleo yetu katika kuleta taifa letu katika misingi ya umoja, amani na utulivu.

Niwaombe sana tunaelekea katika uchaguzi mkuu, tutumie fursa hii katika kuelimisha wananchi wetu kwenye kuwaeleza mambo ambayo ya kuleta amani katika nchi yetu. Na ninawaambia Chama cha Mapinduzi ni chama kipo imara na viongozi wake wapo imara na jembe letu Dkt. Ali Mohammed Shein ataendelea kuongoza nchi hii mpaka 2020.

Ninawahakikishieni kwamba Wawakilishi waliomo humu watarudi kwa kishindo ili kuleta maendeleo katika nchi yetu, kuleta amani na utulivu katika nchi yetu na kudumisha au kuendeleza yale ambayo Dkt. Shein ameanza na kumalizia katika kipindi kilichobakia.

Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, ninaiunga mkono hoja hii kwa asilimia 100. Ninashukuru sana Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe naomba kabla sijaahirisha niseme neno moja. Tukija jioni kwa Wizara nyingi zimeguswa katika hoja za wachangiaji za Waheshimiwa Wajumbe, kwa hivyo kwanza watakuja Mawaziri, Wizara ya Afya, Wizara ya Fedha, Wizara ya Elimu, Wizara ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Watajibu hoja na baadae wataingia wenyewe wenye bajeti hao. Ninachokiomba kwa Wajumbe kwamba wapo Wajumbe mumechangia na mumetoa hoja.

Sasa naomba muje mapema jioni musikilize majibu ya hoja. Mtu atakayekuja nimesikia garini hoja yangu, sitomsimamisha kutoa hoja na huu ndiyo utaratibu wenu; wengi wanasema nilisikia ndani ya gari, haiwezekani Baraza lina heshima yake watu waje hapa wakae wasikilize hoja zao. (*Makofi*)

Kuna Waheshimiwa wawili walikuwa na dharura tutawaombea jioni watapata kuchangia nao japo dakika tano tano. Nao ni Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa, Mhe. Hija Hassan Hija na Mhe. Mlinde Mbarouk Juma.

Watatu hao watapewa japo dakika tano tano nao watoe mawazo halafu tutawaita Mawaziri.

Baada ya maelezo hayo ninashukuru kwa ushirikiano mulionipa tangu asubuhi hadi muda huu. Tunaahirisha kikao chetu hadi saa kumi na moja jioni.

*(Saa 6.50 mchana Kikao kiliahirishwa hadi Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11:00 jioni kikao kilirudia)*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, majadiliano yanaendelea, ipo orodha ndogo ya kuwaita wajumbe kabla hatujafanya majumuisho, ambao wengi wao ni Waheshimiwa Mawaziri, lakini nimpe dakika kumi kama walivyopewa wengine Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa.

**Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa kwa jioni hii ya leo kuweza kuchangia mawili au matatu, katika bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar.

Mhe. Spika, kwanza nichukuwe nafasi hii kuwashukuru sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, pamoja na waziri anayefanyia kazi katika wizara hii Mhe. Mohammed Aboud Mohammed, pamoja na watendaji wote katika wizara hii wanaoongozwa na kaka yangu Dkt. Khalid.

Baada ya pongezi hizo Mhe. Spika, sasa na mimi nijikite moja kwa moja katika michango yangu miwili au mitatu na nitajitahidi kwenda katika maeneo ambayo bado yameachwa na wajumbe hawajachangia. Lakini eneo ambalo nataka nirudie ni eneo zima la mawasiliano katika Baraza letu la Wawakilishi.

Mhe. Spika, pamoja na utamu tunaoendelea nao katika jengo letu hili na Baraza letu hili tukufu, lakini bado iko haja ya kuhakikisha kwamba vipaza sauti vyetu humu ndani pamoja na vyombo vyetu vya kutumia kwa ajili ya sauti, vinafanyiwa marekebisho na hatimaye viweze kuwa katika utaratibu ambao kama Mabunge mengine wanaendelea nao.

Kwa hivyo, ningeomba sana katika bajeti hii tuangalie uwezekano wa kuweza kufanya marekebisho juu ya vitendea kazi hivi na hatimaye tuweze kupata vitendea kazi ambavyo vitaendana na Mabunge ya Kijumuiya ya Madola ambapo sasa hivi tunaendelea nayo.

Mhe. Spika, katika mtandao huo huo wa mawasiliano ndani ya Baraza letu, kuna kitengo hiki cha Hansard pamoja na *Human Resource*. Mhe. Spika, ningeomba sana kitengo hiki kiangaliwe na hawa watendaji watengenezewe utaratibu maalum utakaoendana na afya zao, kama ambavyo vitengo vingine vyote vinavyotumia masuala ya kompyuta wanavyopata baadhi ya *facilities* kwa ajili ya shughuli zao wenyewe za kujenga zaidi afya zao.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo naomba kwenda katika eneo zima la ile ile sheria yetu. Mhe. Spika, kwa kweli nina huzuni kubwa sana kuona kwamba tunamaliza Baraza hili bila ya kukamilisha ile sheria yetu ya Tume ya Utawala wa Baraza, ambayo tulianza nayo kipindi kirefu nyuma na hatimaye leo tunamaliza kikao bila ya sheria hii kuweza kupata baraka katika Baraza lako hili tukufu.

Ningeomba Mhe. Spika, kwa kupitia katika Serikali Kuu, zifanyike juhudi za ziada kwa namna yoyote ile, ili uonekane umuhimu wa sheria hii muhimu katika chombo chetu hiki, ili chombo hiki kiweze kuendesha shughuli zake katika misingi ya kujitegemea wenyewe, kama ambavyo bajeti yetu tunayoipitisha mara hii tunayojitegemea wenyewe pasi na kutegemea nyenzo za wafadhili kama vile ambavyo tumezowea hapo nyuma.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo sasa, haya maeneo mengine wenzangu wameyachangia sana, ukiangalia eneo la udhalilishaji, eneo la *TASAF*, eneo la maafa. Lakini mimi naomba nijikite katika eneo la nyaraka. Mhe. Spika, kwanza napenda nichukuwe nafasi hii katika ukumbi wako huu kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kutokana na juhudi zake ambazo anaendelea kuzichukua, katika kuhakikisha kwamba ile kadhia ambayo ilitokezea katika taasisi za nyaraka inachukuliwa hatua.

Mhe. Spika, naomba kulijulisha Baraza lako hili tukufu, kwamba mara baada ya kuwasilishwa kwa ripoti ile iliundwa kamati ndogo na mimi nikiwa ni miongoni mwa wajumbe hao, tulikwenda kufuatilia suala hili na hatimae tumeweza

kurejesha majibu katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Lakini bado katika hili, naomba kutoa msisitizo maalum, naomba kuwaomba ndugu zetu wa Omar suala hili la nyaraka zetu liweze kupewa umuhimu maalum, ili tuhakikishe yule ambaye anahusika na suala hili anachukuliwa hatua kwa mujibu wa taratibu zilivyo na nyaraka zetu zinarejeshwa hapa Zanzibar, kwani nyaraka hizi ni rasilimali na mali ambayo thamani yake wanaijua Wazanzibari wenyewe, hata ukatumia fedha kwa milioni ngapi, ziwe *dollar* au ziwe *euro* bado haifikii thamani ya nyaraka ambazo zimechukuliwa. Hii ni sawa sawa na kusema kwamba, Waarabu wana msemo wanasema "*mali bila ya daftari ughibu bila khabari*".

Kwa hivyo, na sisi tukiwa tunaendelea kukaa pahala, lakini baadhi ya nyaraka zetu muhimu hatunazo, anazo mtu mwengine amezimiliki. Hili ni tatizo na ni jambo la hatari sana. Kwa hivyo, naiomba sana serikali kwa unyenyekevu wa hali ya juu, pamoja na juhudi ambazo zimechukuliwa na Mhe. Rais na sisi kwenda kunakohusika bado kauli yetu iko pale pale, tunaomba nyaraka zetu zirejeshwe, tunaomba sana hili lizingatiwe.

Baada ya hapo Mhe. Spika, ningeomba kupata maelekezo kutoka serikalini, juu ya suala zima linalohusu yale maeneo ya Menai, hususan katika eneo la Nyemembe. Katika taarifa kule ya kitabu chetu kile cha mipango ya serikali, kuna eneo limezungumzwa kwamba limewekwa katika mipango ya maendeleo. Lakini eneo hili lilikuwa limetengwa ili lisitumike, lakini kinachoshangaza na kushtusha zaidi, kwa sasa kuna wawekezaji naona wale wanatokea Kenya na tayari kuna mawe yamewekwa kule kwa ajili ya matengenezo ya kitu fulani.
Kwa hivyo, tunataka kupata kauli ya serikali. Je, kuna jambo ambalo limeasisiwa kufanywa katika eneo hili, naomba viongozi watakapokuja hapa watusaidie majibu katika hilo.

Jengine Mhe. Spika, naomba vile vile katika kikao cha bajeti kilichopita 2013/2014, mule tulichangia na tuliiomba serikali ifuatilie na hatimaye tuweze kujua suala zima la mgao wetu, juu ya taasisi hizi za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambazo ziko Zanzibar, zinafanyia baadhi ya shughuli zake hapa Zanzibar na Zanzibar inatakiwa ipate gawio lake.
Tunaomba uongozi utakapokuja hapa utusaidie taarifa, kwa sababu katika kikao kilichopita taarifa ya serikali ilikuwa ni kufuatilia hili na baadaye kuja kutupatia taarifa hapa. Lakini kwa bahati mbaya hadi tunafika katika bajeti hii, taarifa hii bado hatujapokea nini hasa mustakabali wa taasisi hizi ambazo ni za Muungano, zina mapato ambayo yanatakiwa kubakia Zanzibar na bado hatujaanza kupokea.

Mfano wa taasisi hizo ni, *TPDC, TCRA, TCAA, TTCL*, Posta na maeneo mengineyo yakiwemo mashirika ya simu ambayo yanafanya shughuli zake hapa Zanzibar. Lakini Shirika letu la Zantel ambalo linafanya kazi upande wa pili wa

Muungano, wao wanalipishwa ada za kule na kodi mbali mbali, lakini mashirika haya yanaendelea na shughuli zake pasina kuchajiwa kodi ya namna yoyote.

Tunaiomba serikali katika kudhibiti na kuhakikisha kwamba mapato yetu tunayasimamia na kuona kwamba tunazuwia mianya yote ya kupotea mapato na maeneo haya yanalipa mapato yetu kwa mustakabali wa kuendeleza shughuli zetu kwa upande wa Zanzibar.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo sasa nakuja katika suala zima la mazingira.

**Mhe. Spika:** Kwa dakika mbili.

**Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa:** Ahsante Mhe. Spika. Katika suala la mazingira Mhe. Spika, ningeomba serikali itufahamishe nini mkakati wake juu ya suala zima la tabia nchi ambayo inaendelea sasa hivi na maji bahari kuja katika maeneo ambayo wananchi wa kawaida wanaishi.

Mhe. Spika, asubuhi nilikwenda katika semina ya kuaga ile taasisi ya *SMOLE* na pale tuliweza kuona baadhi ya picha ambazo zilioneshwa na wenzetu, ambazo zinaashiria hatari kubwa katika kusimamia mlolongo mzima wa suala hili la tabia nchi.

Katika namna ambavyo bahari inajaribu kula ardhi, inaonekana sio muda mrefu wala sio miaka mingi hata kisiwa chetu cha Unguja kinaweza kikageuka katika maeneo mawili kama hatukuchukua juhudi za lazima kuhakikisha kwamba tunatafuta njia muafaka ya kunusuru maeneo ambayo yako wazi na maji yanaingia.

Kwa mfano, kama maeneo ya Kilimani na maeneo mengine ili tuone kwamba tunastiri hiyo hali kabla ya hasara kubwa kuja kwetu. Baada ya eneo hili Mhe. Spika, nimalizie kwa kumuomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais atusaidie.

Tulipokuwa tunachangia kwenye bajeti kuu ya serikali tulisema kwamba hatukufanikiwa vizuri sana katika sekta ya kilimo. Sasa je serikali, kama ambavyo tunatamka kwamba kilimo ni uti wa mgongo wa taifa hili, ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba sekta hii ina imarika, inakuwa na hususan ukizingatia wataalamu wengi sana wamo katika sekta hii, lakini mafanikio yake sio ya kuridhisha mno kama ambavyo tumezowea kuona kwa wenzetu.

Baada ya maelekezo hayo Mhe. Spika, naunga mkono hotuba hii ya bajeti kwa asilimia 99.002 kasoro .008 nitakapojibiwa majibu yangu yakawa sawa na asilimia hizo nazipeleka. Naomba kuwasilisha Mhe. Spika, ahsante.

**Mhe. Spika:** Tunakushukuru Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa. Sasa ni zamu ya mawaziri, mawaziri ambao wameguswa kwa kiasi fulani na hotuba. Lakini pia michango ya wajumbe imewagusa gusa hapa na pale. Tuanze na Mhe. Waziri wa Afya, Mhe. Naibu Waziri atatoa kwa niaba ya Wizara ya Afya na waziri wake, karibu Mhe. Naibu Waziri wa Afya.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Ahsante Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii jioni ya leo. Naomba na mimi nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia sote tukiwa na afya njema na wazima katika kutoa michango mbali mbali ndani ya Baraza lako tukufu Mhe. Spika.

Mhe. Spika, naomba nianze sana kwa kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohammed Shein tokea uteuzi wake alipotuteuwa sisi kuwa katika wizara hii, naweza kusema mimi mwenyewe binafsi kwamba tumesoma mengi sana kutokana na ujuzi, uzoefu na umahiri wake katika sekta ya afya na amekuwa karibu sana kuweka milango yake wazi wakati wowote tukiwa tunahitaji ushauri na muongozo wake, basi yeye hakuna anasita hata kidogo kutupa miongozo hiyo.

Mhe. Spika, naomba nikiri ujuzi na upeo wake katika wizara hii ni mkubwa sana na katika kutimiza ilani ambayo yeye ndio iliyomuweka kwa kupitia Chama cha Mapinduzi, basi naomba niseme wazi kabisa hadi hii leo tumefikia asilimia 98 ya kutimiza ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hayo yatakuja kuthibitishwa wakati bajeti ya Wizara ya Afya itakaposomwa na mambo mbali mbali kuelezwa na yale yote ambayo yamepangwa kufafanuliwa.

Mhe. Spika, pili naomba nichukuwe fursa hii kumpongeza sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, yeye hakuwa nyuma katika kutusimamia na kila alipokuwa akitusimamia sisi tulikuwa tunapata faraja. Wengi walikuwa wakidhania ziara zake ndani ya sekta ya afya au Mnazi Mmoja pale panapotokezea matatizo ya hapa na pale wakidhania kwamba hizi ni ziara za kuja labda kutugomba au kutupa onyo. Lakini ziara hizi daima zimekuwa chachu kwetu sisi za kuongeza kasi za utendaji wetu. Kwa hivyo, tunamshukuru Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na ninampongeza sana jana kwa uwasilishaji wake ambao kwa mara nyengine tena sekta ya afya ameipa kipaumbele. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba nichukuwe fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kaka yetu Mhe. Mohammed bin Aboud ambaye katika upande wa ilani pia yeye ni bosi wangu, maana ndiye Mwenyekiti wetu kwa hapa Zanzibar katika kutimiza yale yote yaliyoahidiwa kutimizwa, hususan katika

sekta ya afya, naomba nimpongeze sana kwa umahiri wake na utendaji wake katika wizara hii.

Pia Mhe. Spika, naomba nimpongeze Mhe. Waziri wa Fedha, ambaye amekuwa daima mstari wa mbele kutupa *priority* ya hali ya juu, kwa sababu anaelewa afya za wananchi ndio uhai wa nchi yenyewe. Kwa hivyo, popote tulipokuwa tunahitaji bajeti katika bajeti yetu, basi yeye alikuwa mstari wa mbele kutupa bajeti hiyo.

Mhe. Spika, baada ya pongezi hizo, naomba niwapongeze pia Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, haya yote waliyoelezea, walionung'unika, sehemu nyengine wametulaumu. Lakini sisi Mhe. Spika, tunayapokea kama chachu ya kuongeza kasi ya maendeleo yetu. Lakini pia nawapongeza kwamba kila linapokuja jambo kama hili au kupatikana fursa kama hii, wao kila wakituambia basi na sisi tunaibua mambo mepya mengi. Kwa hivyo, ahsanteni sana kwa michango yenu, ili na sisi tunaweza kuibua mambo mengi.

Mhe. Spika, miongoni mwa mambo yaliyogusiwa katika Wizara ya Afya, kwanza wauguzi wamelalamikiwa sana, wakati mwengine lugha na hili nimekuwa nikilijibu mara kadhaa. Ni kweli tatizo hilo lipo, lakini tatizo hilo lipo kwa pande mbili.

Kwanza tukubaliane kwamba wauguzi ni muhimu katika jamii yetu, wana umuhimu wao wa aina ya pekee maana huduma wanazotoa na katika hali pia wanayotoa, kwa kweli ni hali ngumu, kwa sababu maeneo ya kufanyia kazi ni madogo, hawana ofisi za kutosha kwa sababu maeneo yetu ni madogo, ndio maana sasa hivi tunaelekea kwenye mpango *referral*, kuongeza hospitali za wilaya ambapo tunatarajia hospitali mbili mpaka tatu zitajengwa kwa misaada mbali mbali, ambapo hivi sasa majadiliano yanaendelea kati ya Wizara ya Fedha, Wizara ya Afya pamoja na wafadhili wenyewe.

Kwa hivyo, kwanza mimi naomba tuwapongeze hawa wauguzi wetu. Lakini pili panapotokea tatizo kama hili la wauguzi kuwa na lugha ama jambo jengine lolote, nawaombeni sana Waheshimiwa Wajumbe kwa kupitia kwako Mhe. Spika, tushirikiane katika kuweka jambo hilo sawa na tushirikiane vipi, kuna sehemu maalum.

Bahati mbaya sana sekta ya afya wao hawapendi kujipigia debe, kwa sababu maadili yao hayawaruhusu kupiga debe, wao maadili yao hayawaruhusu kutoa matangazo kama yale ya kibiashara, kwamba hivi sasa tumewatibu wagonjwa fulani, au tumewapasua wagonjwa fulani au tumefanya vitu fulani, maadili yao huwa hayawaruhusu.

Naomba Mhe. Spika, panapotokezea tatizo lolote tusaidiane na tushirikiane. Kuna kitengo maalum pale ghorofa ya kwanza Jengo la *Administration* (*ELP*), ambacho kinapokea malalamiko yote. Sasa Mhe. Mwakilishi akijakuleta malalamiko yale hapa Barazani bila ya kupitisha kunakohusika, ambapo kuna watu maalum wameajiriwa kwa ajili ya kupokea malalamiko, basi inakuwa hawajawatendea haki wale wauguzi na pia hawajaitendea haki Wizara ya Afya kwa sababu inakuwa haipati kuchukua hatua kwa yale malalamiko yanayotolewa. Naomba niseme nitamke waze kwamba matroni mkuu wa Mnazimmoja mama Magret Masauri yeye ndiye muhusika mkuu wa kupokea malalamiko yote yanayohusiana na hospitali ya Mnazimmoja na Dokta Fadhil Abdalla yeye ndiye muhusika wa vituo vyote vya afya kupokea malalamiko yote. Naomba Mhe. Spika, panapokuwa na malalamiko kama hayo yawasilishwe kwa ushahidi ili hatua zipasazo ziweze kuchukuliwa. Hilo ni kwa upande wa wauguzi na ni suala ambalo liliguswa na Waheshimiwa mbali mbali.

Mhe. Spika, naomba nielekee kwenye kitengo cha *ICU* kipya ambacho kimefunguliwa pale hospitali ya Mnazimmoja katika Sherehe za Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar. Naomba nikiri kwamba kitengo hiki bado hakijaanza kazi rasmi, bado tunatumia ile *ICU* iliyokuwepo zamani. Tatizo kubwa lililokuwepo kitengo hiki kinataka wataalamu hasa wale wanaoitwa wauguzi wa *intensive care* ambao wana taaluma ya kuendesha vifaa vilivyokuwepo pale, mashine zilizokuwepo pale na mambo yote yaliyokuwepo pale.

Naomba niseme kwamba tupo katika hatua ya mwisho hivi sasa kuwaajiri wauguzi waliokuwa *qualified* 40 ili waweze kukidhi haja maeneo mengine yote yalikuwa yana mapungufu, lakini wakati huo huo tuwatoe wale waliokuwa wazoefu waweze kupelekwe kwenye *ICU* mpya ambapo itakuwa inachukuwa wauguzi wa nane kwa siku mara tatu, kwa hivyo, wauguzi 24 ambao watakuwa wanaingia kwa shifti tatu.

Kwa hivyo, suala la *ICU* nawashukuru wale wote waliochangia pamoja nadhani na Mhe. Mwanajuma, Mhe. Shadya na wengine kwamba hili lipo njiani na hivi karibuni tutaanza operesheni maalum ya kuifanyia kazi ile *ICU* mpya ambayo ina vitanda jumla yake vinane vya *ICU* pamoja na viwili vya *VIP*.

Mhe. Spika, nikitoka hapo, naomba nielekee kwenye tatizo lililokuwepo pale Hospitali ya Abdalla Mzee. Naomba niseme Mhe. Spika, ile hospitali ya Abdalla Mzee hivi sasa ni *temporary facilities* na pale hapana nafasi ya kutosha ya kufanya yale yaliyokuwa yakifanyika.

Mhe. Spika, kwa kutumia fursa hii na muda huu mchache uliokuwepo naomba niioneshe kwako Abdalla Mzee mpya inayojengwa ambayo itakuwa ni *referral*

kwa upande wa Pemba ambayo itatoa *facilities* zote, naomba niiwasilishe hii karatasi ipitie kwako na wajumbe waweze kuiyona. Watendaji naomba ipelekeni hii karatasi kwa Mhe. Spika, wajumbe waweze kuiyona.

Na kusema kwamba jengo lile umeme wake ni mdogo. Ni kweli kwa sababu jengo lile halikukusudiwa kuwa hospitali kwa kiwango kama hichi. Kwa hivyo, tumeshazungumza na wenzetu wa *ZECO*, tumeshazungumza na wenzetu wa ZAWA, kwa ajili ya kurekebisha matatizo yaliyokuwepo pale ya umeme pamoja na matatizo ya maji.

Mhe. Spika, naomba niseme pia Hospitali ya Chake Chake, Mhe. Shadya Mohammed, alilitaja hili hakuna daktari mzalendo. Madaktari wapo wazalendo na kwa *figure* niliyoipata ya mwisho hii leo tuna wazalengo saba pale wataalamu ambao wapo. Na kuhusu kifaa cha *blood group* tayari kimeshashughulikiwa na hivi sasa hasa akina mama wajawazito wanaweza wakapimwa pale kwa haya masuala ya *blood group* pamoja na vifaa vyengine kama mashine ya UKIMWI na kadhalika.

Kuhusu suala la maleria Mhe. Spika, naomba niseme kwamba tunashukuru sana Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kupitia kile kitengo chao cha *global fund,* naomba nikitangaze rasmi kwa sababu tumepata kibali na ruhusa ya kutangaza kwamba tumepata msaada wa dola milioni 15 kutoka *global fund* ambao ni sawa au zaidi ya nusu ya bajeti ya Wizara nzima ya afya ambalo suala la maleria litakuwa linashughulikiwa, suala la damu salama, *HIV Aids* pamoja na *TB.*

Mhe. Spika, suala la usafi linaendelea na tunaendelea na msisitizo kila siku kwamba usafi unaendelea kuhimizwa katika maeneo yote ya sekta ya afya. Hivi sasa tunahimiza sana madaktari bingwa zaidi. Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, alitaja hapa tuna madaktari kama 78 wote kwa ujumla madaktari bingwa, lakini hao hawatoshi hata kidogo. Kuna *shortage* bado kama madaktari 50, kwa hivyo, tunaendelea kusisitiza maeneo ya mifupa, maeneo ya *surgery* upande wa Pemba. Hivi sasa tunachukua hata wale wanafunzi au madaktari waliomaliza masomo ya *private* tunawachukuwa.

Mhe. Spika, pia, tuna mpango wa kuchukuwa ma-*intern* tumechukua zaidi ya *interns* 50 ambao hivi sasa tunafanya kazi nao na tunatarajia kuwaongeza zaidi ili wafanye. Kwa hivyo, bado uhaba wa madaktari bingwa upo na tunakaribisha maombi ya madaktari bingwa. Nitawahimiza sana Wawakilishi wawahimize watoto wao kusomea udaktari kwa sababu baada ya hapo kazi za uhakika zitakuwepo, masomo ya uhakika ya kusomea ubingwa yatakuwepo.

Mhe. Spika, kwa kumalizia dakika zangu 5 naomba nikushukuru tena kwa kunipa nafasi hii na kwa hayo, machache naomba kuwasilisha na kuunga mkono hoja hii.

Mwisho kabisa dogo tu nilikuwa nimeliwacha ni lile suala la Mhe. Mshimba Makame, aliloliuliza juu ya ile mashine ya *full blood picture* nimeifatilia kwa karibu sana mashine ile tunapewa msaada na Jumuiya moja inaitwa *ICAP* ambayo ni Jumuiya ya Afrika Mashariki, wao wana utaratibu wa kununua mashine ile ambao haumo katika utaratibu wa manunuzi ya serikali, yaani *Government Procurement Act,* wao wananunua kwa utaratibu wao. Kwa hivyo, mashine ile huwa tunapokea tayari na kila mwaka huwa tunafamyiwa *service* ama *calibration* kwa ajili ya kufanya kazi. Kwa hivyo, hilo nalo limetatuliwa.

Suala la magodoro kuwa membamba hilo Mhe. Spika, tunaendelea kulifanyia kazi na hivi karibuni tunatarajia kuongeza na pia tunakaribisha misaada mbali mbali. Wizara ya Afya ni jambo ambalo linawagusa wananchi wote, kwa hivyo, tunaendelea kukaribisha misaada mbali mbali kwa wale wote wanaotoa misaada ya magodoro na vifaa vyengine vya afya.Tunaendelea kuwashukuru wale ambao tayari wameshatuchangia.

Mhe. Spika, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

**Mhe. Spika:** Nakushukuru sana Mhe. Naibu Waziri wa Afya, kwa maelezo hayo. Mhe. Waziri wa Fedha, nitamruka kidogo kwa sababu yeye ndiye mdakaji wa mipira yote, nitamruka kidogo na niende kwa Waziri wa Elimu, Waziri hayupo, Naibu Waziri hayupo, Kaimu Waziri yupo, basi wacha twende kwa Waziri Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:** Ahsante sana Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi kuongea machache juu ya yale yaliyochangiwa kuhusiana na sekta ambayo ipo ndani ya Ofisi yetu, sekta moja iliyoguswa sana ni ya mazingira.

Lakini kabla ya hapo Mhe. Spika, naomba uniruhusu nimpongeze sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kwa uwasilishaji mzuri wa hotuba yake. Lakini pia nimpongeze Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili na watendaji wote kwa matayarisho mazuri ya Bajeti hii, imefahamika na niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu waiyunge mkono kwa asilimia mia moja.

Mhe. Spika, naomba nianze na Mhe. Shadya Muhammed Suleiman, lakini wakati huo huo nikisaidia kumjibu au kutoa maelezo kwa ajili ya yale yaliyochangiwa na Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi na Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa. Mhe. Spika, Wajumbe wote hawa walielezea juu ya suala ambalo linaikabili nchi yetu,

Visiwa vyetu viwili vya Unguja na Pemba, suala la maji ya chumvi ambayo yamevamia juu ya ardhi katika maeneo mengine ikiwa ni ardhi ya kilimo na kuuliza nini mikakati ya serikali au serikali inajipangaje katika kutatua tatizo hilo.

Mhe. Spika, serikali inatambua athari zinazoambatana na mabadiliko ya tabia nchi yaliyopo katika maeneo mengi ya Zanzibar ikiwa ni pamoja na eneo la Kisiwapanza ambalo ndilo hasa ndilo lililogusiwa hapa. Hivi sasa Zanzibar ina jumla ya maeneo 148 ambayo yameingia maji ya chumvi. Serikali ipo katika hatua za mwisho za kutayarisha mpango wa utekelezaji *(action plan)* kwa mujibu wa mambo yaliyopewa vipa umbele na mkakati wa Zanzibar wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabia Nchi ambao umetengenezwa.

Kabla ya kukamilika utayarishaji wa mpango huo wa utekelezaji, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imetayarisha mradi wa kujenga uwezo wa kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi katika maeneo ya pwani. Mradi huu utatekelezwa katika maeneo ya Bagamoyo, Pangani, Rufuji na Zanzibar. Katika hili eneo la Zanzibar maeneo ya mradi huu yatahusisha maeneo ya Kisiwapanza haya ambayo Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wanayaongelea, eneo la Tumbe, eneo la Ukele, eneo la Chovuno, eneo la Bwawani, na eneo la Kilimani.

Shughuli zitakazofanywa Kisiwapanza ni pamoja na upandaji wa hekta 200 za miti ya mikoko, upandaji wa hekta saba za miti mengine ya pwani, yaani *Kosovo vegetation* ya aina nyengine, lakini pia kuweza kujengwa ukuta wa mita 75 kwa ajili ya kuzuia maji ya chumvi kukiathiri kisiwa hicho.

Mhe. Spika, ni imani ya serikali kuwa shughuli hizi zitapunguza kasi ya athari za mabadiliko ya tabianchi katika kisiwa hicho. Pamoja na jitihada hizi za serikali niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kuwa wengi wameyatambelea maeneo haya wajaribu sana kuzidi kutoa elimu ndani ya maeneo yao ili watunze mazingira.

Mhe. Spika, mbali ya kupanda kwa kina cha bahari, lakini mambo mengine ambayo yanasababisha athari hizi za mabadiliko ya tabianchi kutukabili zinasababishwa na sisi wenyewe binaadamu katika shughuli zetu za kila siku ikiwemo ukataji wa miti ovyo iliomo katika eneo la baharini yaani *(Costal Areas)* miti hii ya mikoko na ya aina hiyo.

Mhe. Spika, Mhe. Mwanajuma, aliuliza iwapo Mhe. Makamu wa Pili wa Rais analifahamu eneo la ngazi mia na kujua kinachoendelea hapo. Naomba nimuarifu Mhe. Mwakilishi, kwamba Mhe. Makamu wa Pili kwa kuwa amekuwa mstari wa mbele sana katika kuangalia shughuli za athari ya mabadiliko ya tabianchi na

mazingira na serikali kwa ujumla analielewa eneo hili la ngazi mia na hali iliyokuwepo pale ambayo ni mmong'onyoko wa fukwe katika eneo hilo.

Mhe. Spika, kwa ujumla maeneo yenye mmong'onyoko wa fukwe Zanzibar ni mengi na karibu maeneo yote yenye fukwe za mchanga yanakabiliwa na tatizo la mmong'onyoko wa fukwe hizo. Kutokana na wingi wa maeneo hayo sio rahisi serikali kuweza kuyashughulikia yote kwa wakati mmoja. Hivyo serikali imeshaanza hatua za kuyashughulikia maeneo hayo ambayo athari zake ni kubwa zaidi. Katika eneo la ukanda wa Mbweni mpaka eneo la Kilimani eneo lilipewa kipa umbele ni eneo la Kilimani ambalo nimelitaja kwamba litakuwemo katika *pilot project* za jinsi ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Mhe. Spika, katika eneo hili narejea kuwaomba Waheshimiwa Wajubme wa Baraza la Wawakilishi watusaidie sana na jamii ambayo wapo nayo. Pamoja na kwamba tunahitaji kuwa na shughuli zetu za kimaisha kila siku, lakini katika uzito huo huo tunahitaji kuyatunza mazingira yetu ili tupunguze athari za mabadiliko ya tabianchi.

Mhe. Spika, Mhe. Mgeni Hassan Juma na yeye aligusia mahusiano yaliyopo kati ya mazingira na maafa ambayo yametokea hiribuni ndani ya visiwa vyetu kutokana na mvua ambazo zilinyesha kidogo kwa wingi kuliko ambavyo tumezowea. Mimi nikubaliane kwamba ni kweli kuna uhusiano wa moja kwa moja juu ya suala zima la utunzaji wa mazingira, suala la ujenzi na suala la maafa ambayo yanaweza kutokea kama haya ambayo yametokea.

Nikubaliane na yeye na niwaombe sana Waheshimiwa wananchi wetu kwamba ni lazima waheshimu na wafuate utaratibu wa majenzi kama unavyotolewa na mipango miji, lakini vile vile waache kujenga kwenye njia za maji. Mhe. Spika, wananchi wetu wanajijengea kiholela na wanaziba njia za maji hali ambayo inasababisha mafuriko kama ambayo tumeyaona.

Mhe. Spika, vile vile, sambamba na hili niwaombe Waheshimiwa Wawakilishi wawahimize wananchi na wenyewe wananisikia kwamba ni lazima tuweze kuyatunza mazingira na kuyaweka safi na kuhakikisha kwamba takataka ambazo tunazizalisha tunazitupa katika maeneo yaliyopangwa, tusitupe taka ovyo. Sehemu kubwa imechangia katika maafa haya ni takataka zinazotupwa ovyo zilizochukuliwa na maji na zikaweza kuziba sehemu za kupitia maji na mitaro katika katika maeneo hayo.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba niunge mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na nakushukuru sana.

**Mhe. Spika:** Mhe. Waziri, tunakushukuru, sasa turudi kwenye Wizara ya Elimu, Mhe. Waziri wa Elimu, naona Naibu Waziri yupo, karibu.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu:** Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa na mimi ya kutoa ufafanuzi juu ya hotuba hii ambayo amewasilisha Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais juu ya masuala mazima yanayohusu Wizara ya Elimu.

Mhe. Spika, katika wizara yangu mengi ambayo yalizungumzwa mengi yao ilikuwa ni pongezi kwa serikali ambavyo imefikiria kufuta malipo kwa wazazi na namna gani ambavyo Wizara ya Elimu italisimamia hilo. Nataka niahidi Baraza lako tukufu kama Wizara ya Elimu itaisamamia kauli hiyo ya serikali na kuifanyia kazi kwa vitendo.

Mhe. Spika, jengine ni juu ya suala la mitaala yetu. Hilo niseme kama tunalichukua na Wizara tutaona ni namna gani ambavyo tunaweza tukalifanyia kazi kwa kushirikisha wadau wote wa elimu.

Mhe. Spika, pia, jambo lililozungumzwa ni kuhusu vyuo vyetu vya amali. Ni kweli nia ya serikali na Wizara ya Elimu kwa jumla ni kuwa wanafunzi wale wanapotoka katika Chuo waweze wenyewe kujitegemea. Kama tunakumbuka kuna mfuko maalum ambao umeanzishwa kwa ajili ya kuwawezesha wanafunzi hao wanapotoka katika vyuo hivyo kuunda vikundi vyao ambavyo vitawasaidia kuanzisha kile ambacho wao wenyewe wanahisi waanzishe kutokana na mafunzo yao ambayo wameyapata.

Kwa hivyo, hilo Mhe. Spika, ni kulitilia mkazo kama Waheshimiwa Wawakilishi ambavyo wamelifikiria na sisi Wizara ya Elimu ndio hasa lengo letu kuhakikisha kama wanafunzi wetu wakitoka pale, badala ya kutegemea ajira kutoka Serikalini, basi wao wenyewe waanze kujiajiri.

Mhe. Spika, nadhani ni hayo na mengine mengi tutazungumza katika hotuba yetu ambayo tunatarajia tarehe 9 Juni, 2015. Ninakushukuru sana Mhe. Spika.

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Mhe. Spika, kwanza na mimi nataka niunge mkono asilimia mia moja hotuba ya Makamu wa Pili wa Rais ambayo imesomwa jana na Mhe. Balozi Seif Ali Idd. Mhe. Spika, kwa upande wa Wizara yangu kuna *issues* 3 ambazo kidogo ningeliomba nizitolee ufafanuzi ingawa *issue* moja niliitolea ufafanuzi juzi lakini naona niitolee tena ufafanuzi ili tuweze kufahamiana vizuri.

La kwanza ambalo liliulizwa ni suala zima kwamba tumeondoa misaada ya *GBS* kwenye bajeti, je, inapotokea ikapatikana tunafanyaje? Naomba Mhe. Spika, nifahamike vizuri sana, kitabu changu cha hotuba ya bajeti ukurasa wa 39 kuna

*table* hapa, katika *table* hii tumeweka 4.5 misaada ya kibajeti lakini ukiangalia katika mwaka 2015/16 nimeweka 100T hii ina maana Mhe. Spika, sio kwamba imewekwa tu. Sasa nitaomba kidogo niitolee maana yake. Maana yake nini?

Mhe. Spika, maana yake ni kwamba pesa zitakapopatikana zitatumiwa, lakini matumizi yetu hayatazidi bilioni 830, yatakapozidi bilioni 830 na kama kunatakuwa na ulazima wa kutumia zaidi ya bilioni 830 ambayo imepitishwa na Baraza lako Tukufu, Serikali italazimika kuomba *supplementary budget*, hii ndio maana yake. Kwa hivyo, tunatarajia kwamba zikipatikana zitatumiwa na kama utakumbuka baadhi ya waheshimiwa wajumbe walisema hakuna haja ya kukopa bilioni 30. Kwa hivyo, zikipatikana suala la kwanza tutaachana na kukopa bilioni 30 ili tuweze kutumia zile lakini kama itahitajika kutumia zaidi ya bilioni 830 Serikali italazimika kuleta mswada wa *supplementary budget* kuliomba Baraza lako Tukufu.

Kwa hivyo, hilo ni kwamba kitakachopatika sisi tutatumia tu lakini masharti yetu kwamba tusizidi bilioni 830, hili nilikuwa nimetaka nilitolee ufafanuzi ili waheshimiwa wajuwe kwamba hakuna kitakachoachwa. Hivi sasa Mhe. Spika, tunafatilia, sio kwamba tumekaa tu kwamba tumesema misaada tumeiwacha tumekaa tu tunafatilia. Kwa sababu kuna misaada ya *GBS* iko katika makundi mawili; kuna misaada ambayo inatolewa na nchi washirika na kuna misaada ambayo inatolewa na mashirika ya kimataifa kama Benki ya Dunia, kwa hivyo, yale tunaita *multilateral* na kuna misaada ambayo inatolewa na nchi inaitwa *bilateral.* Sasa hayo Mhe. Spika, tunafuatilia na zikipatikana tutazitumia.

Hoja ya pili ambayo iliyoibuliwa ni kuhusiana na *account* ya TEGETA, nililitolea ufafanuzi, walio-*sign* Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndio walio-*sign* hii misaada kwa niaba yetu. Kwa sababu ya taratibu zetu za ndani misaada inapopatikana *share* yetu sisi ni asilimia 4.5. Tumejaribu kuzungumza na wenzetu, tumewaambia ilipotokea *EPA* mmetuhusisha Zanzibar wakati Zanzibar hatuhusiki, ilipotokea hii mmetuhusisha wakati sisi hatuhusiki, lakini kinacholetwa nchini kinaletwa kwa ajili ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Sisi tumejaribu kuzungumza nao lakini kilichopatikana kama vile nilivyokisema katika hotuba ya bajeti mpaka ninasoma bajeti zilizopatikana na 8.5 *billion shillings* badala ya 40 *billion shillings.* Lakini wanalijua hili si kwamba hawalijui, lakini wanaona kwamba wakizileta itakuwa tayari wamewapa Tanzania na wao ndio waliotiliana nao mkataba. Kwa hivyo, tutaendelea na kuwafahamisha wenzetu mpaka pale ambapo tutapopata nafasi kuwa na mkataba au makubaliano yetu wenyewe Zanzibar badala ya kupitia Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

La mwisho ambalo liliibuliwa ni suala la bajeti ya Baraza la Wawakilishi. Nimesikia wamesema bajeti ya Baraza la Wawakilishi ndogo, nataka niseme kwamba huu ni mwaka wa demokrasia Mhe. Spika, tumelazimika kutumia fedha nyingi kwa ajili ya demokrasia na tungekuwa na uchumi mkubwa, tungekuwa na mapato makubwa, nadhani Baraza la Wawakilishi wala wasingepiga kelele wangepata pesa wanazozihitajia na Wizara nyengine zote, tumeweka bilioni 7.5 kwa ajili ya uchaguzi. Tumeweka bilioni 8.5 kwa ajili ya kuwalipa waheshimiwa wastaafu, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Hizo mbili tu ukizijumlisha zinakupatia bilioni 16, bilioni, 16 ingekuwa hakuna huu mwaka wa demokrasia nadhani zingetosha kuwapa Baraza la Wawakilishi *and extra* bilioni 3 na wizara nyengine kuwapa bilioni 1, bilioni 2. Lakini hizi tu na hizi zinakuja *once after every five years,* miaka mitano, mwaka mmoja, kila baada ya miaka 5 inakuja hiyo nyongeza. Kwa hivyo, mimi nasema Mhe. Spika, kwamba Baraza lituvumilie, bajeti inayokuja kutakuwa hakuna *costs* hizi, hakuna gharama hizi mambo yatakuwa mazuri. Lakini kwa hili nasema uchumi wetu ndio umetupatia mapato kidogo, lakini imebidi hicho hicho kidogo tugawane kwa mujibu tunavyokipata.

Mhe. Spika, kwa wizara yangu yalikuwa ni hayo matatu. Ahsante sana.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, kwanza naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu ili nianze kujibu hoja mbali mbali ambazo zimeletwa mbele ya Baraza lako na waheshimiwa wajumbe.

**Mhe. Spika:** Tunaotoka nje tukumbuke kwamba baada ya Mhe. Waziri hapa na pia kama Mhe. Makamu wa Pili wa Rais atakuwa na neno basi tunafanya maamuzi, tusiitereshe *quorum* turudi baada ya kumaliza hiyo dharura kwa muda mfupi. Mhe. Waziri endelea.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Lakini pia Mhe. Spika, nikupongeze sana wewe kwa namna unavyoliendesha Baraza hili tukufu kwa umakini, ustadi na kwa demokrasia ya hali ya juu. Tunakupongeza na Mwenyezi azidi kukusaidia, akupe uwezo zaidi wewe na wengine wote wanaoliongoza Baraza hili. Aidha, ninamshukuru sana Mhe. Naibu Spika, waheshimiwa wenyeviti wetu wote wawili kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya katika kusaidia katika kuliongoza Baraza hili.

Mhe. Spika, naomba nitoe shukurani maalum kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwanza kwa imani yangu juu yangu ya kuniteua kuwepo katika Ofisi hii ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kipindi chote tulichoanza nacho cha awamu hii. Mwenyezi Mungu amjaalie azidi kumpa imani

tumalize pamoja kwa salama *Inshaallah*. Vile vile, nimpongeze yeye Mhe. Rais kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya kutumikia nchi yetu na mashirikiano makubwa anayotupa katika kuongoza Wizara yetu. Kwa kweli Mhe. Rais amekuwa dira ya kuongoza Wizara hii.

Aidha, nichukuwe nafasi hii Mhe. Spika, kumshukuru sana Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mashirikiano makubwa anayotupa katika utendaji wetu wa kazi. Lakini Mhe. Spika, shukurani maalum zende kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa namna ambavyo anatuongoza katika Wizara yetu, yeye amekuwa siku zote mfano mzuri wa utendaji wa kazi katika ofisi yetu, ametusaidia sana kwa ushauri na miongozo na wakati wote pale tunapokosea anatukosoa kwa busara kubwa sana. Kwa kweli kufanya nae kazi tunasikia furaha ya hali ya juu. Kwa hivyo, tunakushukuru sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa namna tunavyokuwa na wewe.

Mhe. Spika, naomba pia niishukuru sana Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa, kuanzia Mwenyekiti na wajumbe wote Mhe. Spika, Kamati hii imekuwa dira ya utendaji wetu wa kazi. Imekuwa ikituongoza kutoa miongozo, ikitushauri pale panapostahiki na kwa kweli kama kuna mazuri tunayofanya Ofisini kwetu basi na Kamati hii ni sehemu ya mazuri hayo.

Mhe. Spika, pia, niwashukuru wajumbe wote wa Baraza hili Tukufu kwa namna ambavyo wanashirikiana na ofisi yetu. Kwa kweli wanatupa mashirikiano makubwa, wanatusaidia katika utendaji wetu wa kazi na siku zote wamekuwa mfano mzuri wa kuhakikisha kwamba wanatuwezesha kutekeleza majukumu yetu. Sina cha kusema zaidi ila kusema ahsante sana waheshimiwa wajumbe wote kwa kazi kubwa mnayoifanya. Na mimi niwatakie kheri na mafanikio makubwa nyote pamoja na mimi ili turudi tena katika Baraza hili. *(Makofi)*

Mhe. Spika, niwapongeze sana wale wote waliochangia katika hotuba hii na wale wasiopata nafasi ya kuchangia naamini nia zao zilikuwa moja katika kuimarisha na kukosoa pale panapohitaji kukosoa ili tuweze kutekeleza wajibu wetu vizuri zaidi. Atakapokuwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, atawatambua Waheshimiwa Wajumbe waliochangia na vile vile kutoa ufafanuzi zaidi pale atakapoona inafaa katika maeneo yake.

Waheshimiwa Wajumbe, walizungumzia sana mambo mengi lakini yaligusa sana katika maeneo ya hali ya siasa, yaligusa sana katika Tume ya Uchaguzi, yakagusa katika maeneo ya Mtambuka, yakagusa katika maeneo ya maafa na kadhalika. Nitajitahidi kueleza kwa muhtasari vile ambavyo tutaweza kutokana na hali ya muda.

Mhe. Spika, ni kweli kabisa kama alivyosema Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwamba tujipongeze wananchi wote wa Zanzibar na kabla ya kusema hivyo nataka niwashukuru sana sana wananchi wote wa Zanzibar kwa namna ambavyo wameunga mkono Serikali yao wakasaidia na wakawa na uvumilivu mkubwa katika uongozi wa Serikali katika kipindi cha awamu ya saba.

Mhe. Spika, mwenyekiti wetu wa kamati alisema tujipongeze kwa hatua tuliyofikia ya nchi yetu kwa ajili ya umoja wetu, kwa ajili ya amani yetu na kwa ajili ya mafanikio yaliyopatikana katika kipindi hiki cha miaka 5. Na alisema hivyo kwa sababu mfumo huu sio tu mfumo mpya kwa Zanzibar bali hata duniani mfumo wa namna hii bado ni mpya. Kwa hivyo, kuweza kuumudu na tukaweza kuendesha Serikali yetu na kwa mafanikio makubwa lazima tujipongeze sana sana na tumpongeze sana Mhe. Rais wetu na viongozi wetu wakuu na viongozi wote na wananchi wote kwa kazi iliyofanyika kufikia hapa. Busara za viongozi wetu zimetuwezesha kutekeleza mengi na kupiga hatua kubwa ya mafanikio katika nyanja za kiuchumi, kijamii, kisiasa hususan katika maeneo ya afya, elimu, miundombinu, maji, kilimo na kadhalika.

Mhe. Spika, kuhusu hali ya siasa sote tulizungumzia sana kuhusu suala la amani na utulivu na mimi nataka niunge mkono kwamba jambo hili ni muhimu katika nchi yetu na Serikali yetu siku zote itahakikisha inaimarisha amani na utulivu wa nchi yetu na tukijua kwamba umoja, amani na utulivu ndio raslimali kubwa ya nchi yetu, kwa hivyo, mafanikio yetu yanatokana na amani. Waheshimiwa Wajumbe wengi hapa wamesema kwamba lazima tuyaseme haya ya amani na vitendo vyetu vielekee kwenye amani, tusiseme maneno matupu, lakini vitendo vyetu viwe katika amani. Kwa hivyo, sote kwa pamoja tukubaliane kwamba msingi wa mafanikio ya nchi yetu ni amani na utulivu.

Mhe. Spika, pande zote mbili kwa upande wa CCM na CUF kila aliyenyanyuka alizungumzia suala la amani, maana yake wananchi wote wa Zanzibar wanaujua umuhimu wa amani na utulivu. Kilicho mbele yetu ni sisi viongozi sasa kuhakikisha kwamba tunaisimamia hiyo amani na tusiwe chachu na wa kuchochea vurugu na malumbano katika nchi yetu, likitokea lolote sisi ndio dhamana, likitokea lolote sisi ndio tulioharibu, wananchi wa Zanzibar ni watiifu na wako siku zote tayari kusikiliza viongozi wao.

Mhe. Spika, kwenye hili nataka nichukuwe fursa hii ya kipekee kumpongeza sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Busara zake, hekima zake, uvumilivu wake umetusaidia sana kutufikisha hapa tulipo. Tumuombee dua Rais wetu azidi kupata afya njema, azidi kuwa na umri wenye kheri yeye na familia yake ili azidi kutuongoza katika nchi yetu. Na mimi nataka nikubaliane

sana na wale waliosema na Mungu amjaalie amuwezeshe katika kipindi kinachokuja aendelee tena kuiongoza nchi yetu.

Mhe. Spika, katika michango hii iliyozungumzia amani Mhe. Suleiman Hemed, alisema neno moja kubwa sana, akasema Serikali inasemaje kuhusu kuchokozana kwa vyama vyetu viwili vikubwa vya CCM na CUF, yeye alitoa mchango wake kwa maandishi. Neno la Serikali inasema tusichokozane, haina haja ya kuchokozana bali tupendane, tuhurumiane na tufanye kazi kwa pamoja, hiyo ndio kauli ya Serikali.

Mhe. Spika, vile vile, wajumbe kwa kiasi kikubwa sana walizungumzia suala la Uchaguzi Mkuu. Mimi nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba nia na dhamira ya Serikali yetu ni kuendesha uchaguzi huru na wa haki na kila mmoja apate haki yake ya kidemokrasia ya kupiga kura. Huo ndio msimamo wa Serikali na hiyo ndio nia na dhamira ya Serikali na inakusudia kuendesha uchaguzi huu katika mazingira ya amani na usalama katika nchi yetu. Kwa hivyo, sote kwa pamoja tushirikiane tukiamini kwamba uchaguzi utaendeshwa kwa misingi ya Kikatiba na Sheria iliyopo ili kuvuka kila tatizo ambalo linaweza kujitokeza. Maana Katiba yenyewe inatafsiri vizuri katika kwenye suala zima la kuendesha uchaguzi.

Mhe. Spika, Katiba yetu katika Ibara ya 119 kifungu cha 12 inasema na naomba ninukuu;

"Katika kutekeleza madaraka yake kwa maana ya Tume ya Uchaguzi kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii Tume ya Uchaguzi haitalazimika kufuata amri au maagizo ya mtu yeyote yule au Idara yoyote ila ya serikali au maoni ya chama chochote cha siasa, bali itafanya kazi zake kwa uhuru kwa misingi ya Katiba na Sheria inayoongoza. Kwa hivyo, hiyo ndio imani yetu. Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba huo ndio msimamo na serikali haiingilii wala haitoingilia shughuli za Tume ya Uchaguzi.

Nawaomba tu Waheshimiwa muwelewe na Tume yenyewe muundo wake umekuja kutona na mazungumzo ya muda mrefu kati ya vyama vyetu vyetu viwili. Kwa hivyo, muundo wa Tume uliyopo umeundwa tofauti sana na Tume nyengine ulimwenguni. Tume yetu hii imetoa nafasi kuwa na wajumbe kutoka pande mbili zetu za vyama. Kwa maana imetoa nafasi kutoka upande wa CUF imetoka nafasi kutoka upande wa CCM, maana katika Katiba kifungu 119(1) kinaeleza vizuri kinasema;

"Kutatoka wajumbe wawili watakaoteuliwa, watakaopendekezwa kwa Rais ambao watatokana na ushauri wa kiongozi wa shughuli za serikali katika

Baraza hili na vile vile kuwatakuwa na Wajume wawili watakaopendekezwa kwa Rais, kutoka kiongozi wa Upinzani katika Barazani hili."

Kwa hiyo, hiyo ndio *structure* yetu ilivyoundwa ya Tume ya Uchaguzi. Kwa hivyo, Tume ya Uchaguzi yenyewe imewakilishwa vizuri na pande zote na inafanya kazi zake kwa pamoja. Kwa hivyo, penye kasoro wenyewe wanazungumza wakaondoa kasoro hiyo, penye mafanikio wanazungumza kuweka sawa mafanikio.

Kwa hivyo, naomba tuondoe wasi wasi kuhusu utendaji wa Tume na hatupaswi kuingilia wala kutia jambo lolote la kisiasa katika masuala mazima ya Tume ya Uchaguzi bali tuiwachie Tume ifanya kazi zake.

Waheshimia katika katika suala la Tume walitaka kujua uwandikishaji wa mara ya pili utaanza lini. Mhe. Spika, uwandikishaji wa mara ya pili utaanza tarehe 1/6/2015 na utamalizika tarehe 5/7/2015 na utanzia Micheweni Pemba na utamalizia Wilaya ya Kusini Unguja. Hiyo imetokana na mashauriano ya wadau wenyewe, walivyokutana na Tume badala ya kufanyika ile tarehe ya mwanzo tarehe 15 Mei wakaomba isogezwe mbele na ianzie tarehe 1 Juni. Kwa hivyo, kwa kuheshimu maoni ya wadau ndio Tume ikaamua hivyo na zipo sababu za msingi walizofikia hivi.

Vile vile, kuhusu *display* ya daftari itakuwepo kama kawaida kuanzia tarehe 20/7/2015 mpaka tarehe 26/7/2015, kwa sababu hiyo ni utaratibu wa kisheria tunataka siku 7 ufanyike kuonesha ile orodha yote ya kwenye daftari ya wapiga kura. Lakini vile vile kuna nafasi nyengine ya vyama kujiridhisha, siku 8 kabla ya upigaji wa kura, vile vile, nafasi ya daftari itaonekana na watu wanaweza kujiridhisha wenyewe wenye vyama vyao kuona katika daftari la kudumu la wapiga kura. Kwa hivyo, hatuna haja hata kidogo ya kulumbana na kuvutana kwa mambo ambayo yapo kisheria, tuiwachie sheria ichukue mkondo wake. Pale inapoonekana kuna sheria inavunjwa ni utaratibu wa kisheria ndio utakaotuweka katika mistari ya pamoja ili mambo yetu yaende kwa salama na amani.

Mhe. Spika, iliuliziwa na hasa na kamati bajeti ya Tume kutoka kwa wafadhili mbona haikuoneshwa katika vitabu vya Tume katika mwaka huu. Kubwa kwa sababu vitu vingi ambavyo vitaletwa kwenye msaada wa wafadhili katika Tume ya uchaguzi mara hii itakuwa ni vifaa sio sana *cash*. Ndio maana haikuonyeshwa moja kwa moja sasa itakapopatikana *cash* kwa utaratibu ule ule alioueleza Waziri wa Fedha pia itaonekana kwa utaratibu huo. Kwa hivyo, naomba tuondoe wasi wasi pale ambapo zitakuja fedha zitatumika kwa utaratibu ule tu ambao Baraza limeruhusu na kama kutakuwa na mahitaji mengine basi Baraza litaitishwa kufanya shughuli hiyo kwa mujibu wa sheria ilivyo.

Mhe. Spika, eneo jengine ambalo Wajumbe walilizungumzia sana ni sualala rushwa na ubadhilifu. Nataka Mhe. Spika na Waheshimiwa Wajumbe nataka niwahakikishie sana sana kwamba serikali yetu siku zote imekuwa mstari wa mbele kupambana na rushwa na ubadhilifu. Mhe. Spika, hii sio kazi nyepesi sana ni kazi ngumu lakini tunaifanya kwa bidii zote, licha ya kuweka taratibu za kisheria, taratibu za kitaasisi, lakini hata huu mpango tuliokuja nao wa *programme based budget* nao vile vile, ni sehemu moja ya kupambana na ubadhilifu katika utendaji wa shughuli za serikali.

Mhe. Spika, maana katika mpango huu kila kitu kipo bayana Waheshimiwa mnakiona wazi, kila programu iko wazi, *sub-programme* ipo wazi na semina ile iliwaelewasha kinaga ubaga, maana yake hakuna la kuficha mambo yako wazi, kila mmoja anajua hali yetu. Buku letu sio tu wataliona Waheshimiwa Wajumbe na wananchi wote wataliona, kwa hivyo, mtu yeyote ana haki ya kujua kilichopatikana na kilichotumika na nani kakitumia. Hizi zote jitihada za serikali kwa kusikiliza maoni yenu kwa kupambana na ubadhilifu na rushwa ndani ya serikali na nje ya serikali. Tunasema wazi wale wote wenye mitindo ya ubadhilifu, wenye mitindo ya rushwa wakati umekisha, tutapambana nao kwa hali yoyote.

Mhe. Subeit Khamis, alisema sana kwamba sisi viongozi tuliyokuwemo humu ndani tuwe mfano bora, tuwe kiyoo wa usafi, sisi isiwe miongoni mwetu tunakwenda kinyume na hayo. Tuwe ni viongozi tusiopenda hata kuisogelea rushwa au ubadhilifu wa aina yoyote. Napenda kuwashukuru viongozi kwa mifano yenu na inaonekana safi hivyo ndiyo ilivyo Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ni kiyoo. Mhe. Muhamedraza Hassanali, naye vile vile alilizungumzia sana jambo hili ni lazima tupambane na rushwa kwa kila hali. Nakubaliana sana Mhe. Raza na ushauri wako na tutazidi kuendelea kuufanyia kazi.

Lakini hapa hapa lilizungumziwa suala la vyeti feki vya kuzaliwa, nasema wazi mtu yeyote takaekamatwa na vyeti feki hatuwa kali za kisheria zitachukuliwa, tumeliagiza jeshi la polisi kufanya kila jitihada kutafuta kila namna wale wanaohusika na watengenezaji huu ama kwa njia moja au nyengine wanafanya mbinu za kuwezesha kupatikana vyeti feki wafanye kazi hiyo kwa mujibu wa taratibu za kisheria na wahusika wote hakuna atakaesamehewa wala atakaevumiliwa hatu kali zitachukuliwa. Naomba niwanasihi wananchi wote wasikubali kutumia vyeti feki maana mwisho wake wataingia katika matatizo.

Mhe. Spika, kuhusu maafa, suala la maafa kwa kiasi kikubwa Mhe. Makama wa Pili wa Rais atakuja kulieleza lakini na mimi nilieleze kwa ufupi sana. Chanzo cha maafa yetu hapa Zanzibar hasa yanayotokea wakati wa mvua za masika, ukitizama kwa kiasi kikubwa ni yale ya Waheshimiwa Wajumbe mliyoyasema.

1) Ni kujenga kiholela mabondeni,
2) Kujenga katika njia za maji,
3) Kutia taka katika mitaro yetu, na
4) Wale watu waokwenda kuiba ile mifuniko ya makaro na mitaro ina sababisha badala ya kupita maji ipite na taka pamoja.

Hayo yote ndiyo yanayosababisha kutuwama kwa maji na inakuwa chanzo kikubwa cha mashimo na ndio asili ya kukaa kwa maji na kusababisha nyumba zetu kubomoka. Kwa hivyo, jambo kubwa hapa na suala la msingi katisa ni kuwacha kujenga katika njia zetu za maji, kuacha kujenga mabondeni, kuacha kutia taka katika mitaro yetu na nikuacha kuiba mifuniko ya makaro na tukahakikisha kwamba yale makaro yanafunikwa yanabaki kama yalivyo salama. Tukifanya hivyo kwa kiasi kikubwa sana itasaidia kuepukana na madhara ambayo yanatokea.

Sasa limekuja shauri alilizungumzia sana Mhe. Viwe  la kwamba kwa nini hawa walioathirika na matatizo haya wasipewe viwanja mahala pengine. Wacha tuupokee ushauri, tuupeleke serikalini, ufikiriwe kwa sababu ni jambo linalohitaji tafakuri ya kutosha. Lakini ushauri sio mbaya ni ushauri mzuri wacha tuone namna gani serikali italifikiria jambo hili na halafu tutalitolea majibu yaliyo sahihi.

Kuhusu kwa nini Mfuko wa Maafa bado haujaanzishwa. Mhe. Spika, sasa mfuko wa Maafa uko tayari, tokea kufanya mabadiliko haya ya sheria kuhusu masuala ya mambo ya kukabiliana na maafa sasa Mfuko wa Maafa upo tayari rasmi na kwa bahati nzuri sana serikali imeweka utaratibu mzuri wa namna gani mfuko huu utapata fedha zake. Utapata katika asilimia 25 ya ile asilimia 100 iliyotengwa katika mfuko wa miundombinu; asilimia 75 utakwenda kwenye mambo ya miundombinu asilimia 25 tutagawana sisi wenye mifuko mbali mbali.
Utaratibu huo utafanywa na Wizara ya Fedha vizuri. Mfuko wa Mazingira utapewa chake, Mfuko wa Maafa utapata chake na Mifuko mengine itapata chake kwa utaratibu mzuri. Kwa hiyo, naamini kwenye utaratibu huu itasaidia sana Mfuko wetu wa Maafa kuwa na nguvu zaidi ya kukabiliana na maafa na sisi tunaosimamia mambo haya  kuweza kutoa huduma bora zaidi.

Lakini serikali imejipanga zaidi katika kukabiliana na maafa, licha ya kuanzisha na Kamisheni kutoka Idara, kama nilivyosema sasa mfuko utakuwa *active,* lakini pia tumeanzisha mpango wa mawasiliano ya kukabiliana na maafa, tumeanzisha mkakati ya kukabiliana na maafa, tumeanzisha Kamati mbali mbali zinazoanzia katika shehia mpaka Taifa. Zote hizi nia na madhumuni ni kukabiliana na maafa.

Bahati nzuri katika suala la uwokozi hivi karibuni serikali imeamua kuwa na mpango maalum wa kuimarisha usalama katika mji wa Zanzibar. Katika bajeti yetu

hiyo mtaona kuna shilingi bilioni 10 zimetengwa kwa ajili ya kazi hiyo. Sasa katika eneo hilo pia kuna *component* ya magari ya kuzimia moto, kuna *component* ya boti hizi za kuokolea na mambo mengine muhimu ambayo yatasaidia sana katika kukabiliana na masuala ya maafa. Kwa hiyo, kwanza nataka niipongeze serikali na wizara inayosimamia Tawala za Mikoa kwa kuja mradi huu ambao kwa kiasi kikubwa utasaidia katika kupambana na masuala ya maafa.

Vile vile na wenzetu wa *UNICEF* wamekuwa wakitusaidia sana katika jitihada za kuboresha mfuko wa maafa licha ya bajeti tunayopewa na SMZ, lakini *UNICEF* na wao wamechukua hatua kubwa sana ya kutusaidia.

Mhe. Spika, hivi sasa pia tumo katika mpango wa maandalizi wa kujenga vile vituo vya uwokozi. Tumesama tutajenga vituo vya uwokozi vitano Unguja na Pemba ambacho kimoja kitakuwepo Chake Chake, chengine Mkoani, Nungwi, Fumba, na hapa Malindi mjini. Msingi wake ni kwamba tutakuwa karibu zaidi vituo hivi na pale maeneo ambayo yanatokea ajali. Yote haya ni jitihada za serikali katika kuimarisha uwezo wa kukabiliana na maafa. Naamini kwa kufanya hivi kutasaidia sana.

Mhe. Spika, vile vile, tuliulizwa bwawa la Mwanakwerekwe. Nataka niseme licha ya suala la bwawa la Mwanakwerekwe, kwa ufupi serikali imeona umuhimu wa kuunda Kamati maalum ya Wataalamu itakayotizama kadhia nzima iliyojitokeza ya maafa ili kuona chanzo chake na hatua gani zichukuliwe katika kukabiliana na maafa katika maeneo mbali mbali ya nchi yetu. Kwa hivyo, naomba ndugu Wajumbe tuendelee kuvuta subra wakati Kamati yetu hii ya Wataalamu ikifanya kazi hiyo ili ije na mpango kabambe utakaosaidia kukabiliana na maafa katika nchi yetu. Naamini wataalamu hao watakuja na majibu sahihi ya kuepukana na matatizo yaliyotokea.

Mhe. Spika, katika hili pia lilizungumziwa kwamba na ajali za barabarai ni sehemu ya maafa. Nataka niwahakikishie Wajumbe wa Baraza hili kwamba tutaendelea kushirikiana na ndugu zetu wa polisi katika kuhakikisha kwamba tunaimarisha jitihada za utekelezaji wa Sheria za Usalama Barabarani, ili kuepusha wale wanaovunja sheria na wakasababisha ajali ambayo kwa kiasi kikubwa huwa wanapoteza maisha ya wananchi wetu na wakati mwengine kutoa aina mbali mbali ya majeraha ama maumivu. Kwa hiyo, kwa njia moja au nyengine Mhe. Spika, tutafanya kila jitihada kushirikiana na wenzetu wa polisi ili sheria ya usalama barabarani izidi kutekelezwa kwa nia ya kunusuru ajali ambazo zinatokea sana barabarani.

Mhe. Spika, nataka nimshukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa namna alivyolielezea suala zima linalohusiana na masuala ya

kuimarisha mazingira, hususan katika maeneo ya Kisiwapanza na Mjini Zanzibar, yale ndio mtazamo wa serikali. Kwa upande wetu kwenye suala la Kisiwapanza kupitia mradi wetu wa *TASAF* tuna dhamira ya kusaidia wananchi wa Kisiwapanza. Kwa sababu chanzo kikubwa kama alivyosema Mhe. Waziri hapa ni kukatwa kwa mikoko. Kwa hivyo, uwamuzi ni kwamba kupitia mradi wetu wa *TASAF* utasababisha kuwasaidia wananchi pale waweze kupanda mikoko upya ili kunusu Kisiwa chetu cha Kisiwapanza kisiendelee kupata mmong'onyoko. Kwa hiyo, nakubaliana sana na ushauri wa Mhe. Waziri ili tuweze kukabiliana na hali hiyo twende pamoja.

Mhe. Spika, yamezungumzwa mengi katika mambo mtambuka. Kwa hivyo, nataka nichukue fursa hii, moja lilikuwa linahusu mambo ya Afya. Kwa njia moja au nyengine nataka niseme wazi kwamba Mhe. Naibu Waziri wa Afya ameyaeleza mambo haya kinaga ubaga, kwa kina, vizuri na kwa ufasaha, Mhe. Mahmoud Thabit Kombo, hotengera sana kwa namna ambavyo umeeleza masuala yale.

Lakini pia nimshukuru na kumpongeza sana ndugu yangu Mhe. Naibu Waziri wa Elimu, Mhe. Zahra Ali Hamad, yeye naye alieleza vizuri masuala ya Wizara ya Elimu, sote tumeridhika namna alivyotoa maelezo yake.

Lakini pia nimshukuru rafiki yangu wa siku nyingi Mhe. Waziri wa Fedha, ameeleza mambo kwa ufasaha mkubwa, naamini wajumbe wameridhika na maelezo yake. Kwa hivyo, yale mambo yalikuwa yanagusa Wizara ya Fedha, yanaliyogusa elimu, yanayogusa afya, sina haja ya kuyarudia kuyatolea maelezo bali niunge mkono maelezo ambayo Waheshimiwa Mawaziri wameyaeleza kwa ufasaha mkuwa sana.

Mhe. Spika, kuhusu suala la polisi jamii, Mhe. Mshimba hili ni jambo lake la muda mrefu, kila mara jambo hili ni lazima alikumbushie na ni haki Mheshimiwa kulikumbushia. Nataka nikuhakikishie tu Mhe. Mshimba, kwamba Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inaunga mkono sana jitihada za polisi jamii na tupo na wenzetu wa polisi kwa karibu sana kuhusu kuimarisha suala la polisi jamii.

Mhe. Spika, nataka niseme kwamba tumekuwa na lugha hapa kwamba kuondoka kwa Kamishna Mussa ameondoka na Polisi Jamii. Nataka niseme kwanza Kamishna Mussa hakuondoka, Kamishna Mussa amepata uhamisho kwenda kufanya shughuli kubwa zaidi kwa Tanzania nzima. Sasa yeye ndiye anayesimamia Polisi Jamii Tanzania nzima, kwa hivyo, ikiimarika Zanzibar ijue ni kamishna Mussa na ikishuka Zanzibar ujue tena Kamishna Mussa. Kwa hiyo, tunashikiriana naye vizuri katika suala zima la kuimarisha Polisi Jamii. Hivi sasa utaratibu wa polisi kwenye suala hili licha ya kuwa na polisi yule wa shehia

wameamua kuwa na mkaguzi wa polisi katika jimbo na atakuwa na *taskforce* yake, yote haya ni utaratibu wa kuimarisha Polisi Jamii.

Mhe. Spika, lengo kubwa la Jeshi la Polisi ya kuleta maboresho ndani ya Jeshi la Polisi ilikuwa ni mambo matatu makubwa; Moja ni suala la weledi, jengine usasa, *modernization* ndani ya polisi, lakini jengine ni suala la Polisi Jamii. Kwa hiyo, ile polisi yenyewe imesimama katika mafiga matatu hayo niliyoyataja, kwa hivyo, kwa njia moja au nyengine msingi wa kuimarisha Polisi Jamii utaendelezwa, utaheshimiwa na utakuwa na mashirikiano makubwa kati ya serikali na wananchi wetu.

Tatizo letu mnalijua nyote, tatizo letu ni hali halisi ya uwezo wetu kiuchumi, hali yetu itakapotengemaa na kadiri tutakapopata uwezo tutashirikiana na ndugu zetu hawa wa Polisi Jamii kuwasaidia kwa hali na mali, maana ni wajibu wa serikali, ni wajibu wa Jeshi la Polisi kufanya kazi hiyo ili twende sambamba kwa nia ya kuweka nchi yetu katika hali ya amani na salama. Kwa hiyo, jitihada zinazochukuliwa ni nzuri na naomba niwatoe wasiwasi mafaniko yatakuwepo kwenye eneo hili.

Kuhusiana na nyumba za polisi, kama nilivyosema katika eneo la usasa ni pamoja na ujenzi wa nyumba za askari wa polisi pamoja na vituo vya polisi. Hivi sasa ndugu zetu wa Jeshi la Polisi wamechukua hatua kubwa sana katika suala la ujenzi katika Wilaya ya Wete Pemba, Chake Chake, Micheweni, Konde, Ziwani, Jambiani, Mbweni hapa tulipo, Jozani, Tunguu na Bububu; zote hizo kuna mahala ambapo ujenzi unaendelea ama ujenzi umemalizika ama matayarisho ya ujenzi katika maeneo hayo yanafanyika.

Kwa hivyo, kwa njia moja au nyengine hatuwezi kuona mabadiliko ya ujenzi mara moja kutokana na hali halisi ya uwezo wa kibajeti, lakini kadiri bajeti itavyoruhusu ujenzi wa kuimarisha nyumba za polisi, kuimarisha vituo vya polisi na kuliimarisha Jeshi lenyewe la Polisi kuwa la kisasa zaidi, ndio lengo na madhumuni ya serikali. Waheshimiwa Wajumbe, hivyo naomba sana mupokee hayo maelezo kwa upande huo wa polisi.

Mhe. Spika, katika maeneo mengine juu ya suala hili mtambuka lilizungumziwa suala la mapato ya tafiti zinazofanywa nchini. Je, makusanyo yake mbona hayaonekani? Kwa kuwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ni kweli ndio inayopokea maombi mwanzo kwenye suala la kufanya utafiti nchini, lakini maombi yote haya baadae hupelekwa kwa Mtakwimu Mkuu na yeye ndiye anayetoa kibali cha mwisho cha kufanya utafiti nchini.

Kwa hivyo, na malipo yote ya tafiti yanakwenda katika utaratibu huo kwa Mtakwimu Mkuu, ikija bajeti ya Wizara ya Nchi, (OR), Ikulu na Utawala Bora mtaona namna gani mapato haya yanavyokusanywa. Sasa naomba tuondoe wasiwasi kwamba kila jambo linafuata utaratibu na kama tulivyosema msingi wetu mkubwa kila penye eneo la mapato ya serikali lazima tuhakikishe mapato haya yanapatikana. Mhe. Waziri wa Fedha, alieleza haya kwa kina sana.

Mhe. Spika, vile vile, ulikuja ushauri kwa nini tusifunge skuli. Kwenye masuala ya maafa yana hatua mbali mbali, pale itakapotokea hatua ya kufikia kwamba mvua hizo tunaona sasa zitaleta athari kubwa basi uamuzi huo unafikiwa bila ya tatizo lolote, lakini pale ambapo tunaona hakuna athari ambayo inaweza kupatikana kufikia kufungwa kwa skuli tunaendelea kustahamili na sana sana hili kutegemea na ushauri wa Mamlaka ya Hali ya Hewa kanda ya Zanzibar; wakiona kuna jambo ambalo wao watushauli kwenye suala hili tunafuata ushauri huo ili kunusuru usalama wa watoto wetu na wananchi kwa jumla.

Kuhusu *DNA* nina hakika Mhe. Mahmoud Mohammed, ameelezea vizuri, lakini nataka niseme kwamba kipimo hiki hasa kinatakiwa kiwe chini ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Kwa hiyo, tutawasiliana na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ili suala la *DNA* lipate ufumbuzi ili wale ambao wanafanya vitendo viovu vya kuwababaka watoto wetu au kwenda kinyume na mambo ambayo hayaruhusiwi, basi mashine hii iwepo na hatua za kisheria ziweze kuchukua mkondo wake.

Kuhusu makaazi ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Nataka niwahakikishie Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba tayari tumefanya matengenezo makubwa katika nyumba yake anayoishi hapa Zanzibar ambayo ilipata hitilafu ya moto, hivi sasa tuko katika hatua za mwisho nyumba ile kuwa tayari iweze kukalika upya. Halikadhalika na nyumba ya Dar es Salaam tumechukua hatua ya kuifanyia matengenezo makubwa na muda si mrefu Mhe. Makamu wa Pili wa Rais pia atapata nafasi ya kuendelea kuishi katika makaazi yake ya pale Dar es Salaam.

Kwa upande wa Makamu wa Kwanza wa Rais, Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, atapokuja hapa ataeleza jitihada gani wanazozichukua katika kushughulikia makaazi ya Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais.

Kiwanda cha Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali, wengi walielezea suala la kiwanda hiki kiweze kujiendesha kibiashara na kwa nini hakikuweza kufikia lengo la mwaka jana.

Mhe. Spika, nia na madhumuni ya serikali ni kukifanya kiwanda kijiendeshe kibiashara. Hivi sasa wizarani kwetu tumemaliza hatua mbali mbali ikiwemo

kutengeneza *business plan* ya kiwanda hicho, mpango kazi wa kiwanda hicho na hata rasimu ya sheria ya kukifanya kiwanda hicho kijiendeshe kibiashara imekamilika na sasa itakwenda katika *process* ya kiserikali na mara itakapomalizika *Inshaallah* tutaileta katika Baraza letu tukufu hapa ili muipitishe na sasa kiwanda kiwe na mamlaka nzuri ambayo itaweza kukiwezesha kiweze kufanya shughuli zake kibiashara na pale kitakuwa sasa kina uwezo mzuri zaidi wa kukusanya mapato na kutekeleza wajibu wake vizuri.

Kwa kuwa mwaka jana tulikuwa wapya wateja wetu walikuwa hawajatufahamu vizuri kwa vyovyote hatukuweza kufikia lengo, lakini naamini mwaka huu wa fedha lengo litafikiwa ama hata kuvukwa. Kwa hiyo, naomba muendelee kushirikiana nasi katika kuhakikisha kwamba tunaweza kufanikisha lengo letu hili.

Kuhusu Bohari Kuu, katika mpango huu wa kufanya mabadiliko ya kiwanda kukifanya kijiendeshe kibiashara pia kuna mpango wa kuanzisha Bohari Kuu na tayari serikali jambo hili limeshatupa baraka zake ili tuweze kuendelea na kuanzisha Bohari Kuu hapa nchini kwetu kama ilivyokuwa siku za nyuma.

Mhe. Spika, kwa upande wa Baraza la Wawakilishi. Upande wa Baraza mengi yalizungumzwa ikiwemo suala zima la kuwataka Waheshimiwa Wajumbe wapate safari za kwenda nje ya nchi hasa kamati zetu za kudumu.

Mhe. Spika, jambo hili kwa upande wetu tunaliunga mkono sana, tunaelewa umuhimu wa Wajumbe wetu kwenda kupata mafunzo nje ya nchi, kwenda kubadilishana uzoefu na wenzao nje ya nchi, lakini yote haya yanategemea hali halisi ya uwezo tulioano. Kile ambacho tunakipata ndicho ambacho Baraza linatengewa kama tunavyopata maeneo mengine ili ziweze kusaidia utendaji wa shughuli hizi za Baraza la Wawakilishi, pamoja na kusaidia zipatikane fursa za Wajumbe kwenda kujifunza nje ya nchi.

Kuhusu suala la marejesho ya *CDF*. Mhe. Spika, nataka niseme wazi kwamba mwanzoni tulisema ni majimbo manane tu yaliyoweza kufanya marejesho, lakini mpaka jana sasa ni majimbo 25 tayari yameweza kufanya marejesho na majimbo yaliyobaki Wajumbe tayari wamewasiliana na sisi saa yoyote kuanzia sasa marejesho yatakuwa yamefika ofisini. Kwa hiyo, nataka niwapongeze sana Wajumbe wa Baraza hili tukufu kwa jitihada mnazofanya kufanya marejesho ya majimbo na *Inshaallah* na sisi tutafanya kila jitihada kwa sababu naamini kabisa kwamba wananchi katika maeneo yao, katika majimbo yao wanahitaji mpango huu wa serikali wa kusaidiwa katika kuendeleza miradi mbali mbali ya wananchi katika maeneo yao. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Waziri wa Fedha, ameshaniahidi sana na ameshanihakikishia kwamba jambo hili litafanyika haraka iwezekanavyo, kwa hivyo, Wajumbe hapa Mwenyezi Mungu akitujaalia uhai mambo yatakwenda vizuri kwa nia ile ile ya kuwahudumia wananchi wetu.
Kuhusu umiliki wa ukumbi wa zamani wa Baraza la Wawakilishi leo asubuhi nilipojibu swali hili nafikiri tayari nimeshalieleza vizuri. Kuhusu kutengeneza ndio dhamira na nia ya serikali kuutengeneza ukumbi ule uweze kubaki vizuri uwe na haiba na hadhi lakini pia uweze kuingiza mapato.

Mhe. Omar Ali Shehe, alizungumzia suala la kupungua kwa bajeti yetu. Mhe. Spika, kihesabu bajeti yetu haijapungua ya Baraza la Wawakilishi, lakini inawezekana kimahitaji bajeti yetu ikawa haikidhi yale mahitaji ambayo tunayahitaji yawepo, lakini kwa kiasi fulani katika taasisi ambayo serikali inatoa kipaumbele sana moja ni Baraza letu la Wawakilishi maana inajua bila ya kuwepo bajeti shuguli za Baraza zinaweza kukwama.

Mhe. Spika, kwa kutoa taarifa ya haraka haraka tu katika mwaka 2013/2014 bajeti ya Baraza letu ilikuwa shilingi 12.3 bilioni; mwaka 2014/2015 ilikuwa shilingi 14.8 bilioni; lakini mwaka 2015/2016 ni shilingi 16.7 bilioni. Kwa hiyo, kwa vyovyote vile kimahesabu bajeti yetu haikupungua lakini kimahitaji na shughuli zinavyokuwa, twabaan inaweza kuwa kwamba juu ya bajeti tunayopewa haiwezi kukidhi mahitaji yote ambayo tungetaka yafanyike.

Lakini kutokana na hali halisi ya uchumi hivyo ndivyo ilivyowezekana na naamini Wajumbe mtaendelea kuridhika kwa sababu kadiri ya uwezo wetu Baraza linawezeshwa ili liweze kuendesha shughuli zake kwa kuheshimu ule utawala wa kugawana mamlaka, kwa maana ya Baraza na mamlaka yake, Serikali na mamlaka yake na Mahakama na mamlaka yake. Kwa hiyo, nia yetu ni njema Baraza liweze kufanya vizuri na kutekeleza wajibu wake.

Kuhusu ziara ya mafunzo India ya Kamati ya *PAC* ni kweli kabisa Wajumbe wetu walitaka wapate mafunzo zaidi kule India, maombi yao yalipelekwa kupitia Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, lakini tuliwaomba wenzetu Ubalozi wa India kwa bahati mpaka sasa hatujapata majibu ambayo yangewawezesha Wajumbe wetu kwenda. Nia na dhamira tutaendelea kuwakumbushia wenzetu ili waone umuhimu wa Wajumbe wetu nwa *PAC* waweze kwenda kule. Tulianza vizuri sijui kitu gani hapo katikati kimesababisha kuchelewa jambo hili, lakini nitazidi kufuatilia tuone ni nini hasa sababu kwa nini mpaka sasa majibu bado. Lakini hatuwezi kuwalazimisha wenzetu ambao wana nia njema ya kutusaidia.

Kuhusu Sheria ya Utawala wa Baraza. Mhe. Rais wetu alishatoa agizo zamani la kusema kwamba Baraza la Wawakilishi na serikali ikae mlipatie ufumbuzi suala

hili na suala la Sheria ya Utawala wa Baraza iendelee na ifanye kazi yake. Naamini kwa mazungumzo yetu yanavyokwenda tutafikia muwafaka wa jambo hili na Sheria ya Utawala wa Baraza iweze kuwepo na iweze kufanya kazi kwa Baraza letu tukufu.

Kuhusu programu ambazo zimewekwa kwa Baraza la Wawakilishi kwa sasa, naamini ushauri wa Mhe. Omar Ali Shehe, kwamba bado kuwe na programu nyingi katika programu zetu hizi ni ushauri mzuri, tutakaa na wenzetu tuone ni vipi tutautekeleza ushauri huu wa kushauriana na wenzetu wa Wizara ya Fedha, jambo lolote ambalo litaleta manufaa zaidi ni jambo ambalo siku zote linaheshimiwa na kupokelewa.

Kuhusu uvujaji wa paa la jengo letu la Baraza hili. Hatua zinachukuliwa za kukarabati paa hili, lakini hatuwezi kukarabati sasa kwa ushauri tuliopewa, tumetakiwa tukarabati baada ya mvua. Kwa sababu kuna dawa fulani wanaita faiba hawa wataalamu itahitajika na haiendani na wakati wa mvua inataka wakati wa jua na kwa hali inavyojitokeza hivi si muda mrefu pengine jua tutalipata na baada ya kuakhirisha Baraza letu naamini shughuli za utengenezaji zitakuwepo.

Vile vile, suala la mchwa dawa za mchwa zipo hatua zinaanza kuchukuliwa ili kuua mchwa katika Baraza letu. Nia ni kulifanya Baraza letu liwe la kisasa na linalokidhi viwango.

Kuhusu suala la *Hansard,* ushauri tunaupokea ili tukiimarishe zaidi kitengo chetu cha *Hansard* kiweze kutoa huduma bora zaidi.

Mhe. Spika, kwa upande wa *echo,* hatua mbali mbali zimepitwa katika kulitafutia ufumbuzi suala hili, naamini tutafika mwisho wa kulipatia ufumbuzi suala hili. Lina *challenges* zake lakini bila shaka yoyote tutafikia uamuzi ulio mzuri tuweze kupata ufumbuzi wa suala la *echo* la Baraza letu ili tuweze kusikilizana vizuri.
Mhe. Spika, kwa kuwa mengi ambayo yamezungumzwa hapa nimejaribu kuyatolea ufafanuzi na kwa kuwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, atakuja kutoa ufafanuzi zaidi katika masuala mbali mbali, mengine ambayo nimeyaachia mimi na yale ambayo yeye ataona ayatolee ufafanuzi zaidi kwa sababu yeye hasa ndiye mwenye wizara hii.

Kwa hivyo, naamini haya maelezo yangu mafupi niliyoyatoa hapa yatatosheleza sana kwa Waheshimiwa Wajumbe kuyaelewa na kuyafahamu na kutupitishia bajeti yetu. Kwa sababu kama mnavyojua Waheshimiwa huu ni mwaka wa lala salama basi hata sasa hivi tena mkitaka kunilaza njiani itakuwa kidogo mambo yatakuwa magumu zaidi. Kwa hivyo, nawaomba kwa heshima na taadhima zote Mhe. Spika, Wajumbe wako hawa waiunge mkono bajeti yetu na mimi naiunga mkono bajeti

hii kwa asilimia mia moja. Nawaomba wenzetu wote hawa waiunge mkono na waipitishe ili tuweze kutoa huduma nzuri kwa wananchi wetu, naamini kabisa kwamba tuko tayari kutekeleza yale yote ambayo Waheshimiwa Wajumbe watatuagiza.

Mhe. Spika, ahsante sana nakushukuru. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Mhe. Waziri, tunakushukuru sana kwa kumuwekea njia safi Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ili yeye aje amalizie. Nichukue nafasi hii basi kumkaribisha Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, ili kumalizia majumuisho. Karibu. *(Makofi)*

**Mhe. Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, na mimi nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii kuja kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya mambo yaliyowasilishwa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu. Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako pamoja na Waheshimiwa Mawaziri kwa kuichangia hotuba ya ofisi yangu ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ambapo jumla ya Wajumbe 30 wamechangia hotuba hii, kati ya hao Wajumbe 29 wamechangia kwa kusema na Mjumbe mmoja amechangia kwa maandishi.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kuwatambua Wahehsimiwa hao waliochangia kwa kusema na waliochangia kwa maandishi. Waliochangia kwa kusema ni:

1. Mhe. Hamza Hassan Juma, Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Kwamtipura ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

2. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
3. Mhe. Asaa Othman Hamad
4. Mhe. Shadya Mohammed Suleiman
5. Mhe. Abdi Mosi Kombo
6. Mhe. Subeit Khamis Faki
7. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa
8. Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohamedali
9. Mhe. Marina Joel Thomas
10. Mhe. Fatma Mbarouk Said
11. Mhe. Panya Ali Abdalla
12. Mhe. Omar Ali Shehe
13. Mhe. Mgeni Hassan Juma
14. Mhe. Ali Salum Haji

15. Mhe. Mohammed Mbwana Hamad
16. Mhe. Wanu Hafidh Ameir
17. Mhe. Hassan Hamad Omar
18. Mhe. Mohammed Haji Khalid
19. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
20 Mhe. Bikame Yussuf Hamad
21. Mhe. Viwe Khamis Abdalla
22. Mhe. Nassor Salum Ali
23. Mhe. Suleiman Hemed Khami - Kwa maaandishi
24. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
25. Mhe. Naibu Waziri wa Afya
26. Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais
27. Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali
28. Mhe. Waziri wa Fedha
29. Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais

Mhe. Spika, ninathamini sana michango na mapendekezo iliyotolewa ambayo ninaamini kabisa itasaidia sana katika kufanikisha utekelezaji wa malengo tuliyojiwekea. Aidha, naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe, kwamba Serikali itazingatia mapendekezo na michango hiyo kwa manufaa ya wananchi na taifa kwa jumla. (*Makofi*)

Michango yao itasaidia sana Ofisi yangu ambayo itafanikisha shughuli mbali mbali katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Pia, nawaomba niwashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri kwa kutoa ufafanuzi wa hoja mbali mbali zilizohusu sekta zao.(*Makofi*)

Mhe. Spika, naomba nimshukuru sana kwa namna ya pekee Mhe. Mohammed Aboud Mohammed, ambaye ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kutoa ufafanuzi wa hoja nyingi zilizowasilishwa na Wajumbe wa Baraza lako Tukufu katika kujadili hotuba ya bajeti ya Ofisi yangu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, mengi yaliyozungumzwa ameyatolea ufafanuzi Mhe. Mohammed Aboud Mohammed, mimi nitajikita katika mambo machache sana. Kwanza ningependa kuwashukuru Wajumbe wote wa Baraza hili kwa namna walivyozungumzia suala zima la amani na utulivu wa nchi yetu. (*Makofi*)

Kila mmoja hapa ameona thamani ya amani na utulivu wa nchi na kila mmoja amezungumzia hoja hii ya amani na utulivu. Katika hotuba yangu nilipofunga semina yetu kule *Zanzibar Ocean Hotel* Chuini, nilisema maneno haya;

"Kukua kwa uchumi wetu kutategemea pia uchaguzi wetu mkuu wa mwezi wa Oktoba mwaka huu kama utakwenda kwa amani na utulivu. Serikali kwa upande wake itahakikisha Tume ya Uchaguzi inaendesha uchaguzi wenye uwazi na haki kwa wagombea wote watakaobahatika kushiriki kwenye uchaguzi huu."

Kwa upande wetu wanasiasa ni vyema tukajiepusha na kauli za kuchochea fujo. Kwa upande wa wananchi ni vyema kutokubali kuchochewa kuanzisha vurugu na kwa upande wa vyombo vya habari ni vyema kufanya kazi zao kwa uadilifu. Uchaguzi ulio salama utakuwa kichocheo kimoja wapo kikubwa cha kusaidia kukua kwa uchumi wetu, kwani wawekezaji wengi zaidi wanatamiminika kuja kuweka nchini mwetu.

Aidha, kwa upande wa utalii nchi yetu itapata watalii wengi zaidi na hivyo kuongeza ajira kwa wananchi wetu pamoja na kukuza pato letu. Utaona nimehusisha wananchi, nimehusisha wanasiasa na waandishi wa habari, kwa sababu wote hawa ni wadau wa amani na utulivu wa nchi yetu. (*Makofi*)

Sote hapa ni wadau, amani na utulivu ikivurugika ikipotea mimi, wewe, baba, mama, mke na watoto wote waathirika. Kwa hivyo, ni wajibu wetu sote kuhakikisha kwamba amani na utulivu unaendelea kuwepo nchini mwetu. (*Makofi*)

Wajumbe waliochangia wamegusia suala hili la kudumisha amani na utulivu, na hasa tukielekea katika kipindi cha kura ya maoni na uchaguzi wa Oktoba wa 2015. Ninapenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wajumbe na wananchi wote kwa ujumla kwamba Serikali kupitia vyombo vyake vya ulinzi na usalama vitaendelea kusimamia na kuimarisha usalama wa wananchi na mali zao katika kipindi chote.

Pia, ninapenda kuchukua nafasi hii kuwanasihi wananchi kushirikiana na Serikali yao katika kudumisha amani tuliyonayo na usikubali kushawishiwa kwa njia yoyote ile na wanapoona kuwa kuna dalili za uvunjifu wa amani katika maeneo yao, kutoa taarifa kwa viongozi wao wa maeneo au vituo vya polisi vilivyo katika maeneo yao.

Vile vile, nawaomba viongozi wa dini kutumia nafasi zao kuzidi kuhubiri amani na mshikamano miongoni mwa waumini wao na wananchi kwa ujumla. Ninaamini kwamba viongozi hao wana ushawishi mkubwa na nafasi kubwa kwa jamii.

Mhe. Spika, kwa umuhimu wake ninapenda kuwanasihi viongozi wenzangu wa siasa kuyatumia vyema majukwa yao katika kuhubiri amani, utulivu na mshikamano bila ya kuzingatia itikadi zao za kisiasa na kuacha uchochezi utakaopelekea taifa letu kutumbikia katika machafuko.

Wenzetu waliokosa amani wanaona hali ilivyo sasa, tunaona katika vyombo vya habari yanayotokea Iraq, Syria, Libya, yote haya yanatokea kwa sababu ya ukosefu wa amani. Tanzania katika Afrika ndiyo pekee kinachoitwa kisiwa cha amani. Wenzetu wengi waliopata matatizo katika nchi zao wamekimbilia Tanzania. Zanzibar ni kisiwa, likitokea tatizo hapa tutakimbilia wapi. Kauli zetu wanasiasa na viongozi lazima ziwe za kukaribisha amani na siyo za kufukuza amani.

Mhe. Spika, Wajumbe wengi wamezungumzia suala zima la maafa kutokana na mvua kubwa za masika yaliyosababisha mafuriko. Mhe. Spika, tarehe 3 May, 2015 nchi yetu ilishuhudia kunyesha mvua kubwa za masika zilizofikia kiwango cha kiwango *millimetre 172.2* kwa muda wa masaa matatu mfululizo. Kiwango hicho hakijawahi kuripitiwa kwa kipindi cha miongo minne iliyopita. Kufuatia mvua hizo athari kubwa zilizojitokeza ikiwemo vifo vya watu watu, uharibifu wa nyumba na miundombinu ya barabara na upotevu wa mali za wananchi. Kiasi cha nyumba 1,424 zenye familia 1,819 katika Mkoa wa Mjini/Magharibi zimeathirika.

Serikali kupitia yake Kamati yake ya Kitaifa ya kukabiliana na maafa imesimamia upatikanaji wa huduma zote muhimu za kibinadamu ikiwemo kusimamia na kuratibu huduma za uokozi wa watu na mali zao. Utoaji wa huduma za chakula, malazi na afya.

Aidha, Serikali imefungua kituo maalum cha makaazi ya dharura ili kuwahifadhi wananchi wote ambao nyumba zao zimeathirika zaidi na kushindwa kuishi katika nyumba hizo. Kituo hicho kimefunguliwa katika Skuli ya Mwanakwerekwe "C" ambapo hadi kufikia tarehe 20 May, 2015 kilikuwa na watu 170. Wananchi hao watarudi maeneo yao mara tu baada ya nyumba zao kurudi katika hali ya kawaida.

Mhe. Spika, tunasikitishwa sana na kitendo hichi cha wananchi wetu kukaa katika nyumba zao yakija masika wanahama, yakimalizika masika wanarudi. Nimshukuru Mhe. Viwe Khamis Abdalla, kwa rai yake. Labda Serikali ingetafuta mahali maeneo wakapewa viwanja waathirika hawa ili wajenge nyumba katika maeneo salama.(*Makofi*)

Lakini ninataka nikumbushe yale yaliyotokea kule Dar es Salaam. Kuna sehemu ya Jangwani kila mara yakitokea mafuriko pale watu wanaathirika. Wakapewa maeneo ya kujenga, wakakabidhiwa na hati ili waondoke katika mabonde waende kujenga kwenye maeneo yale ambayo yapo salama. Badala yake wananchi wale wakayauza maeneo yale, wakarudi tena kule kule kwenye mabonde yao Jangwani.

Juzi mvua zilipokuja zimewakumba tena na Rais alipokwenda kuwakagua akawaambia kwamba sasa sikupeni msaada tena. Kwa sababu tulikutoeni hapa

tukakupeni viwanja mumeuza mumerudi tena hapa. Kwa hivyo, sisi tutakuwa tayari kufikiria wazo hili la Mhe. Viwe, hawa waathirika kuwatafutia maeneo. Tukifanikiwa kufanya hivyo, tunawasihi watakaobahatika kupata viwanja hivyo basi wajenge na wasiuze. Wanaweza kuviuza wakarudi tena kule kule ikawa adha ile ile kila wakati kila ikinyesha mvua. (*Makofi*)

Mhe. Spika, tumejaribu kutathmini ni kitu gani hasa kinachosababisha mafuriko haya kila mwaka. Hivyo, Serikali imeunda Kamati ya Wataalamu kutoka sekta mbali mbali iliyopewa kazi ya kufanya utafiti wa kina juu ya sababu za kujitokeza mafuriko ya mara kwa mara na kutoa mapendekezo ya hatua zinazopaswa kuchukuliwa ili kurekebisha hali hiyo. Ni imani yangu kwamba timu hiyo itafanya kazi zake kwa haraka na Serikali itayazingatia na kuyafanyia kazi mapendekezo yatakayotolewa na Kamati hiyo. Bila shaka tutaangalia nyumba zilimojengwa, njia za maji zilizozibwa, mabomba yaliyozibwa na baada ya hapo Serikali itachukua hatua zinazofaa.

Kuna Mjumbe ameulizia kuhusu suala la zima la abiria iliyonunuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Ninasema niwafahamishe Wajumbe kwamba kwa ujumla meli mpya iliyonunuliwa na Serikali tayari imeshakamilika matengenezo yake na itafanya majaribio ya kutembea baharini au *sea tried* tarehe 5 Juni, 2015. *(Makofi)*

Meli hiyo itaondoka Korea kuja Zanzibar tarehe 25 Juni, 2015 na itachukua wiki nne hadi kuwasili kwake kwa kutegemea hali ya bahari na mwenendo wa chombo. Kwa taarifa hiyo ina maana meli hii itafika Zanzibar mnamo mapema mwezi wa Julai. Kwa hivyo, meli hiyo imetengenezwa ipo njiani na siyo muda mrefu hapa itawasili nchini. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kuna mambo machache itabidi niyatolee vile vile ufafanuzi. Mhe. Omar Ali Shehe, ameeleza kwa masikitiko makubwa sana kwamba Serikali haikuwasilisha ripoti ya *CAG* ambayo uchunguzi wake uliagizwa na Mhe. Rais. Niseme tu ripoti hizi ni maalum alizoziagiza Mhe. Rais. Mhe. Rais ana hiyari zake halazimiki kuzileta Barazani, akipenda anaweza akazileta, hafungwi na Kanuni, hafungwi na Katiba. Kwa sababu uchunguzi huu umefanyika kutokana na matakwa yake, kutokana na sababu zake.

Sasa atakaporidhia basi ripoti hizo zitaletwa. Lakini Baraza vile vile lina mamlaka ya kumuomba *CAG* kufanya uchunguzi katika maeneo yote yale wanayoyaona yana hitilafu. Kwa hivyo, Baraza liwe huru na linaweza likafanya hivyo vile vile.

Mhe. Spika, Makame Mshimba Mbarouk, amezungumzia suala la maswali ya papo kwa papo kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Niseme tu sisi Kanuni haziruhusu,

lakini zitakaporuhusu sawa zitafanyika lakini haitosaidia sana Serikali, kwa sababu mimi siyo mtengenezaji wa mambo yote. Ninaweza kuamua kitu hapa Serikalini ikawa kigumu kutekelezeka. Kwa hivyo, ninafikiri tukaendelea na utaratibu wetu huu huu wa maswali ya kawaida na utaratibu wake wa kawaida.

Mhe. Mahmoud, ameulizia juu ya suala zima la Menai kunafanyika nini. Ni kweli Serikali bado hujui haijaelewa kinafanyika, haina habari kinachofanyika Menai. Tunajua kwamba Menai ni eneo lililo katika hifadhi. Nimshukuru sana Mhe. Mahmoud, kwa kutuletea taarifa hiyo, Serikali itachunguza na kuona kinachoendelea kule kinajengwa nini na hatua gani Serikali ichukue. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kama nilivyosema mengi yamejibiwa na Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, lakini niwashukuru tena Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa michango mingi mizuri ambayo ninaamini imetolewa kwa nia safi ya kuisaidia Serikali yetu kufanya kazi zake kwa ufanisi. (*Makofi*)

Kwa hivyo, kwa mara nyengine tena ninachukua nafasi hii kumshukuru tena Mhe. Waziri Mohammed Aboud Mohammed, Katibu Mkuu Dkt. Khalid, Naibu Katibu Mkuu Ndg. Ahmed Kassim Haji, Wakurugenzi na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kwa mashirikiano wanayonipa na ninaamini watakayoendelea kunipa ambayo yananiwezesha kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**Mhe. Spika:** Ahsante sana, Waheshimiwa Wajumbe nakushukuru sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa kukamilisha majumuisho na hatimaye kutoa hoja, sasa hoja hiyo basi tuiamue. Waheshimiwa Wajumbe niwahoji basi wale wanaokubaliana na hoja hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa Mwaka 2015/2016 wanyanyue mikono, wanaokataa waliokubali wameshinda. (*Makofi*)

*(Hoja imetolewa iamuliwe)*
*(Hoja imaamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili:** Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kukubali hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kupitisha vifungu vya matumizi vya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

**KAMATI YA MATUMIZI**

**FUNGU C01 - AFISI YA MAKAMO WA PILI WA RAIS**

Kifungu 04 Idara ya Sheria na Maadhimisho ya Kitaifa Sh. 12,360,000/=
Kifungu 06 Idara ya Upigaji Chapa na Mpigachapa Mkuu wa Serikali Sh. 600,000,000/=

**Jumla ya Fungu Sh. 612,360,000/=**

*(Vifungu vilivyotajwa hapa juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**FUNGU C01 - AFISI YA MAKAMO WA PILI WA RAIS**

Kifungu P01 Programu ya Uratibu wa Shughuli za Makamo wa Pili wa Rais
Kifungu (S01) Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Makamo wa Pili wa Rais Sh. 625,599,000/=

**Jumla ya Programu Sh. 625,599,000/=**

*(Vifungu vilivyotajwa hapa juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu P02 Programu ya Uratibu wa Shughuli za Serikali
Kifungu (S01) Programu Ndogo ya Kukabiliana na Maafa Sh. 405,775,000/=

Kifungu (S02) Programu Ndogo ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa Pamoja na Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa Sh. 987,260,000/=

Kifungu (S03) Programu Ndogo ya Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Sh. 846,692,000/=

**Jumla ya Programu Sh.2,339,727,000/=**

*(Vifungu vilivyotajwa hapa juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu P03 Programu ya Usimamizi wa Shughuli za Upigaji Chapa
Kifungu (S01) Programu Ndogo ya Usimamizi wa Shughuli za Upigaji Chapa Sh. 714,050,000/=

Kifungu P04 Mipango na Utawala

Kifungu (S01) Programu ndogo ya Uongozi na Utawala Sh. 780,741,000/=

Kifungu (S02) Programu Ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti...

**Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa:** Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia hapa nilitaka kujua nini mpango wa serikali juu ya suala zima wa yale mashirika ambayo ni ya Tanzania Bara ambayo ni ya Mawasiliano yanafanya kazi Zanzibar, kwa bahati mbaya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais alipokuja hapa nahisi alisahau kulizungumza hili. Naomba maelekezo zaidi kuhusiana na hilo.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa kweli Mhe. Mwakilishi Mhe. Mahmoud, alilizungumzia hilo, lakini kwa sababu nadhani jambo hili litakuwa linashughulikiwa na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano wao walikuwa wana uwelewa zaidi wa kulielezea hilo.

Hata hivyo, Mhe. Waziri wa Fedha katika kipindi cha muda mrefu kutokana na taratibu za Kanuni zetu jambo ambalo limezungumziwa hivi karibuni nafikiri tayari majibu yale ambayo Mhe. Waziri wa Fedha alikuwa akiyatolea ufafanuzi mara kwa mara kuhusu tukio hili, nadhani majibu yake yatakuwa ni kama alivyoyataka Mhe. Mahmoud Muhammed. Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi kwenye fungu langu sioni eneo ambalo naweza kuzungumzia hilo. Nashukuru.

**Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa:** Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri, lakini suala hili serikali ilitoa maelekezo katika Kitabu cha Bajeti cha mwaka 2013/14 na kutoa maelekezo kwamba suala hili watalifanyia kazi na kulishughulikia na baadae tutapata taarifa. Ndio maana nilipokuja sasa hivi nikaomba kupata maelekezo.

Je, serikali imejipangaje kuhusiana na suala hili ili tuweze kujua mustakbali, nini kitafanyika kwa hizi taasisi au haya mashirika ambayo yapo hapa ambayo yanaendelea na shughuli zake wakati Shirika letu la *ZANTEL* linalofanya kazi upande wa pili wa Muungano linaendelea kulipa baadhi ya *tax* ambazo wengine ambao wako hapa wao hawalipi na hili sio suala la muda mfupi ni suala la mwaka mzima kwa sasa.

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Mhe. Mwenyekiti, kuna mambo mawili hapa ambayo lazima Wajumbe tukubaliane. Jambo la kwanza tusiulize suali ambalo halipo kwenye programu ile itakuwa tunapoteza muda, tunakwenda na kurudi.

Hilo suala analoliuliza Mhe. Mwakilishi, kwanza halipo kwenye programu hii, asubiri programu inayohusika aje aliulize hilo suala atapata majibu. Kwa sababu

ndio kwanza tunaanza kusoma bajeti ya Makamu wa Pili wa Rais ipo bajeti ya Wizara ya Fedha, ipo bajeti ya Wizara ya Miundombinu, atafute kwenye programu gani katika bajeti hizo na vitabu anavyo aje atuuliza hapo. Lakini programu hiyo hapa haipo.

**Mhe. Spika:** Ni sawa labda pengine mngemsaidia Mjumbe kama serikali imesimamia haya, kwa sababu ilikwua ni ahadi ya serikali basi amelisimamia tutaendelea. Kimsingi hakuna nguvu kama unavyosema ya kuzuia fungu, lakini anataka maelezo yanayohusu mlisimamia vipi juu ya jambo hili.

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Mhe. Mwenyekiti, maswali yote ambayo ameuliza Mhe. Mwakilishi, majibu yake yapo na asubiri tutamjibu. Hayo anayouliza kuhusu habari ya *ZANTEL* na mashirika mengine ya simu utaratibu wake upo na tunaelewa kila kitu na anayeuliza chengine kuhusu habari ya *PAYE* maana yake ameyachanganya, mambo mengi kayachanganya kwa pamoja, tutamtolea ufafanuzi lakini na asubiri aidha aisubiri Wizara ya Fedha au aisubiri Wizara ya Miundombinu, hapo tutamtolea ufafanuzi, tutampa kila kitu. Lakini tuki-*entertain* kuuliza maswali katika maeneo ambayo hayahusiani tutapoteza muda wote. Hiyo Programu tuliyoikusudia itakuwa haiendi kabisa na utaratibu tunakwenda *PDB*, twendeni kwa utaratibu ambao tumefundishwa na watalamu, tusuri Wizara ya Fedha itakuja tarehe 29, Juni kuna Wizara ya Miundombinu aulize hapo tutamjibu, hayo yote masuala majibu yake yapo.

**Mhe. Spika:** Majibu yapo kuonesha kwamba serikali imesimamia hayo. Tuendelee.

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu (S02) | Programu Ndogo ya Mipango Sera na Utafiti | Sh. 271,792,000/= |
| Kifungu (S03) | Programu Ndogo ya Ofisi Kuu Pemba | Sh. 534,821,000/= |
| Kifungu P04 | Programu ya Mipango na Utawala | Sh. 1,487,354,000/= |
| | **Jumla Kuu** | **Sh. 5,166,700,000/=** |

*(Vifungu vilivyotajwa hapa juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**FUNGU CO2 - BARAZA LA WAWAKILISHI**

**Kifungu C02 - Programu ya Kutunga Sheria, Kupitisha Bajeti na kusimamia Taasisi za Serikali.**

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu (S01) | Programu ndogo ya Kutunga Sheria, Kupitisha Bajeti na Kusimamia Taasisi za Serikali | Sh. 6,539,295,000/= |

**Jumla ya Programu** **Sh. 6,539,295,000/=**

*(Vifungu vilivyotajwa hapa juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Kifungu P02 - Programu ya Uongozi wa Utawala wa Baraza la Wawakilishi**

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu (S01) | Uongozi na Utawala wa Baraza la Wawakilishi | Sh. 10,223,305,000/= |
| | **Jumla ya Programu** | **Sh. 16,762,600,000/=** |

*(Vifungu vilivyotajwa hapa juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**FUNGU C03 - TUME YA UCHAGUZI**

**Kifungu P02 - Programu ya Usimamizi wa Kazi za Utawala na Uendeshaji wa Shughuli za Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.**

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu (S01) | Usimamizi wa Kazi za Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Uchaguzi | Sh. 1,214,021,000/= |
| Kifungu (S02) | Uratibu wa Shughuli za Shughuli ya Uchaguzi Pemba | Sh. 189,979,000/= |
| | **Jumla ya Programu** | **Sh. 1,404,000,000/=** |
| | **Jumla ya Programu Kuu** | **Sh. 1,404,000,000/=** |

*(Vifungu vilivyotajwa hapa juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

*(Baraza lilirudia)*

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, najua minong'ono hiyo mnazungumzia kwamba utaratibu hautoi jasho.(*Makofi*)

**Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Fedha ya Wizara ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais bila ya mabadiliko sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako liyakubali Makadiro hayo. Naomba kutoa hoja.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Spika, naafiki.

**Mhe. Spika:** Sasa niwahoji basi Waheshimiwa Wajumbe, wale wanaokubaliana na makadirio hayo wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. (*Makofi*)

Katibu kuna jambo lolote. Waheshimiwa Wajumbe, Katibu ananambia orodha ya shughuli za leo ndio zimekwisha. Basi tusitishe shughuli zetu, maana ndio hazipo kwa sasa. Waheshimiwa Wajumbe basi nawashukuru sana kwa mashirikiano makubwa, tumepitisha Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mashirikiano makubwa sana, hiyo ni baada ya kazi nzuri ambayo Waheshimiwa, Watendaji pale juu, wenzetu wa Wizara ya Fedha, lakini hasa zaidi Waheshimiwa Wajumbe, lakini na Mawaziri ambao mmesaidia kutoa ufafanuzi uliokuwa wa uwazi kiasi cha kwamba hakukuwa na hoja.

Nachukua nafasi hii kuwashukuru wote kwa kazi hiyo nzuri. Basi baada ya hayo Waheshimiwa Wajumbe sasa niahirishe kikao hichi hadi kesho tarehe 22/05/2015 saa 3:00 za asubuhi.

*(Saa 1:17 za usiku Baraza liliahirishwa hadi tarehe 22/05/2015 saa 3:00 za asubuhi)*